



Kiigizo kisichokuwa na mfano

*Muhammad*  
*Mustafa* ﷺ

Othman Nuri TOPBASH

 **ERKAM**  
PUBLICATIONS



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Istanbul - 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

Kiigizo kisichokuwa na mfano

*Muhammad*  
*Mustafa* ﷺ

Othman Nuri Topbash

- Jina la Asili:** Emsalsiz Örnek Şahsiyet  
**Mwandishi:** Othman Nuri Topbash  
**Msimamizi Mkuu:** Abdi Mohamed Adam  
**Mfasiri:** Ibrahimu H. Kabuga  
**Mhariri:** Mohamed M. Potea  
**Msanifu jalada:** Altinoluk Graphics  
**Kupangiliwa vizuri na:** Sarkhan Isgandarov  
Nijat Garibov  
**ISBN:** 978-9944-83-669-2  
**Mchapaji:** Erkam Printhouse  
**Anuani:** Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi  
Mah. Atatürk Bulvarı, Haseyad  
1. Kısım No: 60/3-C Başakşehir,  
Istanbul, Turkey  
**Simu:** (+90-212) 671-0700 pbx  
(+90-212) 671-0748  
**Barua pepe:** info@islamicpublishing.org  
**Tovuti:** www.islamicpublishing.org  
**Language:** Swahili / Kiswahili



Kiigizo kisichokuwa na mfano

*Muhammad*

*Mustafa* ﷺ

Othman Nuri TOPBASH

Allah Mtukufu anamtambulisha  
Mtukufu Mtume ﷺ katika namna ifuatayo:

**“Nasi hatukukutuma ila uwe ni  
Rehema kwa walimwengu wote.”**

(Al – Anbiya: 107)



**“Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekutuma uwe  
shahidi na mbashiri na mwonyaji, Na mwitaji  
kumwendea Mwenyezi Mungu kwa idhini yake,  
na taa yenye kutoa nuru.”**

(Al-Ahzab: 45-46)



**“Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa  
Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji  
Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho,  
na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.”**

(Al- Ahzab: 21)



**“Na kwa hakika wewe una malipo yasiyo katika.  
Na hakika wewe una tabia tukufu.”**

(Al – Qalam: 3 – 4)



**“Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi  
Mungu, na mt'iini Mtume, wala  
msiviharibu vitendo vyenu.”**

(Muhammad: 33)



**“Na wenye kumt'ii Mwenyezi Mungu  
na Mtume, hao wa pamoja na wale alio  
waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa  
Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu  
wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!”**

(An – Nisa: 69)



**“Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika  
wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini!  
Msalieni na mumsalimu kwa salamu”**

(Al – Ahzab: 56)







## Utangulizi

Himidi na sifa njema za milele ni za Mola wetu Mtukufu kwa kutupa heshima ya kuwa katika *ummah* wa Muhammad Mustafa ﷺ aliyetukuzwa kuwa kipenzi cha Allah na taji tukufu la Mitume wote.

Rehma na salam za milele ziwe juu ya Mtume wetu ﷺ aliyebarikiwa, mwanga wa milele, ambaye shakhsia yake ya kipekee imetoa nuru isiyofifia ya muongozo na ukweli juu ya watu wote wanaotafuta njia yenye furaha ya milele.

Mwenyezi Mungu alimtuma katika kipindi ambacho binadamu alikuwa amekwama na kutatizika katika giza nene na akamfanya kuwa neema yenye faraja kwa walimwengu wote katika kipindi hicho ambacho dunia ilikuwa imezama katika bahari ya dhulma na giza.

Alimuinua kutoka katika anga za mbali kama nyota ing'aayo ikiangaza juu ya ulimwengu uliofunikwa na giza la ujinga wa jamii iliyokuwa ikiishi katika hali ya ukatili, unyama na mtawanyiko kuliko hata wanyamapori.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimtuma kuwa rehma ya milele kwa viumbe hai na visivyokuwa hai, kuanzia kwenye udongo na mawe mpaka mito na bahari. Alimleta awe baraka kwa mbingu na ardhi, awe baraka kwa kila mahali na kila



zama, hususan kwa wanadamu kama njia yao ya kupata wokovu, muongozo na rehma daima.

Yeye ni rehma ambayo, viumbe viliumbwa kwa heshima yake na viumbe hivyo hupata heshima mbele ya Mungu kulingana na mapenzi waliyonayo kwake.

Yeye ni rehma ambayo mbawa za huruma yake zimewae-neo binadamu na hata viumbe wote pia.

Yeye ni Rehma ambayo, Mola Mtukufu ameifanya kuwa chimbuko la milele lililojaa baraka na sifa za kipekee, na chemchem ya uhai kwa nyoyo zote zenye kiu.

Yeye ni Rehma ambayo, kupitia kwake Qur'an Tukufu na Muongozo wa milele ulipata kuteremshwa.

Yeye ni Rehma kwa sababu ndiye kipenzi zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu, na ndiye Mtume aliyepata baraka ya zawadi adhimu ya kupandishwa mbinguni, *Miraj*.

Yeye ni Rehma ambayo bila Yeye ulimwengu mzima ungegeuka kuwa jangwa la kutisha.

Yeye ni Rehma kwa sababu ulimwengu uliumbwa kwa nuru yake.

Yeye ni Rehma ambayo kila uzuri hutokana naye, na uzuri umeumbwa kwa ajili yake. Hakuna ua linalochanua pasipo nuru yake, kwani kama si kwa ajili yake kisingeumbwa chochote. Kwa ajili yake tumeumbwa. Yeye ni maua kutoa kwa Mungu yatokanayo na nuru iliyokamilika isiyofifia ambayo huzidi kuchanua na kutoa nuru kila wakati.



Yeye ni Rehma kwa sababu Mwenyezi Mungu Mwenyewe amekiinua cheo na hadhi yake kwa kumtakia rehma.

Chini ya paa la Utume wa Rehma hii ya kipekee ulimwengu wote ulipokea ladha na raha ya amani ya kweli. Binadamu ambaye wakati huo alikuwa katika hali ya kukosa hewa na kusongwa na pumzi kutokana na moshi wa uasi wake, akaweza kusafiri kuelekea anga za juu kupitia mlango wa hekima uliofunguliwa na Mtukufu Mtume ﷺ, na kuvuta hewa mpya ya uhai. Dhamiri zilizokuwa kama mawe magumu ziliyeyuka katika mikono yake mitukufu. Nyoyo zilizochafuliwa na taka na kutu zikatakaswa na chemchem yake tukufu na kuwa makazi safi ya upendo.

Wahshi, yule Mhabeshi, kabla ya kupokea muongozo alikuwa mtu katili anayeishi kwa damu za watu. Lakini baada ya kujisalimisha kwenye mafunzo matukufu ya Mtume ﷺ akawa sahaba mwenye moyo laini na mwenye kulia sana. Kuna wengine wengi kama yeye ambao kabla ya kuongoka roho zao zilikuwa zimekufa na kujeruhiwa vibaya na makucha ya uovu. Lakini baada ya kunywa katika chemchem hiyo ya uongofu wakaweza kupata uhai mpya na kupokea heshima ambayo itaandamana na majina yao daima.

Yote hayo yanaonyesha ukweli ndani na nje kwamba, Mtukufu Mtume ﷺ ndio kielelezo kikubwa zaidi cha muujiza ulioubwa na Allah ﷻ. Yeye ni mtakatifu na kipenzi zaidi kiasi kwamba wanahekima na mashujaa wote waliotokea katika uso wa ardhi ni madhihirisho tu ya Mtume ﷺ, ni sehemu ndogo sana ya kiigizo hicho adhimu na ni mbalamwezi



ambazo huakisi mwanga wa jua hilo lililoletwa kama tunu ya Rehema ya Allah kwa kila himaya ya viumbe.

Hivyo, njia ielekeayo kwa Allah ﷻ na radhi zake inapitia katika kumpenda na kumfuata Mtume ﷺ. Ukweli huu umebainishwa na Mwenyezi Mungu katika aya zifauatzo za Qur'an Tukufu:

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ  
وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ

“Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu.” (Ali Imran: 31)


مَنْ يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ وَمَنْ تَوَلَّى  
فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا


“Mwenye kumt’ii Mtume basi ndio amemt’ii Mwenyezi Mungu. Na anaye kengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao.” (An – Nisa: 80)


Hayo yaliyoelezwa ni ukweli ambao hakuna amuaminiye Mwenyezi Mungu anayeweza kuupuuza na kutoujali. Kama inavyosisitizwa na Qur'an katika aya hizo, kipimo pekee cha mtu kumpenda Allah ni kumfuata Mtume Wake ﷺ na kushikamana naye kama vipepo kwenye maua. Kinyume na




hivyo, *Imani* – kumuamini Allah na yale yote aliyotuteremshia – haiwezi kuwa na maana yoyote. Ni lazima kujua kuwa hakuna njia nyingine ya kumpenda Allah zaidi ya kumfuata Mtume; na bila kumpenda Mwenyezi Mungu matendo yetu yote yatakuwa bure.

Hivyo, siku zote lazima tumuweke Mtukufu Mtume  katikati ya nafsi zetu na ndani ya kiini cha nyoyo zetu na kuifanya shakhsia yake ya kipekee kuwa mjenzi wa shakhsia na tabia zetu.


Bila shaka ili kufanikisha jambo hilo, tunahitaji kumjua kiundani na kwa ukaribu zaidi mpaka pumzi zetu ziwe sawa na zake na mapigo ya nyoyo zetu yaende sambamba na mapigo ya moyo wake kama walivyokuwa Maswahaba watukufu waliokuwa wakimpenda sana Mtume .



Ingawa tuna nyoyo dhaifu na hatuwezi kumpenda Mtume  kwa kiwango kinachomstahiki, basi tukishikamana na njia ya kuelekea kwake itatosha kutupatia furaha na *saadah* ya hali ya juu na ya daima. Tukipata sehemu ya nuru ya tabia yake adhimu itatosha kutufungulia milango ya furaha ya milele.

Ni kwa sababu hii ya kutaka kuijua shakhsia tukufu ya Mtume  kwamba tumejaribu kuandika kitabu hiki, japokuwa kwa kutumia wino wenye mapungufu na udhaifu. Kitabu hiki ni muhtasari wa yale yaliyoelezwa katika vitabu vyetu vilivyotangulia kuhusu shakhsia tukufu ya Mtume watu mwenye baraka.

Maneno yetu, hata yawe na urefu kiasi gani, hayatoshi kuelezea vilivyo hadhi na cheo chake, bali tunawajibika kue-



lezea shukrani yetu kwa zawadi hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuzifafanua tabia na njia ya maisha yake na kuzilingiza katika maisha yetu. Jukumu letu kubwa, kulingana na uwezo wetu, ni sisi kuwa daraja la kubeba Rehma na amani yake isiyo na kikomo - iliyoenea ulimwengu wote – na kuipeleka katika zama zetu za sasa zinazokabiliana na tabu na shida za kila aina. Tunawajibika kuuwasilisha muujiza huu wa ajabu uliotoka kwa Mwenyezi Mungu na kuutambulisha kwa wanadamu wote kwa kadri ya uwezo wetu wa kuzungumza. Lakini hakuna shaka hata kidogo kwamba, heshima yetu kubwa itapatikana katika kumtambulisha Mtume  kwa namna iliyo bora ya kufuata matendo yake.

Tunamuomba Allah Mtukufu ampe kila mmoja wetu fungu na sehemu ya tabia njema ya Mtume  na azifanye nyoyo zetu kuwa makasri ya upendo kwa Mtume! Tunamuomba atujaalie mafanikio katika mtihani mgumu wa uchamungu unaohusu kumtii na kujisalimisha kwa Mtukufu Mtume  na kutubariki kupata upendo na radhi za Mwenyezi Mungu!

Amin...<sup>1</sup>



---

1. Ninamuomba Allah azifanye juhudi za wanafunzi wetu waliosaidia kuandaa kitabu hiki, ziwe sadaqatul jaria kwa ajili yao.

---



# *Sehemu Ya Kwanza*



✿ Kitgizo cha Kipekee

✿ Uswatul – Hasana / Ruwaza njema





## Shahsia Ya Kipekee Iliyokamilika: Mtume Muhammad Mustafa ﷺ

Kurasa za kitabu cha historia ya Mtume zilianza kufunguliwa kwa kuitambulisha Nuru ya Muhammad kwa binadamu wa kwanza, akiishuhudia mwenyewe alama ya Muhammad ﷺ ardhini. Ilielezwa kuwa, tokea mwanzo Nuru hii tukufu ilipita katika nasaba safi na tukufu ikaja kwa Abdullah mpaka kwa Aminah, Mwanamke aliyepata bahati ya kubeba mimba ya Nuru hii adhimu. Kisha nuru hiyo ikafika kwa mhusika wake wa kweli, Mtume ﷺ Mbora wa viumbe.

Mfumo unaoshangaza wa ulimwengu, uwepo wake unatokana na Nuru ya Muhammad ﷺ. Mtiririko wa maajabu ya uumbaji unaonekana katika ulimwengu na mikondo mbalimbali ya uzuri inayoonekana kwa uwazi ni kielelezo na dhidhirisho tu la Nuru hiyo. Kama ilivyodokezwa katika dondoo ya hadithi hapo chini, sababu pekee ya kukubaliwa kwa toba ya dhati ya Adam ﷺ ni kwa kuwa udongo alioumbiwa ulikuwa na chembe ya udongo wa Mtume ﷺ:

*“Mola wangu ... ninaomba msamaha wako kwa cheo cha Muhammad!” Adam ﷺ aliomba baada ya kutambua kosa lake alililofanya na kusababisha kufukuzwa peponi.*

*Allah akamuuliza: ‘Umemjuaje Muhammad haliyakuwa sijamuumba?’*



Adam ﷺ akasema: uliponiumba na kunipulizia Roho Yako, nilitazama juu na kuona kwenye nguzo za arshi yako pameandikwa **La ilaha ill'Allah Muhammad Rasulullah.** Hapo nikajua kuwa usingeliweka jina pembezoni mwa jina lako isipokuwa yule umpendaye zaidi kuliko viumbe wote.’

Allah akasema:

‘Umesema kweli, ewe Adam! Hakika yeye ni kiumbe nimpendaye zaidi! Hivyo niombe kwa cheo chake; na kwa kuwa umekwishafanya hivyo, nimekusamehe makosa yako. **Kama sio Muhammad, usingeumbwa.**”<sup>2</sup>

Kwa kutumia jina la Muhammad ﷺ kama njia ya kutubia, Adam ﷺ alipata msamaha wa Mwenyezi Mungu. Kisha Nuru hiyo ya Muhammad iliendelea na kuwekwa kwa muda kwa Nabii Ibrahim ﷺ, ambapo moto wa Namruudh ulibadilika kuwa baridi na salama. Nuru hiyo ilikuwa kama lulu iliyofungwa katika setiri ya Ismail ﷺ, ikasababishwa kuteremshwa kondoo kutoka mbinguni.

Kama inavyoweza kuonekana, hata mitume waliomba Rehma kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia jina lake. Kuna mitume kama Musa ﷺ aliyefikia hatua ya kuomba angalau awe katika *ummah* wake, ili tu achume baraka za kumfuata, kama inavyoelezwa katika hadithi iliyopokelewa na Qatadah ibn Numan ؓ:

“Siku moja Musa ﷺ aliomba akisema:



*'Mola wangu ... Katika mbao <sup>3</sup> ulizonipa, ninaona umetajwa umma bora uliotolewa kwa ajili ya watu, unaamrisha mema na kukataza mabaya. Basi, Ee Mola wangu, ufanye umma huo uwe wangu!'*


*Allah Mtukufu akasema: **'Huo ni umma wa Ahmad.***

*Musa akaomba tena akisema: 'Mola wangu ... Katika mbao hizi ninaona umetajwa umma wa mwisho kudhihiri ardhini lakini umefanywa kuwa wa kwanza kuingia Peponi. Basi, naomba umma huo uwe umma wangu!'*

*Mwenyezi Mungu akamjibu akisema: **'Huo ni umma wa Ahmad'.***

*'Mbao hizi zinataja umma ambao maandiko yao yapo nyoyoni mwao na kuyasoma, wakati ambapo wale waliokuwa kabla yao walikuwa wakisoma kwa kutumia maandiko yao yaliyokwishaandikwa na pale yanapoondolewa hawayakumbuki tena. Umeupa umma huu uwezo wa kuhifadhi ambao haukupewa umma wowote kabla yao. Hivyo, naomba huo uwe umma wangu!'*

*Mwenyezi Mungu akamjibu tena: **'Huo ni umma wa Ahmad.'***

*Musa  akaendelea kuomba: 'Mola wangu kuna umma umetajwa, ambao huamini yale yaliyoteremshwa kwao na yale yaliyoteremshwa kabla yao. Wanakabilia na kila aina ya upotofu na ulaghai wa Dajjal mwenye jicho moja. Mola wangu, naomba huo uwe umma wangu'*



Mwenyezi Mungu akasema: **‘Wao ni umma wa Ahmad’.**

‘Mola wangu, Mbao hizi zinautaja umma unaopewa thababu kwa mtu kukusudia kufanya jambo jema hata kama hatolifanya, na iwapo wakilifanya wanapewa kuanzia thababu kumi mpaka mia saba. Nakuomba ufanye kuwa umma wangu!’

Mwenyezi Mungu akamjibu tena: **‘Huo ni umma wa Ahmad’.**

Hapo Musa ﷺ aliziweka pembeni mbao hizo alizokuwa amezibeba na kuanza kuomba:

‘Basi Mola wabgu, nifanye niwe katika watu wa umma wa Ahmad!’<sup>4</sup>

Hivyo kila mzunguko katika nyororo ya Mitume Watukufu ﷺ ilikuwa ikitoa bishara njema ya ujio wa Muhammad Mustafa ﷺ aliyetumwa kuwa rehma kwa Walimwengu wote.

Hatimaye, tarehe 12 Rabiul – awwal, mwaka 571, Nuru iliyokuwa ikisubiriwa ikawasili ulimwenguni, kupitia ndoa tukufu ya Abdallah na Aminah, ili kuipa heshima kila zama na kila mahali.

Kwa kuwasili kwake, rehma ya Mwenyezi Mungu ilienea na kujaa ulimwengu mzima. Rangi za usiku na mchana zilibadilika. Furaha za nyoyo zikaongezeka, ladha zikabadilika na kila kitu kikapata maana tofauti pamoja na uzuri mwingine.

4. Tabari, Jamiul Bayaan an tawilil Qur’an, Beirut 1995, IX, 87 – 88; Ibn Kathir, Tafsirul Qur’anil Adhiim, I – V, Beirut 1988, II,259, (Tafsiri ya surah Al A’raf 154).



Masanamu yalidondoka na kukatika vipandevipande. Nguzo kubwa na minara ya makasri ya kifakhari ya Madain, himaya ya Wafalme wa Uajemi, zikaanguka. Ziwa Sawa lililokuwa likitukuzwa na jamii ya kijahiliya likakauka. Nyoyo zilijawa na baraka na neema zilizoenea ulimwenguni kote, yaani kila wakati na kila mahali.

Lau kama Mtukufu Mtume ﷺ – ambaye ni mfano halisi wa wema – asingedhihiri katika ulimwengu huu, binadamu wangebaki katika mateso na unyama mpaka siku ya mwisho, wanyonge wangeendelea kuwa mateka wa watu wenye nguvu. Shari ingeishinda kheri na dunia ingetawaliwa na madhalimu na waonevu. Hali hiyo imeelezwa vizuri na mshairi mmoja katika tungo zake akisema:

*“Ewe Mtume wa Mungu, lau usingekuja,  
Maua yasingechanua,  
Kurumbizi (ndege) wasingeimba,  
Majina yasingejulikana kwa Adam na yangebaki bila  
maana,  
Viumbe wangezama katika huzuni.*

Maulan Rumi, Sauti ya ukweli ﷺ, anaeleza ni kwa kiasi gani tunapaswa kumshukuru kwa dhati Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye alitumia muda wa maisha yake yote katika kuvumilia tabu na shida nzito katika kuyavunja masanamu na kuondosha dhulma:

*“Enyi mnaofurahia kuwa Waislamu; tambueni kuwa  
kama si juhudi kubwa ya Bwana wetu Ahmad ﷺ, na hima*



*yake katika kuyavunja masanamu, nawe ungekuwa ukiabudu masanamu kama wahenga wako walivyofanya”.*



Mtu huyu ambaye “hakusoma wala kuandika” na ambaye alitokea katika jamii ya kijahiliya isiyokuwa na ustaarabu, sio tu kwamba aliwashangaza watu wa zama hizo kwa elimu na maarifa yake, bali pia alikuja na muujiza ambao hakuna aliyeweza au atakayeufikia mpaka siku ya mwisho. Muujiza huo ni Qur’an Tukufu.

Qur’an Tukufu imezungumzia mambo mengi ya kihistoria yaliyotokea zamani na yatakayotokea, pamoja na kuzungumzia mambo mengi ya kisayansi na ya kijamii, ambapo ni zaidi ya miaka 1400 iliyopita na mpaka sasa hakuna ugunduzi wowote ulioweza kukanusha yaliyoelezwa na kitabu hicho kitukufu. Kinyume chake tunaona kuwa hata insaiklopedia maarufu zaidi ulimwenguni leo hii kila mwaka hulazimika kusahihishwa na kuboreshwa kwa kuchapisha jozi za maneno ya ziada.

Mtume huyo yatima na ambaye hakuwahi kusoma wala kuandika, hakuwahi kusoma kwa mwalimu yeyote wa kibinadamu, lakini alithibitika kuwa mwokozi wa wanadamu, mkalimani wa ulimwengu wa siri na mwalimu mkuu wa shule ya Ukweli.

Nabii Musa ﷺ alikuja na sheria. Nabii Dawud alikuwa mahiri katika maombi na dua alizofunuliwa na Allah ﷻ. Nabii Issa ﷺ alitumwa kuwa mfano halisi wa wema na uchaji. Mtume Muhammad Mustafa ﷺ alikuja na hayo yote. Alifundi-



sha sheria na wakati huohuo akafundisha usafi wa moyo na jinsi ya kumuomba Mwenyezi Mungu kwa moyo safi. Aliwafundisha tabia njema na akawa kielelezo cha tabia hizo katika maisha yake. Akawausia kutohadaika na mambo ya dunia yenye kuondoka. Kwa ufupi, alikusanya kazi na majukumu ya Mitume wote waliomtangulia. Alikusanya nasaba na matendo matakatifu pamoja na uzuri na ukamilifu uliotukuka.

Aliishi miaka arobaini katika jamii ya kijahiliya, kipindi ambacho mambo mengi mema aliyokuja kuyatangaza baadaye yalionekana kuwa ya ajabu na mageni kwao. Hakuwahi kuwa kiongozi wa dola. Hakuwa akijulikana kuwa mfasaha wa kuongea. Hakuwa akijulikana kuwa askari wa kawaida achilia mbali kuwa kamanda mkubwa.

Lakini bila shaka, mwaka wa arobaini wa maisha yake ulithibitisha kuwa ni mtu muhimu sana katika historia yote ya binadamu.

Kabla ya hapo hakuna aliyemsikia akizungumzia historia ya watu na mitume waliotangulia, au kuzungumzia pepo na moto. Alikuwa akiishi maisha yenye staha na tabia za hali ya juu. Lakini baada ya kurudi kutoka katika pango la Hira, mahali alipokabidhiwa jukumu hili kutoka kwa Allah, mambo yote yakabadilika kabisa.

Aliipoanza mahubiri yake, Arabia yote ilipatwa na mshitungo na mshangao mkubwa, wakivutiwa na kustaajibishwa na ufasaha wake. Ghafla mashindano yao ya ushairi na fasihi yakawa hayana maana. Ikawa hakuna anayethubutu kutundika juu ya kuta za Kaaba mashairi yake yaliyoshinda katika mashindano. Huo ukawa mwisho wa utamaduni huo wa kale,



kiasi kwamba dada wa mshairi maarufu aitwaye Imrul – Qays aliposikia aya ya Qur'an isemayo:

وَقِيلَ يَا أَرْضُ ابْلَعِي مَاءَكِ وَيَا سَمَاءُ أَقْلِعِي  
وَوَغِيضُ الْمَاءِ وَقُضِيَ الْأَمْرُ وَاسْتَوَتْ عَلَى الْجُودِيِّ  
وَقِيلَ بُعْدًا لِلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ

“Na ikasemwa: Ewe ardhi! Meza maji yako. Na Ewe mbingu! Jizuie. Basi maji yakadidimia chini, na amri ikapitishwa, na (jahazi) likasimama juu ya (mlima) wa Al Juudiy. Na ikasemwa: Wapotelee mbali watu walio dhulumu!” (Hud, 11: 44)

Akasema: “Hakuna awezaye kutamka chochote. Hakuna faida ya kuzitundika tungo za kaka yangu kwenye kuta za Kaabah, kwa sababu hakuna faida yoyote sasa kwa mshairi yeyote kujigamba”. Kwa haraka sana akazishusha tungo za kaka yake Imrul – Qays zilizokuwa zimetundikwa mwanzoni kabisa mwa kuta za Kaabah kisha zikafuatia tungo nyingine saba za Muallaqat, moja baada ya nyingine.<sup>5</sup>

Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwafundisha wanadamu wote maana ya kweli ya binadamu kuwa Khalifa wa Mwenyezi Mungu duniani. Akaweka misingi bora zaidi katika nyanja zote za maisha, kama vile kanuni za kijamii, utamaduni, uchumi, utawala na mahusiano ya kimataifa. Misingi ambayo wasomi

5. Ahmad Jawad Pasha, Kisasul – Anbiya wa Tarikhul- Khulafaa, Istambul, 1976, I, 83.





bora hawakuweza kuijua hekima yake mpaka baada ya kufanya utafiti mkubwa uliogharimu kipindi chote cha maisha yao, na baada ya kufanya uhakiki wa ndani kuhusu watu na vitu. Ni hakika kuwa, kadri binadamu anavyopiga hatua katika nyanja ya maarifa ya kinadharia na uhakiki wa kisayansi ndivyo ana-  
vyezidi kuutambua **“Ukweli wa Muhammad”**.

Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye hapo kabla hakushiriki katika vita isipokuwa mara moja tu ambapo alikuwa kama shuhuda pasipo kushika upanga mkononi mwake, akaja kuwa kamanda hodari bila kupitia mafunzo yoyote ya kijeshi na askari shujaa na jasiri asiyerudi nyuma katika mapambano ya lazima katika kuipigania *tawhid* na kuimarisha amani ya kijamii, pamoja na huruma pana kwa watu wote.

Alikuwa akiwahubiria watu dini ya Allah nyumba kwa nyumba, lakini wale wenye bahati mbaya ndio walioukataa uongofu wake wakamfungia milango na kuikataa nuru yake isiwafikie na hivyo wakabaki katika giza nene. Baadhi yao, kwa sababu ya ususuavu na ugumu wa nyoyo zao, walimtendea ubaya na wakaamiliana naye kwa ukaidi. Lakini Mtume ﷺ hakujali ukaidi wao, badala yake aliwahuzunikia na kuwasikitikia kwa ujinga wao wa kutojali. Mara zote alikuwa akiwaambia watu kama hao:

**“Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu”**. (Sad, 38: 86) akiwatanabahisha kuwa yeye hat-  
aki chochote zaidi ya radhi za Allah tu.

Katika kipindi kifupi cha miaka tisa aliweza kupata ushindi na kuifungua Peninsula yote ya Arabia akiwa na robo tatu zaidi ya ukubwa wa jeshi la maadui na kwa hasara ndogo



ya watu kwa pande zote mbili. Kwa kupandikiza nguvu ya kiroho na mafunzo ya kijeshi kwa kundi la watu wa kawaida wa enzi hizo kulimpatia ushindi wa ajabu katika harakati hizo, kiasi kwamba wale waliokuja baada yake waliyashinda mataifa makubwa mawili yaliyokuwa na nguvu sana wakati huo, yaani Warumi na Wafursi.

Licha ya mazingira yote magumu, aliweza kuleta mapinduzi makubwa katika historia ya binadamu, na akayafuta machozi ya muda mrefu ya wanyonge. Mikono yake mitukufu ilikuwa chanuo katika vichwa vya yatima. Nuru ya huruma yake ikaziondoa huzuni nyoyoni mwao.

Mshairi wa kituruki, Mehmed Akif, anaelezea jambo hili kwa maneno ya kuvutia akisema:

*Pindi yatima huyo alipokuwa na kufikia miaka arobaini,  
Nyayo zenye kuvuja damu na kutembea juu ya  
vichwa zikasafika,  
Mtakatifu huyo aliwakomboa wanadamu kwa pumzi ali-  
yoyitawanya nyoyoni mwao,  
Kwa pigo moja aliwashinda na kuwaangamiza Kaisari  
na Khosrou,  
Aliwaokoa wanyonge ambao hawakuwa na haki isipoku-  
wa uduni na madhila,  
Udhalimu haukuwa ukiwaza hata kidogo kwamba utak-  
ufa na kuondoka,  
Sheria yake ya wazi ikawa rehma kwa walimwengu,  
Akazitandaza mbawa za rehma kwa wale wanaotafuta  
haki na uadilifu,  
Kila ilichonacho dunia ni zawadi yake,*



*Mtu mmoja mmoja na jamii yote ni wadeni wake,  
Binadamu wote ni wadeni wa Mtume huyo Mtakatifu,  
Ewe Mola wetu Mtukufu tufufue siku ya kiama tukiwa  
na fikra hii vichwani mwetu.*



Utume wa Bwana wetu Muhammad Mustafa ﷺ ni kama bahari pana isiyo na mipaka, na Mitume wengine ni kama mito itiririkayo ndani ya bahari hiyo. Alikusanya sifa zote za ukamilifu za mitume waliokuja kabla yake wapatao laki moja na elfu ishirini na nne (124,000) sifa zilizokuwa katika kilele cha maadili na tabia njema. Ukijumuisha maaendeleo waliyopata wanadamu katika zama zake katika uwanda wa fikra na maisha, Shakhisia yake ni “mfano wa kuigwa” unaoweza kukabiliana na mahitaji ya binadamu yanayoweza kutokea mpaka siku ya kiyama. Kwa sababu hiyo alitumwa kwa watu wote kama “**Nabii wa zama za mwisho**”.

Hivyo Mtume ﷺ akizungumzia tabia zake za hali ya juu alisema:

*“Hakika mimi nimetumwa kuja kukamilisha tabia njema”*  
(Muwatta Husnul-khuluq)

Kwa hakika yeye hakuacha baada yake mali yoyote ya kidunia bali aliwaachia wanadamu wote urithi bora zaidi na mtukufu, nao ni shakhisia na tabia zake za maadili matukufu.



## Uswatul-Hasanah / Mfano Bora Uliokamilika

Mtume Muhamad Mustafa ﷺ ndio mtume na binadamu pekee ambaye historia ya maisha yake imeandikwa kwa upana na kwa undani. Kwa hakika ni katika ukamilifu wa mitume kwamba ni viigizo vizuri katika kumwelekeza mwanadamu kwenye haki na kheri. Lakini mienendo na matendo yao katika zama hizi yamebaki kwa kiwango kidogo sana. Ama kuhusu Mtume wetu wa zama za mwisho ﷺ, historia ya maisha yake imeandikwa hatua kwa hatua kwa namna inayopakisi matendo na maneno yake kuanzia yale madogomadogo mpaka yale makubwa makubwa na yenye ukamilifu wa hali ya juu. Historia ya maisha yake imeendelea kutunzwa kama urithi wa thamani katika historia.

Mbali na hilo matendo na maneno yake yameendelea kuwepo kwa baraka na fadhila za Allah Mtukufu na yataendelea kubaki na kumfikia mwanadamu wa mwisho atakayekuja kabla ya siku ya mwisho.

Ili tuweze kushinda katika kukabiliana na mitihani mbali mbali ya maisha tunatakiwa kuwa na imani na Mwenyezi Mungu, kuiridhia kadari, kuwa na subira, ujasiri, kujitoa muhanga, kutosheka moyoni na kuwa na msimamo madhubuti katika kukabiliana na matatizo mbalimbali. Mwalimu



bora (Murshidul-kamili) katika kutekeleza hayo mema yote kama mfano halisi na kielelezo kamili ni Mtume Muhamadi Mustafa ﴿﴾ aliyetumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kama zawadi kwa wanadamu.

Maisha ya Mtume ﴿﴾ ni mfano bora uliotukuka kwa vizazi vyote vijavyo mpaka siku ya mwisho. Qur'an Tukufu inamzungumzia ikisema:

**“Na kwa hakika wewe una malipo yasiyo katika. Na hakika wewe una tabia tukufu”.** (Al – Qalam, 68: 3 -4)

Maisha na tabia tukufu ya Mtume ﴿﴾ ni kilele cha mwenendo wa mwanadamu, hata mwelekeo wa tabia zake za nje zinazoweza kueleweka vizuri kwa mwanadamu. Mtume huyu ambaye ni mnara wa Mitume na kielelezo cha tabia ya binadamu aliyekamilisha kazi yake katika jamii kwa kuweka mifano bora ya kuigwa, aliletwa na Allah Mtukufu kwa wanadamu awe kama *Uswatul – Hasanah* (kiigizo chema). Qur'an Tukufu inabainisha ukweli huu kwa kusema:

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ  
يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا

**“Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anayemtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.”**

(Al – Ahzab, 33: 21)

Katika hatua zote za maisha, Mtume ﴿﴾ anatoa ukamilifu naong'aa ili macho yote yauone, huku akitoa kila aina ya



matendo bora, kwa namna ya jumla au kwa undani zaidi. Hivyo, katika maisha ya Mtume ﷺ na *Sunnah* zake Tukufu, kila mtu anaweza kupata mfano bora na uliokamilika wa kuufuata.

Mtume Muhammad Mustafa ﷺ ni kiongozi wa dini na ni mkuu wa dola. Yeye ni mfano halisi kwa wale wanaoingia katika bustani la mapendo ya Mungu, lakini haachi kushukuru na kunyenyekea pale anapojazwa baraka na neema za Allah.

Kama alivyo mfano wa subira na kumtegemea Mwenyezi Mungu katika nyakati ngumu, ndivyo alivyo mfano wa ukarimu na kujinyima wakati anapopata ngawira. Yeye ni mfano wa huruma kwa familia yake, vivyo hivyo ni mwenye huruma sana kwa watumwa, wanyonge na wasafiri. Ni mwenye roho nzuri na ukarimu mkubwa kwa wale wanaomkosea.

*Hivyo, kama wewe ni tajiri, basi tafakari juu ya unyenyekevu na ukarimu wa Mtukufu Mtume ﷺ aliyemitawala Arabia yote na akawavuta waarabu wote kwa moyo wa upendo...*

*Kama wewe ni miongoni mwa wanyonge, jifunze namna alivyoishi Mtume mjini Makka chini ya utawala kandamizi wa washirikina. ...*

*Kama umepata ushindi, fikiria juu ya Mtume mwenye ujasiri na kuridhika ambaye, aliwashinda maadui katika vita vya Badr na Hunayn ...*

*Lakini – Mungu aepushie mbali – kama utashindwa, mkumbuke Mtume ﷺ aliyekuwa akitembea kwa uvumilivu baada ya kujeruhiwa na akiwa amewapoteza masahaba zake katika vita vya Uhud katika kutekeleza maagizo ya Mwenyezi Mungu ...*



*Kama wewe ni mwalimu, mfikirie Mtume ﷺ alivyokuwa laini wa moyo, msikivu na mvumilivu katika kufikisha lulu za moyo wake kwa wanafunzi wa Suffa katika msikiti wake (Masjidun – Nabawi)...*

*Kama wewe ni mwanafunzi, vuta picha ya Mtume ﷺ akiwa amekaa mbele ya Jibril ﷺ kwa adabu, usikivu na shauku kubwa akiwa amemletea wahyi...*

*Kama wewe ni mtoa mawaidha au mhubiri unayewaita watu kwenye mambo mema, basi isikilize sauti tamu ya Mtume ﷺ akitoa cheche za hekima kutoka moyoni mwake kwenda kwa masahaba msikitini ...*

*Kama huna mtu wa kukutetea na kukusaidia kuenzeza neno la haki na kuliinua, basi mtazame Mtume ﷺ aliyetangaza neno la haki kwa watu wajinga na kuwaita kwenye uongofu katika kipindi ambacho alikuwa hana msaada wowote mjini Makka...*

*Kama umeivunja ngome ya maadui, ukawadhoofisha na kuuangamiza uovu kwa lengo la kutangaza haki, basi uvute mbele ya macho yako muonekano wa Mtume ﷺ siku ya ushindi wa Makka akitembea kwa unyenyekevu hali ni mwenye kushukuru, akaingia katika ardhi takatifu ya Makka akiwa juu ya ngamia kana kwamba anataka kusujudu kutokana na kunyenyekea licha ya kuwa ni kamanda aliyekuwa amepata ushindi ....*

*Kama unamiliki shamba na ukataka kuratibu mambo ya shamba lako, jifunze kwa Mtume ﷺ alipofanya uteuzi makini wa mtu anayeweza kumudu na kuendesha mashamba ya Banu*



Nadir, Khaybar na Fadak baada ya kuyaweka chini ya himaya yake ...

Kama wew ni mpweke, mfikirie yatima mtakatifu aliyekuwa kipenzi cha Abdullah na Aminah ...

Kama wewe ni kijana, yatafakari kwa undani maisha ya kijana huyu, aliyetarajiwa kukabidhiwa jukumu la Utume, akichunga kondoo wa Abu Talib mjini Makka ...

Kama wewe ni mfanyabiashara unajiandaa kutoka na mizigo ya bidhaa, tafakari juu ya uaminifu wa mtu mtukufu zaidi alivyotoka na msafara wa biashara kuelekea Yemen na Damascus ...

Kama wewe ni hakimu, kumbuka uadilifu na busara za Mtume ﷺ katika kuamua kadhia ya kuweka jiwe jeusi kwenye ukingo wa Kaaba na kuepusha mauaji ambayo yangetokea ...

Yageuze macho yako tena kwenye historia na mtazame Mtume ﷺ kwa mara nyingine akiwa amekaa katika msikiti wa Madina akitoa hukmu mbalimbali katika namna ya uadilifu wa hali ya juu na kutenda haki sawa baina ya maskini dhaifu na tajiri mwenye kuheshimika ...

Kama wewe ni mume, fikiria hisia ya upendo na huruma kubwa aliyokuwa nayo mume mtukufu wa Bibi Khadija na Bibi Aisha ﷺ...

Kama wewe una watoto, jifunze mwenendo mzuri wa baba yake Fatimah, babu wa Hassan na Husayn ...

Sifa yoyote utakayokuwa nayo, na mazingira yoyote yale yatakayokukabili, utamkuta Muhammad Mustafa ﷺ akiwa





*kama mwalimu kamili na muongozo wako mzuri kila wakati na kila mahali.*

Ni mwalimu ambaye mtu anaweza kusahihisha makosa yake yote kwa kufuata Sunnah zake na hatimaye akaweza kurejesha kila kitu mahali pake na kurekebisha nguvu na juhudi zilizopotea.

Kwa kufuata nuru ya muongozo wake unaweza kuondoa vizuizi katika njia yako na kujikuta umeifikia milango ya furaha ...

Kwa hakika, ulimwengu wa ndani wa Mtukufu Mtume ﷺ ni bustani bora sana kuliko bustani ya peponi iliopambwa maua mazuri na mawaridi yenye kutoa harufu ya miski.

Hivyo ni dhahiri kwamba Maisha ya mtume ﷺ yanaendelea kuwa mfano bora kabisa uliokamilika hata kwa wale walio katika maisha ya kawaida. Kwa mfano, maisha ya aliyehukumiwa hayawezi kuwa mfano kwa hakimu, kama ambavyo hakimu hawezi kuwa mfano kwa aliyehukumiwa. Vivyohivyo, maskini aliyetumia umri wke wote kutafuta kitu cha kushibisha tumbo lake akiwa ametopea katika dibwi la umaskini hawezi kutoa mfano kwa tajiri anayeogelea katika mali. Lakini misha ya Mtume ﷺ yanatoa mfano kwa pande zote mbili, kwa sababu Mwenyezi Mungu alimfanya mtume ﷺ aanze kuwa “**Yatima**” ambaye ni kielelezo cha hali ya chini katika jamii ya binadamu. Kisha akawa anapanda kupitia hatua zote za maisha mpaka akafika kwenye kilele cha juu cha nguvu na madaraka, yaani utume na ukuu wa dola. Kila hatua katika maisha ya Mtume ﷺ inatoa miongozo na mienendo mingi inayofaa kufuatwa na kila kundi la jamii katika maisha ya mwanadamu.



Hivyo maisha yake, vyovyote mtu atakavyokuwa katika maisha, yatakuwa ni mfano halisi na kamili ambao unaweza kuigwa na binadamu wote kila mmoja kulingana na uwezo wake.

Mbali na mitume na watu wema waliofuata njia yao kila aliyejidai kuwa anaweza kuwaonyesha wanadamu njia ya uokovu na kudai kuwani kiigizo kwa watu wengine, hasa wanafalsafa waliojaribu kuelezea kila kitu kwa kutumia akili zao zenye kikomo na ufahamu wao finyu wameshindwa katika uwanda huu. Kwa kuwa Mitume walikuwa wakiungwa mkono na ufunuo wa Mwenyezi Mungu wote walikuja kama miongozo ya haki na kila mmoja alimthibitisha mwenzake. Kila mmoja alifikisha sheria alizotumwa na Mwenyezi Mungu. Siku zote walikuwa wakisema “Mwenyezi Mungu anasema hivi au ameamuru hivi”.



Kwa hivyo, wanafalsafa pamoja na kwamba walilenga kuwaongoza watu kwenye njia ya haki, kutokana na kutoungwa mkono na Mwenyezi Mungu, kutokana na kufikiri mambo kwa akili zao finyu na zenye ubinafsi, walikuwa wakitoa sheria zao kulingana na rai zao na kusema: “Hii ndio rai yangu au ninaona hivi” Matokeo ya mgongano huo tunawaona baadhi yao wakibatilisha nadharia za wenzao na wengine kuwakadhibisha wengine. Kwa sababu hiyo, hawakuweza kujiongoza wala kuziongoza jamii zao.

Kwa mfano, Aristotle, pamoja na kuweka msingi wa kutumia sheria za falsafa ya maadili hakuwa mwenye kuungwa mkono kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hivyo hakuweza kupata mtu hata mmoja anayeiamini falsafa yake au aliyepata



furaha kwa kuitekeleza falsafa hiyo. Sababu ya hali hiyo ni kwamba wanasfalsafa hao hawakuwa wasafi, hawakuzitakasa nafsi zao na kukamilika kwa kusaidiwa wahyi (ufunuo).

Njia pekee inayoweza kumuokoa binadamu dhidi ya shida zinazoletwa na matakwa ya kiakili na mielekezo ya kinafsi ambayo haikulelewa na wahyi ni Qur`au tukufu. Qur`an ndio kamba madhubuti ambayo Allah aliitoa kama zawadi kwa wanadamu pamoja na mtume huyu wa zama za mwisho. Vielelezo vya kimatendo na vya ukweli vilivyopo ndani ya Qur`an vinaonekana wazi katika histori yenye ustawi ya Mtume Muhammad ﷺ. Hivyo matendo mengi ya dharura na ya lazima sana ambayo binadamu wanatakiwa kuyafanya ili kutekeleza lengo la kuumbwa kwao wanatakiwa kuyatenda kwa mujibu wa Qur`an na sunnah. Qur`an na sunnah ni ponyo ya kupata furaha ya maisha ya dunia na Akhera, na ni kumbukumbu ya milele ya Nuru ya viumbe, Mtume Muhammad ﷺ, ambaye ametuachia nguzo hizo mbili zenye thamani.

Kabla ya kuanza kazi yake ya utume, Mtukufu Mtume ﷺ aliwavuta watu kwa tabia njema za hali ya juu zilizowafanya watu wote wamkubali na kumpa jina la “Mkweli, Mwaminifu”. Ni baada tu ya uthibitisho huu ndipo kazi ya mahubiri ilipoanza.

Tangu mwanzo walikuwa wakiujua kikamilifu mwenendo mwema na ukamilifu uliotukuka wa Mtume ﷺ na hivyo walimtumainia sana. Walipozozana kuhusu uwekaji wa jiwe jeusi kwenye Kaaba wakati wakiikarabati na kukaribia kupigana, walimteua kuwa msuluhishi wao na wakakubaliana na hukmu na uamuzi wake bila kupinga.



Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa mashuhuri sana kwa uamini-fu wake kiasi kwamba hata Abu Sufiyan, aliyekuwa adui yake kipindi hicho, alipoulizwa na Heraclius, mfalme wa Rumi, kuhusu iwapo kuna wakati ambapo Mtume ﷺ hakutekeleza ahadi zake. Abu Sufiyan hakuwa na chaguo jingine zaidi ya kujibu kwa kusema:

“Hapana ....Hutimiza kila ahadi anayoiweka”. (Bukhari, Bad’ul – Wahy 6, Salat 1, Sadaqat 28; Muslim, Jihad 74)

Ushahidi mwingine unaoonyesha kiasi gani Waarabu wa kabla ya Uislamu walimuamini Mtume ﷺ ni maneno ya Abu Jahl, adui mkubwa wa Mtume, pindi yeye na wenzake walipomwambia:

“Ewe Muhammad, naapa kwa Mungu kwamba, sisi hatu-kupingi wewe ... kwani kwetu wewe ni mtu mwaminifu na mwenye kuheshimika. Sisi tunapinga kile ulichokuja nacho!”

Kuhusu jambo hilo, Qur’an Tukufu inasema:


**“Tunajua ya kwamba yanakuhuzunisha wanayo yas-ema. Basi hakika wao hawakukanushi wewe, lakini hao madhaalimu wanazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu”** (Al – An’aam, 6:33)<sup>6</sup>


Hata maadui zake wakubwa walikuwa wakijua nyoyoni mwao kuwa Muhammad ﷺ ni mtume wa kweli, huku wakim-kataa kwa sababu ya matamaniao ya nafsi zao.


---

6. Wahidi, Asbaabu Nuzuulil – Qur’an, chapa ya Kemal Besyun Zaglul, Beirut 1990, uk. 219.





Tukio jingine linaloangazia sababu ya Nuru hii ya viumbe  kupewa jina la *Al – Amin* (mwaminifu) hata kwa na maadui zake ni hili lifuatalo:


Wakati vita vya Khaybar vikiendelea, mchungu kondoo mmoja kutoka safu za Wayahudi aitwaye Yasar alikuja kwa Mtume  na baada ya mahojiano mafupi alielezea hamu yake ya kutaka kuingia katika Uislamu.

Mtume  alimkubalia lakini akamtaka kwanza arejeshe kondoo kwa wamiliki wake. <sup>7</sup>

Tukio hili lilitokea katika kipindi ambacho ukomo wa muda na ufinyu wa vifaa vya matumizi ulikuwa umeanza kuitoka kutokana na hali ya hatari na wasiwasi miongoni mwa safu za waislamu. Bila shaka hatua hii inatoa dhihirisho la waziwazi la umuhimu wa uwajibikaji, mwamko wa dhima na utunzaji wa amana hata katika nyakati ngumu.

Ama kwa upande wa kufaidika zaidi na mwenendo mwema na maadili ya mtukufu Mtume  ni pale mtu atakapofikia daraja ya utu aliofikia Abu Bakr  iliyobainishwa na maelezo yake kuhusu miraji pale aliposema:

“Kama amesema amekwenda huko, lazima itakuwa ni kweli!”

Vielelezo visivyokuwa na idadi kuhusu uadilifu, upole na huruma ndani ya maisha ya Mtume  ni mambo halisi yanayotakiwa kuigwa na kufuatwa na ulimwengu mzima mpaka siku ya mwisho. Jicho lolote lisilokuwa na chuki ambalo lime-

7. Ibn Hisha, *Siratun – Nabi*, Beirut 1937, Darul- Fikr, III, 397 – 398; Ibn Hajar, *al – Isaba*, Beirut 1328, Daru Ihyaith – Turathil – Arabi, I, 38 – 39.



furahia fadhila ya kuitazama nuru ing'aayo inayotokana na Taa hiyo bora haliwezi kupinga ukweli hata kama itaendelea kufichwa ndani ya dhamiri zao. Wasomi wengi wa kimagharibi waliolazimika kuukubali ukweli wake licha ya kuendelea kuwa makafiri, wametoa sauti ya nyoyo zao kuutambua mwenendo na mafanikio ya Mtukufu Mtume ﷺ. Miongoni mwa wasomi hao ni Thomas Carlyle anayeelezea mazazi ya Mtume ﷺ kama

“Kufunguka kwa nuru kutoka kwenye giza”.

Ikidhibitisha mwenendo wa mtukufu Mtume ﷺ Insaiklopedia Britanica inaeleza yafuatayo:

“Katika historia nzima ya binadamu hakuna Mtume wala mwanamageuzi aliyekaribia mafanikoa ya Muhammad”.

Maelezo kama hayo yanayotolewa na B.Smith:

“Hakuna shaka hata kidogo kwamba watu wote wanakubali Muhammad ndiye mwanamapinduzi mkubwa zaidi”.

Mwandishi Stanley Lane-Polo anaungama na kukiri kwa kusema:

“Siku Muhammad alipopata ushindi mkubwa dhidi ya maadui zake ndio siku ambayo pia nafsi yake ilipata ushindi wa mwenendo wake.


Kwa sababu siku alipoitwaa Makka, aliwaacha huru Maquraishi bila lawama, akionyesha huruma kubwa ilioacha athari kwa jamii nzima ya Makka. Ungamo kama hilo limefanywa na mwandishi Athur Gilman: “Tumeshuhudia ukuu wake wakati alipoitwaa Makka. Athari za aliyokuwa amefanyiwa zamani zingechohea moyoni mwake hisia za kulipa kisasi. Lakini badala yake Muhammad alizuia jeshi lake lisimwage hata tone




moja ya damu. Kitu pekee alichofanya ni kumshukuru Mwenyezi Mungu, akionyesha huruma kubwa kwa watu hao”.

Utafiti wa kina uliofanywa kuhusu mifano mbalimbali ya kisheria kabla ya kutolewa kwa Tangazo la haki za binadamu, ulimhamasisha La Fayette, Mwanafalsafa anaejulikana kuwa miongoni mwa watu walioanzisha mapinduzi ya ufaransa ya mwaka 1789, akatangaza waziwazi kuutambua ukuu wa sheria ya kiislam:

“Ewe Muhammad mwenye utukufu....! Umefika kwenye kilele cha hali cha uadilifu ambao mpaka sasa hakuna aliyeu-kifikia na hakuna atakayeufikia!”<sup>8</sup>

Uadilifu ulioje kiasi cha kuwafanya hata maadui wakiri na kuthibitisha ukweli wake....Ni ubora na uwadilifu wa mtume  ulioaminiwa hata na makafiri wakubwa...


Maisha ya kipekee ya Muhammad Mustafa  yametoa jawabu kwa kila jambo na kukusanya ndani yake ukamilifu wa kimaadili uliotawanya nuru kwenye njia ya wale waita-futayo. Yeye ndiye eneo muhimu la elimu ya jamii nzima ya binadamu akitoa cheche za nuru kwenye njia yawale wanao- tafuta mwanga. Yeye ni mwalimu pekee wa wanadamu atoaye muongozo kupitia nuru madhubuti na inayong'ara kwa wale wote wanaotafuta njia ya haki. Umati wa wanafunzi wenye shauku waliomzunguka ulikuwa chuo kilichokusanya watu kutoka matabaka yote ya jamii bila kujali rangi ya ngozi zao, tofauti ya lugha zao, tamaduni zao na nafasi zao katika jami. Walikusanyika pamoja kama wamoja. Hakuna kilichomzuia

---

8. Tazama kamil miras,tacrid-I sarih tercemesi, Ankara 1972




yeyote aliyetaka kujumuika nao. Umati huo haukuwa wa kabila maalumu, bali ilikuwa chemchem ya maarifa na hekima kwa wanaume na wanawake madamu wote ni wanadamu. Hivyo hapakuwepo na tofauti yeyote baina ya mnyonge na yule mwenye nguvu...

Hebu watazame wale waliomfuata Mtume  utaona kuna watu maarufu kama vile Najashi Mfalme wa Uhabeshi (Ethiopia), Farwa kiongozi wa ma'ania, Dhul'qila chifu wa Khimyar, Firuz Daylami, Maraqaboud kiongozi wa yemen na magavana wa Umman, Ubayd na Jafar.

Hata hivyo jambo litakalokushangaza zaidi, tazama pembezoni mwa hao wafalme waliotajwa utakuta watu wa kawaida kama vile Bilal, Yasir, Suhayb, Habbab, Ammar, Abu Fuqayha na wengineo, sambamba nao wapo wanawake wajane na vijakazi kama vile Sumyya, Lubayna, Zinnirah, Nahdiya na Umm Abis.

Katika Maswahaba hao walikuwemo watu wenye akili na uelewa wa hali ya juu ambao walijaliwa uwezo wa kuamua mambo. Vilevile walikuwemo wenye uwezo wa kutatua mata-tizo yenye utata mkubwa, wana utambuzi wa mambo yanay-owahusu ulimwengu, wana uwezo wa kuongoza dola na nchi kwa ustawi mkubwa.

Katika wafuasi wa Mtume  wapo waliotawala miji na majimbo makubwa. Kwa juhudi zao watu wengi walipata uon-gofu na kuonja ladha ya haki na uadilifu. Walieneza amani na utulivu katika jamii na kuungana nao kama ndugu zao.







# *Sehemu Ya Dili*



❁ Tabia Za Hali Ya Juu Za Mtume Wa Allah ❁

❁ Viwango Vya Juu Zaidi Ya Nyota



## Tabia Za Hali Ya Juu Za Mtume Wa Allah ﷺ


Tukitazama historia ya binadamu hakuna mtu ambaye maisha yake yamesomwa, yakatafitiwa na kudurusiwa kwa kina kama yalivyodurusiwa na kuandikwa maisha ya Mtume Muhammad Mustafa ﷺ. Na lau kama tukijaribu kuelezea kila kitu na kila eneo linalounda shakhsia ya kipeke ya Mtume ﷺ hata vitabu vya ukubwa wa kiasi gani havitatosha.


Sayansi za Kiislamu, kwa maana ya msingi<sup>9</sup> ijthadi<sup>10</sup>, nazo pia zimefanya aina mbalimbali za shakhsia ya Mtume ﷺ kuwa ushahidi na uthibitisho muhimu. Ni kwa sababu hii kwamba matawi mbalimbali ya elimu yote yanafanya kazi ya kudurusu na kuhakiki sifa za msingi za maisha ya Mtume ﷺ.

Kwa hakika vitabu vyote vya Kiislam vilivyotungwa tangu miaka 1400 iliyopita vinalenga moja kwa moja kukifanua kitabu na kumfafanua mtu, yaani Mtume Muhammad ﷺ.


9. Misingi inayotegemewa nasayansi zakiislam ni quran na sunnah ambayo kwa pamoja vinajurikana kama nass.sunnah ni kila kauli kitendo kuridhia au mwenendo wa mtumeis)Hakuna ijthad katika mambo yaliyotolewa maamuzi ya wazi katika quran na sunnah.
10. Ijthad ni mchakato unaofanywa na mujtahid, yaani msomi mwenye mafunzo maalu ya kutoa fatwa, ili kutatua suala ambalo halikutolewa maamuzi ya wazi katika qur'an na sunnh, lakini mchakato huo huwa ndani ya misingi hiyo miwili ya qur'an na sunnah.






Mtume  ambaye ni muujiza mkubwa hatuwezi kumfahamu kikamilifu kwa kutumia vipawa vyetu vya kibinamu vyenye kikomo. Kwa mfano, hatuwezi kujua ipasavyo nuru ya Muhammad kwani jambo hilo ni sawa kumwaga bahari ndani ya kikombe.

Kitu pekee tunachofanya hapa ni kujaribu kuelezea kwa kadri ya uwezo wetu –mifano michache ya matone kutoka katika bahari hiyo kuu ya kielelezo cha kuiga cha Mtume wa Allah  tukitaraji kuwa itasaidia katika kupata kumuelewa.

### **Uzuri Wa Sura, Umbile Na Tabia Za Mtume**


Mtukufu Mtume  ni muujiza uliobarikiwa ambao mfano wake haujapata kuumbwa. Alikuwa mzuri wa sura, maisha na muongozo uliokamilika. Kuhusu ukweli huo, Imam Qurtubi anasema:



“Uzuri wa muonekano wa mtume wa Allah  haukujidhirisha wote. Lau kama uzuri wake wote ungejidhirisha, jinsi ulivyo, masahaba wasingeweza kuwa na nguvu ya kumtazama”<sup>11</sup>


Kwa kweli, hata katika masahaba walio karibu sana na mtume , kuna ambao hawa kuweza kutazama uzuri wa sura yake kiasi cha nyoyo zao kuridhika, kutokana na adabu waliyokuwa nayo mbele yake. Imesimuliwa kuwa wakati wa kuongea na Mtume  Masahaba wote walikuwa wakiinamisha macho yao isipokuwa Abu Bakr na omar ambao walikuwa




wakimtazama naye akiwatazama wakimuonyesha tabasamu naye akiwaonyesha tabasam. (Tirmidhi, Manaqib, 16/3668)

Mwisho ni mwa umri wake, Amr Ibn As  aliyeifungu misri alielezea jambo hili:

Ingawa muda mwingi nilikuwa karibu na mtume  haya iliyonizidi niwapo mbele yake nahisia kubwa ya utukufu wake iliyokuwa ndani mwangu vilimizuia kukinyanyua kichwa kuitazama sura yake tukufu kwa ajili ya kufurahisha moyo wangu. Hakika kama sasa hivi ningepombwa kuelezea muonekano wa Mtume  nisingeweza hata kidogo” (Muslim, Iman 192)<sup>12</sup>

Uso wa Mtume  ulikuwa ukienzea utulivu na amani kwa wale waliokuwa karibu naye, ulikuwa uso mzuri zaidi na maridadi, kiasi kwamba Abdullah ibn salam alikuwa mwanazuoni wa kiyahudi, aliposikia ujio wake Madina alimtembelea, na alipoutazama muonekano wake akasema “kamwe uso huu hawezi kuongopa “,na haraka sana akasilim. (Tirmidhi, Qijamah 42/2485; Ahmad, V, 451)

Uzuri, haiba, mwanga, nuru na umaridadi wa Mtume 

Ulikuwa katika kiwango na daraja kubwa kiasi kwamba hakuhitaji ushuhuda wa nyongeza wala muujiza kuthibitisha kwamba yeye ni Mtume wa Allah.

Pindi anapofurahishwa na kitu au kutofurahishwa nacho haraka sana uso wake ungejieleza. mwili wake safi ulikusanya nguvu, haya na azma ya hali ya juu. Ama kuhusu kiwango cha hisia ya ndani ya moyo wake hakiwezi kuelezeka.

---

12. Tazama pia, Ahmad Ibn Hanbal, Al-musnad, Istanbul 1992 1v, 199.



Nuru maridhawa ilikuwa ikitawanyika kutoka usoni mwake. Mtiririko mzuri ulikuwa katika maneno yake, madaha katika mwendo wake, uwezo usiokuwa wa kawaida katika kujieleza, na ufasaha mkubwa katika kila neno lilotoka kinywani mwake


Hakuwa akisemasema bure kila neno lake liliwakilisha hekma na nasaha. kamusi yake kamwe haikuwana nafasi hata kidogo ya kuteta, kusengenywa wala mazungumzo ya upuuzi. Alikuwa na watu kulingana na uwezo wa kuelewa

Alikuwa mwema na mnyenyekevu. Kamwe hakuwa akicheka kwa sauti, bali sikuzote alionyesha furaha yake kwa tabasam. Kila aliemuona papo hapo angejawa na hali ya kumuheshimu. Kusuhubiana naye au kuzungumza naye kungetosha kumfanya mtu aingiwe na upendo wake.

Alikuwa akiamiliana na watu wema kwa heshima kulingana na daraja lao la uchamungu. Alikuwa mkarimu zaidi kwa jamaazake wakaribu. Ukaribu huo kwa jamaa zake aliuenza hata kwa watu wengine.

Alikuwa akiamiliana na watumishi wake katika namna nzuri sana kiasi kwamba alikuwa akiwalisha kile anachokula yeye na kuwavisha kile anachovaa yeye.

Hatuwezi kukadiria ukarimu na utoaji wake kwa kiasi kinacholingana naye. Kwani alikuwa akitoa sana bila kuogopa hata kidogo suala la ufukara.

Jabir  anaelezea jambo hili kwa kusema: "Hakuwahi kusema "Hapana" kwa yule anayemuomba kitu." (Muslimu, Fadhail, 56)



Mtume ﷺ alikuwa mwingi wa kuwatembelea jamaa zake wa karibu, akionyesha mapenzi makubwa na huruma ya hali ya juu kwa watu, akiamiliana na watu kwa namna nzuri zaidi, na siku zote alijiepusha na tabia mbaya.

Siku zote alisema:

“Hakuna kitu kitakacho kuwa kizito kwenye mizani ya muumini siku ya qiyama kuliko tabia njema. Hakika Allah humchukua mtu mwenye tabia mbaya, mwenye maneno machafu” (Tirmidhi, Birr, 62/ 2002)

Mtume ﷺ alikuwa mkweli katika maneno yake na mtekelezaji wa ahadi zake.

Aliwashinda watu wote kwa wema, akili na wepesi wa uelewa. Alikuwa mwingi wa huzuni na tafakuri ya kuendelea.

Ingawa alikuwa mwingi wa ukimya lakini alikuwa akikamilisha kila sentensi anayozungumza.

Alikuwa akikusanya maana nyingi katika maneno machache, yaani alikuwa na uwezo wa kufikisha ujumbe au maana ya ndani zaidi kwa kutumia maneno machache. Maneno yake yalikuwa yakitoka kidogo kidogo kama punje za tasbihi.

Ingawa alikuwa na haiba ya hali ya juu lakini hadhi yake ilikuwa ya kuvutia.

Alikuwa haghadhibiki ila pale haki inapovunjwa au isipofuatwa.

Haki inapovunjwa ghadhabu yake ingeendelea mpaka haki hiyo inaporejea mahali pake. Baada ya kuhakikisha haki imerudi angejawa na utulivu wa hali ya juu.



Kamwe hakuwa akighadhibika kwa ajili ya nafsi yake, na hakuwa akigombezana au kulumbana na watu katika mambo yake binafsi.


Alikuwa haingii nyumba ya yeyote bila ya idhini.

Anaporudi nyumbani kwake, alikuwa akiugawa muda wake wa kukaa hapo katika sehemu tatu:

Muda wa kwanza ni kwa ajili ya Allah, muda wa pili kwa ajili ya familia yake mwenyewe. Muda anaoutenga kwa ajili yake alikuwa akiutumia kwa ajili ya watu wa aina zote, watu maalumu na watu wa kawaida.

Hakuwa akimnyima mtu yeyote katika muda wake huo, na moyo wake aliufungua kwa watu wote.

Awapo msikitini alikuwa akikaa sehemu tofauti tofauti, ilikuzuia tabia ya watu kukaa eneo maalum kuwa takatifu zaidi ya nyingine. Hakupenda tabia ya majivuno na kiburi mbele ya watu. Anapoingia katika mkutano, alikuwa anakaa mahali popote penye nafasi na kuwausia wengine kufanya hivyo.

Iwapo mtu angemuomba kitu ili kutatua tatizo fulani, bila kujali ukubwa wa ombi hilo, Mtume  asingejisikia uzito kutekeleza ombi hilo. Kama akishindwa kulitekeleza ombi hilo. Kama akishindwa kutekelza, basi alikuwa hamrejeshi mikono mitupu bali angeusafisha moyo na akili ya mtu huyo angalau kwa maneno ya faraja. Kwake watu wote walikuwa sawa, bila kujali daraja zao za kijamii, bila kujali kama ni masikini au tajiri, msomi au asiye msomi.


Vikao vyake vyote ilikuwa ni mahali pa kutekeleza kwa vitendo mambo mema kama vile: upole, elimu, tabia njema,









subira, kutunza amana na kumtegemea Mwenyezi Mungu pekee.

Hakuwahi kumlaani mtu kwa aibu au mapungufu yake. Bali iwapo angeona haja ya kumzindua na kumuelimisha mtu mfulani, alikuwa akimuelekeza kwa ishara fulani na kwa namna nzuri bila kumuudhi. Sio tu kwamba hakushughulika na aibu za wengine, bali pia alikuwa akiwakataza sana watu kufuatilia aibu za wenzao.

Mtume , Nuru ya Ulimwengu, hakuwa akizungumza bila malengo ya kutaka thawabu na radhi za Allah. Katika mikusanyiko aliyozungumza ilikuwa ni mabustani ya furaha. Alipokuwa akiongea wale waliomzunguka walikuwa wakijawa na shauku, upendo na kumsikiliza kwa umakini mkubwa. Masahaba wanaielezea hali hii kama ifuatavyo:

“Tulikuwa tukikaa kimya na kwa umakini mkubwa kana kwamba kuna ndege katua vichwani mwetu na tunahofia kumpeperusha”. (Abu Dawud, Sunnah, 23 – 24/4753)


Adabu na hayaa iliwaingia sana masahaba kiasi kwamba walikuwa wakipata ugumu na kukosa uthubutu wa kumuuliza Mtume . Hivyo, walikuwa wakisubiri fursa ya kujiwa na Bedui kutoka jangwani aje kumuuliza Mtume  ili nao wafaidike na chemchem na baraka za Mtume  zilizokuwa zikimiminika juu ya kikao chao.

Katika maisha yake yote, Mtukufu Mtume  alikuwa ni mfano hai wa ikhlas na moyo safi. Kamwe hakuwahi kusema jambo lisilotoka moyoni mwake na hakumwambia mtu afanye





jambo ambalo yeye mwenyewe halifanyi. Kwa tabia hizo za hali ya juu alikuwa ni Qur'an hai. <sup>13</sup>

### **Unyenyekevu Wa Mtume**

Licha ya Mtume , kwa muda mfupi, kupata mafanikio ambayo wafalme wengine hawakuweza kuyafikia, akazivuta nyoyo za watu wote kama mwalimu na muadilishaji wa watu wote, aliendelea kuishi maisha yake ya kawaida bila kuangalia hata kidogo utajiri wa kidunia uliokuwa umelala miguuni mwake. Aliendelea kuishi katika chumba chake cha udongo chenye hadhi ya chini na kitanda kilichotengenezwa kwa majani ya mtende. Alikuwa akivaa mavazi ya kawaida. Wakati anapokosa hata chakula alikuwa akimshukuru Mwenyezi Mungu na kufunga jiwe tumboni mwake ili kupunguza ukali wa njaa. Japokuwa Allah alikuwa amemsamehe makosa yake yaliyotangulia na yale yajayo, bado aliendelea kumshukuru na kumuomba. Alikuwa akiswali mpaka miguu yake inavimba.

Alikuwa akiwasaidia maskini, akiwafariji yatima na wenye upweke. Licha ya ukuu wake, alishughulishwa na watu wasiojiweza na kuwatandazia mbawa za huruma yake.

Siku ya ufunguzi wa Makka ambapo alitokeza machoni mwao kama mtu mwenye nguvu kubwa, alikuja mmoja wao mbele ya Mtume  akikhofu na kutetemeka na kumwambia:

“Ewe Mtume wa Allah... tafadhali ... nifundishe Uislamu”. Mtukufu Mtume  alianza kumfundisha utulivu na

---

13. Tazama: Ibn sa'd, at – Tabaqaatul – kubra, Beirut, Daru Sadir, I, 121, 365,422 – 422; Haythami, Majmauz – Zawaid, Beirut 1998, IX, 13.



kutokuwa na wasiwasi akimkumbusha hali yake ilivyokuwa katika miaka ya nyuma, akamwambia:

“Tulia na usiwe na wasiwasi, kwani mimi sio mfalme”, kisha akaendelea kwa kumkumbusha kuhusu mamaye Mtukufu, “... bali mimi ni mtoto wa mwanamke aliyekuwa akila nyama zilizokaushwa na jua.”<sup>14</sup>

Kwa maneno haya, Mtume ﷺ alifika kwenye kilele cha unyenyekevu ambacho hakijawahi kutokea katika historia yote ya binadamu.

Siku hiyohiyo alionyesha ulaini wa moyo wake kwa Abu Bakr ؓ, ambaye alikuwa amembeba baba yake kikongwe kumleta kwa Mtume ﷺ kumuomba amfundishe tamko la imani. Mtume ﷺ alipomuona akamwambia kwa maneno ya kuonyesha huruma: “*kwa nini umemchosha mzee wako kuja hapa? Kwa nini badala yake sisi tusingemtembelea?*”<sup>15</sup>

Mara zote Mtume ﷺ alikuwa akijitambulisha kama kiumbe dhaifu. Alikuwa akijieleza kwa kusema:

“*Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi*”  
(Al- Kahf, 18: 110)

Alikuwa akiutahadharisha *ummah* wake kuangukia kati-ka shimo la upotevu kama *ummah* zilizotangulia, na hivyo alikuwa akiongeza neno ‘*abduhu*’, yaani mja wa Allah, kwenye kifungu cha maneno ya shahada kinachoshuhudia utume wake.

14. Tazama: Ibn Majah, At’imah, 30; Tabatabai, al – mu’jamul Awsat, II, 64.

15. Tazama: Ahmad, VI, 349; Haythami, VI, 174; Ibn Sa’d, V, 45.



Kwa wale walioonyesha taadhima kupita kiasi, alikuwa akiwaambia:

*“Msinipandishe zaidi ya daraja ninayostahiki kwani Allah alinifanya kuwa mtumwa wake kabla ya kuwa mjumbe wake”*  
(Haythami, IX, 21)

Mtume 🌿 alikuwa na beseni la chakula lijulikanalo kama *gharra* likibebwa na watu wanne. Baada ya swala ya *Dhuha* lililetwa likiwa limejaa mchuzi, ambapo masahaba walikusanyika. Baada ya watu wengi kukusanyika, Mtukufu Mtume 🌿 alipiga magoti na kisha akakaa vizuri ili kuwapa nafasi wengine.

Bedui mmoja aliyeona kitendo hicho kuwa ni staha iliyo-zidi kiwango akasema:

*“Huu ni mkao gani?”*

Mtume 🌿 akajibu:

*“Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amenifanya kuwa mja mtukufu, mnyenyekevu, na wala hajanifanya jeuri mwenye ukaidi.”* (Abu Dawud, 17/3773)

Kwa hiyo tunaweza kusema kwa uhakika kwamba alitan-gaza kuwa hakuwa mwenye majivuno na kiburi.

Sehemu nyingine anafafanua jambo hili akisema:

*“Hakuna mtu anayeweza kuingia peponi kwa matendo yake tu.”*

Masahaba walishangaa na kumuuliza:

*“Hata wewe, ewe Mtume wa Allah?”*



Akajibu:

*“Hata Mimi. Isipokuwa kwa neema ya Mola wangu. Hata mimi siwezi kuingia peponi mpaka neema, huruma na rehema Yake vinifunike ... vinginevyo matendo yangu pekee hayawezi kuniokoa!”* (Bukhari, Riqaq, 18; Muslim, Munafiqun, 71-72; Ibn Majah, Zuhd, 20; Darimi, Riqaq, 24)

Kwa mara nyingine Mtume ﷺ anawaonya wale wanaovaa mavazi yao kwa namna ya majivuno, kiburi na kujiona, kwamba wanasubiriwa na ndimi za moto wa Jahannam.

Baadhi ya hadithi kuhusu jambo hili ni kama ifuatavyo:

“Siku ya Kiyama, Allah hatomtazama yule anayeburuza chini nguo yake kwa namna ya majivuno”. (Bukhari, Libas, 1, 5)

“Yule avaa vazi la umashuhuri hapa duniani, Allah atamvika vazi la udhalili siku ya Kiyama.” (Ibn Majah, Libas, 24)

Mtume ﷺ alikuwa akitoa hata ngawira zilizokuwa katika fungu lake, akiendelea kuishi maisha ya staha nay a chini sawa na mtu wa hali ya chini kabisa katika *ummah* wake.

### Ukarimu Wa Mtume ﷺ

Mara zote Mtume ﷺ alijieleza kama mtu aliyeamriwa kutoa huku akisisitiza sana kwamba Allah pekee ndiye Mtoaji wa kweli na ndiye Mmiliki wa vitu vyote.

Safwan ibn Umayya, ambaye alikuwa mmoja wa watu mashuhuri wa kabila la Quraysh kabla hajasilimu, alisuhibiana na Mtume ﷺ katika vita vya Hunayn na Taif. Baada



ya kuuona mshangao wa Safwan aliyekuwa akitazama kundi fulani la ngawira za vita zilizokuwa zimekusanywa katika eneo la Jirannah, Mtukufu Mtume 🕌 akamuuliza:

“Umezipenda?”

Safwan alipojibu kwa kukubali, Mtume 🕌 akamwambia:

“Zichukue ... zote ni zako!”

Hapo Safwan akashindwa kuizuia furaha yake akasema:

“*Hakuna moyo unaoweza kuwa na ukarimu kiasi hiki isipokuwa moyo wa mitume pekee*”. Akatamka shahada na kusilimu.<sup>16</sup>

Aliporejea kwa watu wake akatangaza wazi kuwaambia:

“*Enyi watu wangu, ingieni katika Uislamu, kwa hakika Muhammad anatoa bila kuogopa umaskini hata kidogo!*” (Muslim, Fadhail, 57 – 58; Ahmad, III, 107)

Siku nyingine alikuja mtu kwa Mtume 🕌 na kumuomba kitu lakini akawa hana chochote cha kumpa. Hata hivyo, Mtume 🕌 alimwambia mtu huyo atafute mkopo na akamhakikishia kuwa Yeye angeulipa kwa niaba yake. (Haythami, X, 242)<sup>17</sup>

Mtume 🕌 alikuwa kama baba yake, Nabi Ibrahimu 🕌: alikuwa hali chakula peke yake bila wageni. Alikuwa akiwali pia madeni waliokufa au kuwatafutia watu wa kulipa madeni hayo. Hakuwa akiswali swala ya jeneza bila wahusika kulipiwa madeni yao.

16. Waqidi, Maghazi, Beirut 1989, II, 854 – 855.

17. Tazama pia: Abu Dawud, Haj, 33 – 35/3055; Ibn Hibban, Sahih, Beirut, 19993, XIV, 262 – 264.



Mtkufu Mtume ﷺ ana hadithi tukufu isemayo:

*“Mtu karimu yu karibu na Allah, yu karibu na pepo, yu karibu na watu na yu mbali na moto. Lakini mtu bakhili yu mbali na Allah, yu mbali na pepo, yu mbali na watu na yu karibu na moto”.* (Timidhi, Birr, 40/1961)

Katika hadithi nyingine anasema:

*“Sifa mbili hazikusanyiki kwa muumini wa kweli: ubakhili na tabia mbaya...”* (Tirmidhi, Birr, 41/1962)

### **Uchamungu Wa Mtume ﷺ**

Alikuwa mchamungu zaidi kuliko watu wote. Siku zote alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu ampe *taqwa*, yaani uchamungu:

*“Ewe Allah, ipe nafsi yangu uchamungu na uitakase, kwani Wewe ndiye Mwenye kuitakasa; Wewe ndiwe msaidizi wake na ndiwe Bwana wake”.* (Muslim, Dhikr, 73)

*“Ewe Allah, nakuomba inijaalie uongofu, staha na utajiri wa moyo”.* (Muslim, Dhikr, 72)

Uchamungu ulimfanya aishi kama maskini. Bibi Aisha anaeleza kuwa, kamwe Mtume ﷺ hakuwahi kushiba hata mkate wa shayiri kwa siku mbili mfululizo, na katika maelezo mengine, mkate wa ngano kwa muda wa siku tatu mfululizo (Bukhari, Ayman; Muslim, Zuhd, 20 – 22; Ibn Majah, At’imah, 48)

Katika kuuhamasisha *ummah* wake kuishi maisha ya uchamungu, anasema:



*“Hakika watu walio karibu nami zaidi ni wachamungu popote walipo”.* (Ahmad, V, 235; Haythami, IX, 22)

*“Hakika rafiki zangu ni wachamungu”* (Abu Dawud, Fitani, 1/4242)

*“Mche Mewnyezi Mungu popote uwapo, na jambo baya lifuatishe kwa jambo jema litalifuta. Amiliana na watu kwa tabia njema...”* (Tirmidhi, Birr, 55/1987)

Ama kuhusu njia ya kupata *taqwa* ya kweli, anasema:

*“Mja hawezi kufikia daraja ya taqwa ya kweli mpaka aepuke baadhi ya mambo yanayoruhusiwa kwa hofu ya kuingia katika mambo yasiyoruhusiwa”.* (Tirmidhi, Qiyamah, 19/2451; Ibn Majah, Zuhd, 24)

Kwake Yeye hakuna ubora wa mtu mweupe dhidi ya mtu mweusi, wala taifa fulani dhidi ya jingine; bali ubora wa mtu hupatikana kwa uchamungu. (Ahmad, V, 158)

Nabii Isa ﷺ alitoa maelezo yenye kuvutia kuhusu *taqwa* katika kumjibu mtu mmoja aliyemuuliza:

*“Ewe mwalimu wa wema na kheri! Mtu anawezaje kuwa mchamungu mbele ya Mola?”*



Nabii Isa ﷺ akamjibu:

*“Ni rahisi. Shikamana na Mola wako kwa upendo wa dhati, kisha tenda matendo mema kwa uwezo wako wote na uwahurumie wana wa Adamu wote kama unavyoihurumia nafsi yako”.*





“...na usiwatendee watu wengine kile usichopenda kutendewa. Ukifanya hivyo utakuwa mchamungu mbele ya Mola wako”.<sup>18</sup>

Siku moja Umar  alimuuliza Ubayy ibn Kaab  maana ya *taqwa*.



Ubayy akamuuliza: “Umewahi kupita kwenye njia yenye miba?”


“Ndiyo”

“Ulifanya nini?”

“Nilipandisha nguo zangu na kuangalia kwa umakini kila hatua ninayopiga ili nisichomwe na miba”, Omar alijibu.

Hapo Ubayy akasema: “Hiyo ndiyo *taqwa*”.<sup>19</sup>

Wale walio karibu zaidi na moyo wa Mtume  ni wachamungu. Maelezo yafuatayo yamesimuliwa na Muadh ibn Jabal :

“Wakati akinituma kama gavana nchini Yemen, Mtume  alinisindikiza mpaka kwenye viunga vya mji wa Madina ili kuniaga. Nilikuwa juu ya mnyama naye akiwa anatembea kwa miguu. Baada ya kunipa ushauri na usia kadhaa, aliniambia:

‘Ewe Muadh! Huwenda usiweze kuniona tena baada ya mwaka huu. Lakini waweza kuutembelea msikiti wangu huu au kaburi langu...’

Baada ya kusikia maneno hayo kwa huzuni ya kuachana na rafiki yangu kipenzi, nilianza kububujikwa na machozi.

18. Ahmad, az-Zuhd, uk. 59.

19. Ibn Kathir, Tafsirul- Qur’anil – Adhim, Beirut 1988, I, 42.



‘Usilie’, Mtume 🕌 alinifariji. Kisha akatazama upande wa msikiti wake na kusema:

‘Watu walio karibu zaidi nami ni wachamungu ambao, popote wanapokuwa humuogopa Allah.’<sup>20</sup>

### **Zuhdi ya Mtume** 🕌

Wakati ulifika ambapo mataifa mbalimbali yalimkubali Mtume 🕌 na kukubali kuwa chini ya uongozi wake na kumfanya kuwa Bwana wa Arabia yote. Licha ya kwamba angeweza kuishi maisha ya ufakhari wa hali ya juu, badala yake aliendelea na maisha yake ya hali ya kawaida. Alikiri kwamba Yeye hamiliki chochote na kwamba kila kitu ni milki ya Allah Mtukufu.

Wakati ulifika ambapo mali zilianza kumiminika. Misafara iliyobeba hazina kubwa ilimwaga mali katika mitaa ya Madina. Aligawa mali zote hizo kwa watu wenye shida, akaendelea na maisha yake ya kujinyima, yaani *zuhdi*. Alikuwa akisema:

*“Kama ningekuwa na dhahabu nyingi kama mlima wa Uhud, mbali na kiasi kinachohitajika kulipia madeni yangu, nisingekaa nayo zaidi ya siku tatu.”* (Bukhari, Tamanni, 2; Muslim, Zakat 31)

Siku zingepita bila moto kuwashwa katika nyumba ya Mtume 🕌 kwa ajili ya kupika; na mara nyingi alikuwa akilala njaa. (Ahmad, VI, 217; Ibn Sad, I, 405)



Siku moja Omar aliingia kwa Mtume ﷺ. Aliangaza chumbani kaona hakuna chochote zaidi ya tandiko lililotengenezwa kwa majani ya mtende, ambalo wakati huo Mtume ﷺ amelilalia. Tandiko hilo la majani lilikuwa limeacha alama kwenye ngozi tukufu ya Mtume ﷺ. Katika pembe ya chumba palikuwepo na chombo kidogo cha unga wa ngano na kiriba kikuukuu cha maji kilichotengenezwa kwa ngozi. Hivyo tu ndivyo vilivyokuwepo! Hizo ndizo mali za mtu ambaye Peninsula yote ya Arabia ilisalimu amri kwake kwa hiari.

Omar ﷺ akashusha pumzi na ghafla akabubujikwa na machozi kutokana na hali aliyoiona.

“Kwa nini walia?” Mtume ﷺ aliuliza.

Omar ﷺ akajibu: “Kwa nini nisilie? Kaisar na Khosrou wanaogelea katika furaha za dunia hali ya kuwa Mtume wa Allah analala kwenye tandiko lenye viraka....”

Mtume ﷺ akaufariji moyo wenye maumivi wa rafiki yake mpendwa na kusema:

“Usilie, ewe Omar. Je hupendi wao wawe na dunia nasi tuwe na Akhera?”<sup>21</sup>

Sehemu nyingine katika tukio kama hilo alisema:

*“Nina nini Mimi na Dunia? Hakika Mimi na Dunia ni kama msafiri aliyekaa chini ya kivuli cha mti kisha akaendelea na safari yake.”<sup>22</sup>*

21. Tazama: Ahmad, II, 298; Tabarani, al-mu'jamul- kabir, kilichohakiki na kuchapishwa na Hamidi Abdul Majid as-salafi, Beirut, Daru Ihyaith-Turathil-Arabi, X, 162.

22. Tirmidhi, Zuhd, 44/2377; Ibn Majah, Zuhd, 3; Ahmad, I, 301.



Mtume 🌿 alikuwa na hofu ya kuulizwa kuhusu neema za dunia siku ya hesabu, na hivyo alikuwa akiomba:

“Ewe Allah! Nifanye niishi hali ya kuwa ni maskini, nifishe nikiwa maskini na unifufue katika kundi la maskini!” (Tirmidhi, Zuhd, 37/2352; Ibn Majah, Zuhd, 7)

Japokuwa Mitume wote wana dhamana ya moja kwa moja ya kuingia peponi, lakini nao pia wataulizwa kuhusu neema mbalimbali walizopata hapa duniani na kama walifikisha au hawakufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Qur’an Tukufu inasema kuhusu jambo hili:


“Na kwa yakini tutawauliza wale walio pelekewa Ujumbe, na pia tutawauliza hao Wajumbe” (A’raf, 7: 6)



Maneno kama vile *zuhd*, *taqwa na ihsan* ni maneno tofauti lakini yenye maana moja. Lengo la pamoja la mawazo hayo ambayo pia ni msingi wa mafunzo ya *Usufi*, ni kuuongoza moyo kwenye amani na utuvu kwa kuyafunga matamanio ya nafsi na kuinua vipawa vya ndani ya roho, ambapo matokeo yake ni kupata msingi wa moyo salama na uliosafika (*qalbus- salaim*), na kuwa mja wa kweli wa Mwenyezi Mungu.

### Ulaini Wa Moyo Wa Mtume 🌿


Mtukufu Mtume 🌿 alikuwa mwenye moyo wenye hisia sana na laini sana. Siku moja alimuona mtu akitema makohozi ardhini, uso wa Mtume ukawa mwekundu, akasimama mahali pake akawa hajaendelea. Maswahaba wakafanya haraka kwenda kunika kohozi hilo kwa mchanga kisha Mtume 🌿 akaendelea na safari yake.



Mtume  alikuwa akiwataka watu kuvaa mavazi nadhifu na hakupenda mtu asiyesafisha mavazi na mwili wake. Kadhalika hakupenda nywele na ndevu zilizochakaa.

Siku moja alipokuwa msikitini aliingia mtu mwenye nywele na ndevu zilizovurugika. Mtume  akamuashiria kuwa azipangilie nywele na ndevu zake. Baada ya kufanya kama alivyoambiwa, Mtume  akasema:

“Je hii sio bora kuliko kutembea na nywele chafu kama shetani?” (Muwatta, Shaar, 7)<sup>23</sup>



Katika tukio jingine, Mtume  alimuona mtu mmoja akiwa katika hali ya uchafu wa nywele.

Alishangaa, kisha akasema:

“Kwa nini haoshi nywele zake na kuzitunza?”

Alimuona mtu mwingine akiwa na nguo chafu akasema:

“Je mtu huyu hawezi kupata maji akafua nguo zake?” (Abu Dawud, Libas, 14/4062; Nasai, Zinat, 60)

Siku nyingine mtu mmoja alikuja kwake akiwa katika mavazi yaliyochafuka. Mtume  akamuuliza iwapo ana uwezo mzuri kifedha. Mtu huyo alipokiri kuwa na uwezo mzuri, Mtume  akamtahadharisha akisema:

“Hakika Mwenyezi Mungu akikupa mali basi acha aone athari ya neema yake kwako” (Abu Dawud, Libas, 14/4063; Nasai, Zinat, 54; Ahmad, IV, 137)

Hadithi nyingine kama hiyo inasema:

---

23. Bayhaki, Shuabul-Iman, Beirut 1990.



“Allah anapenda kuona athari ya neema yake kwa mja wake”. (Tirmidhi, Adab, 54/2819; Ahmad, II, 311)

Shakhsia ya Mtume 🕌 ni kilele cha huruma, upole na ulaini wa moyo, hata kwa Bedui mkaidi ambaye alikuwa akim-pigia makelele kwa kumuita kwa upande wa nyuma:

“*We Muhammad, We Muhammad*” lakini Mtume 🕌 ali-zungumza naye kwa upele na kumwambia:

“*Ndiyo, nikusaidie nini?*”<sup>24</sup>

Kwa sababu ya ulaini wake na tabia zake tukufu, alikuwa akiwahudumia wageni wake yeye mwenyewe. (Bayhaki, Shuab, IV, 518, VII, 436)

Hata wakati wa utoto wake hakuwahi kugombezana na yeyote wala kuingia katika mijadala na malumbano yasi-yokuwa na maana yoyote. Na kwa kuwa alikuwa mtu mwenye moyo laini na upole sana, aliwalea watu wa nyumba yake katika maadili haya ya hali ya juu.

Mjukuu wa Mtume 🕌, Hasan ibn Ali 🕌 ni kielelezo kizuri cha malezi hayo:

Siku moja Hasan ibn Ali 🕌, baada ya kunguka Kaaba na kuswali raka mbili kwenye eneo la *maqam Ibrahim*, aliweka shavu lake chini na kuanza kulia:

“Ewe Allah, mja wako dhaifu nimekuja mlangoni kwako. Ewe Allah, mtumwa wako maskini nimekuja kukuomba. Ewe Allah, muombaji amekuja kwako...”

24. Tazama: Muslim, Nudhur, 8; Abu Dawud, Ayman, 21/3316; Tirmidhi, Zuhd, 50; Ahmad, IV, 239.




Baada ya maombi hayo aliondoka na kupita sehemu walipokuwa maskini waliokuwa wakila kipande cha mkate. Alipowasalimia walimkaribisha naye akaungana nao na kisha akawaambia:



“Lau kama mkate huu usingekuwa sadaka nisingesita kula pamoja nanyi”. Kisha akawafariji na kuwaambia:

“Twendeni nyumbani kwangu!”

Huko aliwapa chakula, mavazi mapya, pesa kisha akawaaga kwa furaha. (Abshihi, Al-mustafa, Beirut 1986, I, 31)


Ulaini, upole na huruma hii ni miongoni mwa mifano mikubwa ya namna huruma ya Allah inavyojionyesha kwa wanadamu kwa kuwahurumia na kuwa na upole kwa wanadamu wote.

Mfano mwingine wa huruma ya Hassan  ni pale ambapo siku moja alikuwa akipita katika shamba la mizabibu mjini Madina akamuona mtumwa mweusi akila mkate na kumlisha pia mbwa aliyekuwa mbele yake.

Hassan  alishangazwa sana na jinsi jina la Allah la “*Rahman*” linavyojionyesha katika huruma ya mtumwa huyu aliyekuwa akimlisha mbwa. Akamuuliza sababu ya kufanya hivyo, japokuwa mtumwa huyo alionekana kuwa na aibu sana usoni mwake kiasi cha kutomtazama Hassan .

Hassan akamuuliza:

“Wewe ni kijana wa nani?”

Akajibu: “Mimi ni kijana wa Abana bin Othman .

“Hii mizabibu ni ya nani?”



“Ni ya Aban...”

Hapo Hassan ❦ akataka kuwa na huyu mtumwa ambaye kwa nje ni mtumwa lakini kwa ndani ni kipenzi cha Allah. Akamwambia:

“Usiondoke hapo, nitarudi baada ya muda mfupi”.

Alikwenda kwa Aban, mmiliki wa mizabibu, akainunua mizabibu hiyo pamoja na yule mtumwa. Kisha akarudi kwa yule mtumwa akamwambia:

“Ewe kijana, nimekununua”

Kijana huyo akasema kwa namna ya heshima na adabu:

“Vizuri sana, hivyo ni wajibu wangu kumtii Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na wewe...”

Hasan aliposikia maneno hayo alizidi kumpenda huyo kijana kutokana na utiifu wake wa kweli. Kutokana na moyo mwema wa mtumwa huyo na usafi wa mwenenndo wake, Hassan akamwambia:

“Kuanzia leo uko huru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na mizabibu hii ni zawadi yangu kwako!” (Ibn manzur, muhtasar tarikh dimashq, vii, 25)

### **Adabu Na Hayaa Za Mtume ❦**

Mtume ❦ hakuwa akizungumza kwa sauti ya juu. Alikuwa akikutana na watu kwa tabasamu na unyoofu wa moyo. Anaposikia neno lichukizalo au asilolipenda, alikuwa hasemi chochote mbele ya watu.





Kwa kuwa uso wake uliakisi hali ya moyo na hisia zake za ndani, hivyo wale waliokuwa karibu naye walikuwa wakichukua tahadhari katika maongezi yao na vitendo vyao.

Kutokana na *hayaa* aliyokuwa nayo, hakuwa akicheka kwa sauti ya juu, bali tabasamu ndilo lililokuwa cheko lake. Maswahaba walikuwa wakimuelezea kuwa mwenye *hayaa* sana kuliko hata mwanamwali katika shela yake.

Ameielezea *hayaa* katika hadithi akisema:




“*Hayaa* inatokana na imani, mwenye haya atakuwa peponi. Ukosefu wa haya unatokana na ugumu wa moyo, na ugumu wa moyo humpelekea mtu kuingia motoni” (Bukhari, Iman, 16)

“Haya na imani ni vitu viwili vinavyokaa pamoja, kimoja kikiondoka na kingine huondoka.” (Tabarani, Awsat, VIII, 174; Bayhaqi, shuab, VI, 140)

Hakika upole unapokuwa katika jambo hulipamba, na unapoondoka katika jambo huliharibu”. (Muslim, Birr, 78; Abu Dawud, Jihad, 1)


*Hayaa* ya kweli hupatikana kwa kukumbuka mauti, ambayo ni nyenzo ya kuondoa mapenzi ya dunia moyoni. Mtume ﷺ mara zote alikuwa akiwausia masahaba kuwa na *hayaa* ya kweli kwa Mwenyezi Mungu. Wakati fulani, walipoeleza kuwa walikuwa na *hayaa* kwa Mwenyezi Mungu, aliwaeleza kuwa *hayaa* ya kweli ni kuulinda mwili dhidi ya mambo ya haramu na kutokitoa kifo katika akili zao. Akaendelea kusema kuwa wale waiendeayo Akhera kwa kuaacha kuitenda dunia, hao ndio watu wenye *hayaa* ya kweli kwa Mola wao. (Tirmidhi, Qiyamah, 24/2450)




Mtume  hakuwa akitazama sana usoni mwa mtu. Alikuwa akitazama sana chini kuliko juu. Kutokana na hayaa na shakhsia yake ya hali ya juu, hakuwa akitaja aibu au mapungufu ya mtu mbele yake. Bibi Aisha  anaeleza kuwa Mtume  anapopata habari ya jambo asilolipenda alikuwa hasemi: “Kwa nini fulani anasema mambo hayo?”, bali alikuwa akisema: “kwa nini watu wanasema mambo hayo?” (Abu Dawud, Adab, 5/4788)

Wakati fulani anapotaka kuwatanabahisha kosa fulani alikuwa akiwakumbusha katika namna nzuri kwa kusema:


“Kwa nini ninaona mambo kadhaa yakitendeka?”<sup>25</sup> kana kwamba anaelekeza lawama kwake mwenyewe.

Mtukufu Mtume  anapotaka kumshauri mtu jambo, alikuwa makini sana ili asinghadhibishe au kumhuzunisha mhusika, kwa sababu alikuwa mnara wa huruma.

Maulana Rumi, rafiki wa Haki, ambaye alijipamba kwa tabia hizo za Mtume  anaelezea ukweli wa kidhahania kwa maelezo ya kushangaza kwa kusema:

“Akili yangu iliuliza moyo wangu: imani ni kitu gani? Moyo wangu ukaliinamia sikio la akili yangu na kuiambia: imani ni adabu”.

### **Ushujaa Wa Mtume**

Hatuwezi kufikiria kuwa kuna shujaa zaidi ya Mtume  kwa sababu katika maish yake yote hakuonekana kuwa na hofu wala wasiwasi.



Mtume ﷺ alikuwa akionyesha uvumilivu na umadhubuti katika kukabiliana na nyakati ngumu na kamwe hakuingiwa wala kughilibiwa na hofu na woga wakati wowote ule.

Mtume ﷺ akisoma aya mbili zifuatazo za surat Yasin, alipita kishujaa na bila wasiwasi katikati ya safu za maadui waliokuwa wakimsubiri ili wamuuwe:

إِنَّا جَعَلْنَا فِي أَعْنَاقِهِمْ أَغْلَالًا فَهِيَ إِلَى الْأَذْقَانِ فَهُمْ  
مُقْمَحُونَ وَجَعَلْنَا مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ سَدًّا وَمِنْ خَلْفِهِمْ  
سَدًّا فَأَغْشَيْنَاهُمْ فَهُمْ لَا يُبْصِرُونَ

*“Tumeweka makongwa shingoni mwao, yakawafika videvuni. Kwa hivyo vichwa vyao viko juu tu. Tumeweka kizuizi mbele yao, na kizuizi nyuma yao, na tumewafunika macho yao; kwa hivyo hawaoni.”* (Yasin: 8 – 9)

Sayyidna Ali ؑ anaelezea ushujaa wa Mtume ﷺ akisema:

“Wakati vita vya Badr vikiendelea na kushtadi sana, tulikuwa tukijikinga nyuma ya Mtume ﷺ. Siku hiyo yeye ndiye aliyekuwa karibu zaidi na safu za maadui ... yeye ndiye aliyekuwa na ujasiri kuliko watu wote.” (Ahmad, I, 86)

Maelezo kama hayo yametolewa na Bara ؑ kuhusu ushujaa wa Mtukufu Mtume ﷺ:

“Wallahi, kila vita vinapopamba moto na kushtadi, tulikuwa tukitafuta hifadhi nyuma ya Mtume ﷺ. Shujaa kati yetu



ni yule aliyekuwa akimfuatia Mtume ﷺ katika kuziendea safu za maadui” (Muslim, Jihad, 79)

Siku zote alikuwa akipambana katika safu zambele katika vita ili klinua neno la Mwenyezi Mungu.

Katika vita vya Hunayn, ambapo mwanzoni jeshi la Waislamu lilitikisika, yeye hakutikisika bali alionyesha ushujaa na ujasiri wake akajitupa katika safu za maadui na kuamsha hamasa na ushujaa wa masahaba zake. Mwisho waliweza kupata ushindi kwa msaada wa Allah Mtukufu.

Alikuwa akisema:

“Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake, ningetamani kupambana katika njia ya Mwenyezi Mungu nikauawa kisha nikafufuliwa kupambana tena nikauawa tena na tena...” (Muslim, Imaraha, 103)



### **Upole Wa Mtume ﷺ**

Mtume ﷺ alikuwa mpole na muungwana kuliko watu wote. (Muslim, Hajj, 137)

Bibi Aisha akizungumzia upole na uungwana wa Mtume ﷺ anasema:


*“Hakuna aliyekuwa na tabia njema kama Mtume ﷺ. Anapoitwa na mmoja wa wanafamilia yake au rafiki zake alikuwa akiitika wito kwa namna ya upole. Ni kutokana na tabia zake za hali ya juu kwamba Allah Mtukufu aliteremsha aya isemayo "hakika wewe ni mwenye tabia za juu" (Al-Qalama, 4)” (wahidi, uk. 463)*




Katika maisha yake yote hakuwahi kulipiza kisasi kwa kosa analotendewa yeye, badala yake alipendela kusamehe. Kwa mara nyingine, Bibi Aisha  anatumieze mambo mengi yanayohusu uungwana wa tabia na maadili ya hali ya juu ya Mtume . Anasema:


*“Kamwe hakuwahi kupiga mtu yeyote... hakulipiza ubaya kwa ubaya bali kwa msamaha na uungwana. Siku zote alikaa mbali na shari. Hakuwahi kulipiza kisasi binafsi. Hakuwahi kumdhulum mtumwa wala mtumishi, na hata mnyama”.*<sup>26</sup>

Maelezo yafuatayo yamesimuliwa na Anas  kuhusu Mtukufu Mtume :

*“Sikuwahi kugusa satini au harirui iliyo laini kuliko miko-no ya Mtume . Sikuwahi kunusa harufu nzuri yenye kunukia kuliko harufu yake. Nilimtumikia kwa kipindi cha miaka kumi. Hakuwahi kuniambia “Akh!” wala kuuliza ‘kwanini umefanya hivi?’ na ‘kwa nini hujafanay hivi?’”* (Bukhari, Sawm, 53, Manaqib, 23; Muslim, Fadhail, 82)

Siku moja Mtume  alimsifu mmoja wa masahaba wake akisema:

*“Una sifa mbili zinazopendwa na Allah: Upole (hilm) na busara”.* (Muslim, Iman 245. 26)

Siku moja Bedui mmoja alikojoa ndani ya msikiti wa Madina. Kwa aharaka sana masahaba wakaanza kumkaripia mpaka Mtume  akaingilia kati na kuwaambia:

---

26. Muslim, Fadhail, 79.



“Muacheni mtu huyo. Mwageni maji ya kutosha mahali alipokojoa ... kwani mmeagizwa kurahisisha mambo wala sio kufanya uzito katika mambo”. Kisha Mtume kwa upole, ulaini na hekma akamueleweshwa umuhimu nan adabu za msikiti.

Anas akizungumzia upole wa Mtume anasema:

“Nilikuwa nikitembea na Mtume akiwa amevaa joho la Kinajrani lenye ukingo mzito. Bedui mmoja akaja na kulivuta sana kwa nyuma kiasi kwamba ukingo wa joho hilo ukaacha athari mabegani mwa Mtume na kusema kwa sauti ya juu:

‘Ewe Muhammad! Waamuru wanipe mali ya Mungu uliyonayo!’

Mtume akageuka huku akitabasamu, kisha akaagiza apewe mali”. (Bukhari, Khumus 19, Libas 18, Adab 68; Muslim, Zakat 128)

Mafanikio makubwa aliyoyapata Mtume katika kuwalingania watu yalipatikana kutokana na tabia yake hiyo nzuri ya upole. Allah Mtukufu analielezea hili kwa kusema:

“Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia” (Ali Imran: 159)


Kwa hakika watu wa enzi za Jahilia walikuwa wakiyeyuka kama mshumaa mbele ya tabia ya uungwana ya Mtume na mbele ya maadili yake mema, upole na tabia yake ya kusamehe. Wakaokolewa dhidi ya unyama na tabia zao mbaya wakawa kama kipepeo wakiizunguka nuru yake tukufu. Kwa sababu Mtume hakuleta hasara kwa wanadamu, bali alikuwa muongozo na rehema kwao.




## Huruma Ya Mtume

Mtume  anasema katika hadithi tukufu:

“Wenye huruma atawahurumia Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma. Wahurumieni walio ardhini atakuhurumieni aliye mbinguni”. (Tirmidhi, Birr, 16/1924)

Huruma kubwa aliyokuwa nayo Mtume  – pamoja na sifa nyingine njema – inajionyesha wazi katika kumpa mama mmoja ruhusa ya kufupisha sala yake kutokana na kuwa na mtoto aliyekuwa akilia.



Mtume  aliposikia mtoto akilia alihofu kuwa mama yake atapata tabu hivyo akafupisha sala yake ili kwamba mama huyo apate kumuangalia mwanaye.

Alikuwa akiswali usiku kucha na macho yake yakibubujika machozi akiuombea umma wake. Muda wake wote alikuwa akiutumia katika kuwaokoa watu dhidi ya moto.

Kwa kuwa alitumwa kuwa rehma kwa walimwengu wote, basi huruma yake na mapenzi yake kwa kila kiumbe.

Siku moja aliombwa kuwalaani makafiri, akasema:

“Hakika Mimi sikutumwa duniani kuja kulaani, bali nimetumwa kuwa rehma”. (Muslim, Fadhail, 126; Tirmidhi, Daawat, 118)

Mtume  alipokwenda katika mji wa Taif kulingania Uislamu, alipigwa mawe na watu wajinga na wenye ubinafsi katika mji huo. Akaja Malaika wa milima akiwa pamoja na Jibril na kumwambia Mtume  kuwa:



“Ukitaka nitaiporomosha milima hii miwili na kuwaangamiza”. Lakini Mtukufu Mtume ﷺ alikataa na kusema:

“Hapana, bali ninapenda Mwenyezi Mungu atoe katika migongo yao kizazi kitakachomuabudu Mwenyezi Mungu peke yake bila kumshirikisha na chochote”. (Bukhari, Bad’ul-Khalq, 7; Muslim, Jihad, 111)

Ama kuhusu watu wa Taif waliomfukuza katika mji wao, wakamtukana kwa matusi mabaya kabisa, wakaamiliana naye kwa ukali mpaka mwaka wa tisa wa Hijra, Mtume ﷺ aliwaombea akisema:

“Ewe Allah! Waongoze watu wa Thaqif na uwalete kwetu kwa hiari yao”. Aliendelea kuwaombea na hatimaye wakaja Madina na kuingia katika Uislamu kwa hiari yao. (Ibn Hisham, IV, 134; Tirmidhi, Manaqib, 73/3942)

Siku moja Abu Usayd ﷺ alikuja kwa Mtume ﷺ akiwa na baadhi ya mateka wa vita kutoka Bahrain. Mtukufu Mtume ﷺ akamuona mateka mmoja wa kike akilia, akamuuliza sababu ya yeye kulia.

Akasema: “Mtu huyu amemuiza mwanangu”.

Mtume ﷺ akamuuliza Abu Usayd ﷺ: “Umefanya hivyo?”

Akajibu: “Ndiyo”.

Akauliza: “Kwa nani?”

Akajibu: “Kwa Bani Abs”.

Mtume ﷺ akamuamuru kwamba:

“Panda farasi wewe mwenyewe ukamlete huyo mtoto”.





Huruma na upole wa Mtume ﷺ vilienea dunia nzima. Siku moja aliwaambia wafuasi wake waliokuwa karibu naye:

“Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mikononi mwake, hamtoimgia peponi mpaka mhurumiane”.

Wakasema:

“lakini sisi ni wenye kuhurumiana”.

Akasema: “Huruma ya kweli sio kuhurumiana nyinyi kwa nyinyi tu, bali kuwahurumia viumbe wote; ndiyo, kuwahurumia viumbe wote”. (Hakim, IV, 185/7310)

### **Mtume ﷺ Mwenye Kusamehe**

Allah ﷻ anapenda kusamehe. Mwenyezi Mungu ameahidi kumsamehe yule atakayetubu kwa dhati akayajutia makosa yake.

Kwa kuwa Yeye Allah ni mwingi wa kusamehe, vivyo hivyo anawataka waja wake wawe wenye kusamehe. Sharti la kupata msamaha wake ni mhusika kujuta, akatii maamrishi ya Mwenyezi Mungu na akajiepusha na haramu.

Mfano mzuri wa kuwasamehe watu wengine unapati-kana katika maisha ya Mtume wa rehma ﷺ.

Siku ya ufunguzi wa Makka alimsamehe Hind, mwanamke ambaye hapo kabla alilitafuna ini la Sayyidna Hamza ﷺ wakati wa vita vya Uhud.

Habbar ibn Aswad alikuwa miongoni mwa maadui wakubwa wa Uislamu. Alipigwa mkuki ngamia aliyekuwa



amepandwa na Zainab binti wa Mtume ﷺ wakati akihamia Madina akadondoka chini na kuumia vibaya sana, na zaidi ya hapo Bibi Zainab alikuwa na ujauzito na hivyo mimba yake ikaharibika.

Jambo la kusikitisha zaidi ni kuwa maumivu hayo yali-  
pelekea kifo chake muda mfupi baada ya tukio hilo. Habbar  
alitenda makosa mengi sana yasiyokuwa na idadi.

Siku ya ufunguzi wa Makka alikimbia na akawa hajaka-  
matwa.

Siku moja Mtume ﷺ alipokuwa amekaa pamoja na mas-  
wahaba zake mjini Madina, mara akatokea Habbar na kusi-  
mama mbele ya Mtume ﷺ na kutangaza kuwa tayari ames-  
haingia katika Uislamu. Sio tu kwamba Mtume ﷺ alimsame-  
he, bali pia aliwakataza watu kumtukana na kumuaibisha.  
(Waqidi, II, 857 – 858)

Adui mwingine maarufu dhidi ya Uislamu ni Ikrimah  
bin Abi Jahl. Siku ya ufunguzi wa Makkah alikuwa amekim-  
bilia Yemen. Baada ya tabu kubwa, Ikrimah alishawishiwa na  
mkewe kwenda kuomba msamaha kwa Mtukufu Mtume ﷺ,  
ambapo alifika akiwa Mwislamu.

“Karibu ewe mpanda farasi mwenye kutangatanga”,  
Mtume ﷺ alimkaribisha kwa amani bila kumkumbusha  
makosa yake ya zamani, akamsamehe. (Tirmidhi, Isti’zan, 34/2735)

Mara nyingi Mtume ﷺ alikuwa akimuomba Mwenyezi  
Mungu kwa kusema: “Ewe Allah, wasamehe watu wangu  
kwani hawatambui”. (Ibn Majah, Manasiq, 56; Ahmad, IV, 14)



Kiongozi wa Yamamah, Sumamah ibn Usal, alipoingia katika Uislamu alikata mahusiano yote ya kibiashara pamoja na Maquraishi wa Makka waliokuwa wakiitegemea Yamamah kwa haja zao zote. Walipojikuta katika hali ngumu ya njaa na ukame walikwenda kwa Mtume ﷺ kumuomba aingilie kati. Mtume ﷺ akamuandikia barua ya kumtaka asikate mahusiano ya kibiashara na watu wa Makkah.<sup>27</sup>

Washirikina hawa wa Makka walisahau kuwa wao ndio waliowanyima Waislamu chakula na maji kwa muda wa miaka mitatu wakihangaika katika jangwa la Abu Talib. Lakini Mtukufu Mtume wa rehma ﷺ aliwasamehe.

Vilevile katika mwaka wa saba wa Hijra, baada tu ya ufunguzi wa Khaybar, Mtukufu Mtume ﷺ aliwasaidia watu wa Makka waliokuwa wakikabiliwa na ukame wa kutisha akawapa dhahabu, ngano na mbegu za tende.

Baada ya kuupokea msaada huu, Abu Sufiani aliugawa kwa watu maskini wa Makka akaonyesha shukrani yake kwa kusema:

“Mwenyezi Mungu amlipe mtoto wa ndugu yetu kwa kuwakumbuka ndugu zake...” (Yaqubi, II, 56)

Nyoyo zao zikiwa zimelainika na kupiga magoti mbele ya haya matendo yenye kuvutia, watu wa Makka walijikuta wakiukubali Uislamu kwa moyo mmoja.

---

27. Ibn Abdil – Barr, al- istiab, Cairo ts, I, 214; Ibn Athir, Usdul – ghaba, Cairo, 1970, I, 295.



Mtukufu Mtume 🕌 alikisamehe hata kikundi kilichotaka kumuua katika eneo la Hudaybiyyah. Kikundi hicho kilikamatwa na kukiri kupanga njama ya kumuua. (Muslim, Jihad, 132, 133)

Baada ya ufunguzi wa Khaybar, mwanamke mmoja alim-uwekea sumu Mtume 🕌 katika chakula. Mtume 🕌 akaigundua sumu hiyo wakati alipotaka kula kipande cha nyama. Licha ya mwanamke huyo kukiri kupanga njama hiyo ya kiovu, Mtume 🕌 alimsamehe. (Bukhari, Tibb, 55; Muslim, salam, 43)

Kupitia *wahyi* (ufunuo), Mtukufu Mtume 🕌 aligundua kuwa Labid na wenzake walikuwa wakijaribu kumroga. Lakini Mtume 🕌 hakutaja hata kidogo kosa la Labid na wala hakutaka kumuadhibu kwa uhalifu wake.

Kamwe hakutaka kulipiza kisasi kwa kumuua Labid na Wayahudi wenzake wa Banu Zurayq.<sup>28</sup>

Katika hilo Qur'an Tukufu inasema:

*“Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuuze wajinga.”* (Al- Araf, 199)

Wanahikma – ambao wameweza kuwa karibu na Mtume 🕌 kwa kumpenda na wakawa na sehemu ya msamaha wake – siku zote walikuwa wakishikamana na njia ya kusamehe kwa matumaini ya kupata msamaha wa Mola wao. Mfano wa watu hao ni Hallaj Mansur. Alipokuwa akipigwa mawe alikuwa akimuomba Allah Mtukufu kwa kusema:

“Mola wangu! Msamehe anayenipiga mawe kbala ya kunisamehe mimi”.

---

28. Tazama: Ibn Sad, II, 197; Bukhari, Tibb, 47; Muslim, salam, 43; Nasai, Tahrim, 20; Ahmad, Iv, 367, VI, 57; Ayni, XXI, 282.



## Mtume ﷺ Na Kuchunga Haki Za Jirani

Mtume ﷺ alikuwa akitilia umuhimu mkubwa sana katika kulinda haki za jirani. Kwa hivyo, anasema katika hadithi tukufu: “Jibril aliendelea kuniusia sana kumtendea wema jirani mpaka nikadhani kuwa jirani naye angekuwa miongoni mwa warithi wa mtu.” (Bukhari, Adab, 28; Muslim, Birr, 140 – 141)

Katika hadithi nyingine anasema:

“Jirani asiyekuwa Mwislamu ana haki moja. Jirani Mwislamu ana haki mbili. Mwislamu ambaye pia ni ndugu ana haki tatu.”<sup>29</sup>

Kuchungulia katika dirisha la jirani, kumnyima raha kwa harufu hata ya chakula na kufanya mambo ya maudhi yasiyopendeza ni miongoni mwa uvunjaji wa haki za jirani. Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ anasema: “Jirani aliye bora mbele ya Allah ni yule mwenye kumfaa jirani yake.” (Tirmidhi, Birr, 28)

“Si Mwislamu wa kweli yule anayelala ameshiba hali ya kuwa jirani yake yu na njaa.” (Hakim, II, 15/2166)

Abu Dharr Ghifari  anasema:

“Kila nilipotaka kupika, Mtume ﷺ alikuwa akiniambia niongeze maji na kugawana na jirani yangu.” (Ibn Majah, Atimah, 58)

Kutokana na ukweli kwamba Abu Dharr alikuwa miongoni mwa masahaba maskini zaidi, hivyo ina maana kuwa hata umaskini sio kisingizio cha kutochunga haki za jirani.

---

29. Suyut, al – Jamius – saghir, Misri, 1321, I, 146.



Imesimuliwa na Abu Hurayra kuwa, siku moja Mtume 🕌 alisema: “Wallah si muumini wa kweli! Wallahi si muumini!”

Masahaba wakauliza:

“Nani huyo ewe Mtume wa Allah?”

Akasema:

“Yule ambaye jirani yake hajihisi kuwa salama dhidi yake.” (Bukhari, Adab, 29; Muslim, Iman, 73; Tirmidhi, Qiyamat, 60)

Katika riwaya nyingine anasema:

“Hatoingia peponi yule ambaye jirani yake hajihisi kuwa salama dhidi ya madhara yake.” (Muslim, iman, 73)

### **Mtume 🕌 Na Watu Maskini**

Mtume 🕌 alikuwa akiamiliana na maskini, yatima, wajane na wale wenye upweke kwa kuwahurumia, kuwajali na kuwapa umuhimu. (Bukhari, Nafaqat, 1; Muslim, Zuhd, 41 – 42)

Alikuwa akiwapa kipaumbele cha hali ya juu ili wasin-yongeke kwa hali zao za umaskini.

Abu Said 🕌 anasimulia kuwa:

“Nilikuwa nimekaa pamoja na kundi la watu maskini katika *Muhajirina*. Baadhi yao, kutokana na kutokuwa na mavazi ya kutosha kustiri miili yao, walikuwa wakijikinga nyuma ya wenzao ili kujistiri. Mtu mmoja alikuwa akitusomea Qur’an nasi tukisikiliza. Mara akatokea Mtukufu Mtume 🕌 akasima na kusubiri. Alipowasili, yule msomaji akaacha kusoma. Kisha Mtume 🕌 akatusalimia na kutuuliza:



‘Mnafanya nini?’

Tukasema:

‘Huyu ni mwalimu wetu, anatusomea Qur’an nasi tuna-sikiliza.’

Mtume ﷺ akasema:

“Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyejaalia katika ummah wangu watu ambao nimeamrisha kuisubirisha nafsi yangu pamoja nao.”<sup>30</sup>

Hapo Mtume ﷺ akakaa katikati yetu ili kutoa haki sawa baina yetu sote. Akatuashiria kwa mkono wake tutengeze mkao wa duara. Tukakaa katika muundo wa duara huku tukimuelekea. Ndipo akatupa habari njema akisema:

“Furahini enyi *Muhajirina* maskini! Ninawapa habari njema ya kupata nuru kamili siku ya Kiyama. Mtaingia peponi nusu siku kabla ya matajiri... nusu siku hiyo ni sawa na miaka mia tano ya duniani!” (Abu Dawud, ilm, 13/3666)

Siku moja kundi moja la watu lilifika Madina likiwa halina viatu miguuni, wamedhoofika na kukonda kwa sababu

---

30. Mtume ﷺ anaashiria kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: “Subirisha nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola wao asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka radhi yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia. Wala usimtii tuliyemghafilisha moyo wake asitukumbuke, na akafuata matamania yake yakawa yamepita mpaka” (Al – Kahf: 28).

Katika ayah ii, Allah anamtaka Mtume wake ﷺ kuwa na subira na uvumilivu kwa wanyonge na maskini ambao wameuitikia wito wa Uislamu na awe nao bega kwa bega katika shida zinazoweza kuwakuta, na aamiliane nao kwa wema mkubwa.



ya njaa na jua kali. Mtukufu Mtume ﷺ aliguswa sana na hali yao kiasi kwamba uso wake ukapauka. Akaingia na kutoka kisha akamuamuru Bilal atoe adhana. Baada ya masahaba kukusanyika aliwatanabahisha juu ya hali mbaya ya watu hao. Masahaba wakajitolea kuwasaidia, na hapo Mtume ﷺ akapata ahueni moyoni mwake. (Muslim, Zakat, 69 – 70; Ahmad, IV, 358, 361)

Hivyo, maisha ya Mtume ﷺ yalikuwa kama mnara unavutia wa huruma, upole na upendo wa dhati.

Mara zote alikuwa akimuusia mkewe, Bibi Aisha akisema:

“Ewe Aisha, usiwafukuze maskini hata kwa kipande cha tende. Wapende na uwe karibu nao ili Allah naye akuweke karibu siku ya Kiyama” (Tirmidhi, Zuhd, 37/2352)

Abbad ibn Shurahbil  anasimulia akisema:

“Mwaka mmoja nilipatwa na janga la njaa, nikaingia katika shamba miongoni mwa mashamba ya Madina ili nipate chochote cha kula. Nilikusanya nafaka kidogo, baadhi yake nikala na baadhi nikazijaza katika mkoba wangu. Mara, mwenye sahama akaja, akanipoga na kuninyang’anya mkoba na kisha akanipeleka kwa Mtume ﷺ.

Mtume ﷺ akamwambia:

‘Hukumuelimisha alipokuwa hajui, wala hukumlisha alipokuwa na njaa’, akamtaka anirudishie mkoba wangu.


Kisha Mtume ﷺ alinipa chakula cha kutosha.” (Abu Dawud, Jihad, 85/2620 – 2621; Nasai, Qudat, 21)





Hadithi hii inaonyesha kuwa Uislamu unahimiza kufanya uchunguzi kwanza wa chanzo cha kosa husika, kisha ifanyike juhudi ya urekebishaji wa kosa hilo. Ni kwa mtazamo huu kwamba adhabu mbalimbali zitolewazo na sheria ya Kiislamu zinafanana na adhabu zitolewazo na baba na mama kwa mtoto wao. Lengo lake sio kumfukuza na kumpiga marufuku mhalifu, bali kumrejeshwa upya katika maisha sahihi ya kijamii.

### **Mtume ﷺ Na Mateka Wa Vita Na Watumishi**

Huruma ya Mtume ﷺ iliwaenea hata mateka wa vita, ambapo siku zote alikuwa akitaka watendewe wema. Ushahidi wa kusisimua unatolewa na Abu Aziz, nduguye Mus'ab ibn Umayr :

“Nilikuwa miongoni mwa mateka wa vita vya Bdri nikakabidhiwa kwa kundi la *Ansar*. Amri ya Mtume ﷺ ya kuwaten-dea wema mateka wote wa vita ilitangazwa kwa kila mtu, lakini jukumu lililofanywa na *Ansar* katika utekelezaji wa amri hiyo halikuwa la kawaida. Wakati wa chakula cha mchana na usiku walikuwa wakinipa fungu lao la mikate mizuri nao wakila tende tu. Nilikuwa nikitahayari na kuirudisha mikate hiyo lakini hakuna ambaye angekubali kuipokea.” (Haythami, VI, 86; Ibn Hisham, II, 288)

Mtume ﷺ alikusudia kuondosha mfumo wa utumwa uliokuwa umedumu kwa muda mrefu na akachukua hatua kubwa katika kufikia lengo hilo. Katika kila fursa aliyopata, alihamasisha kuwaacha huru watumwa, akatangaza kuwa kitendo hicho ni ibada kubwa.



Pindi Mwislam anapofanya kosa fulani alitakiwa kumua-cha huru mtumwa kama fidia ya kosa lake hilo. Kutokana na uhamasishaji huu, rafiki yake wa karibu, Abu Bakr ؓ alitumia sehemu kubwa ya mali yake kuwakomboa watumwa.

Siku moja Mtume ﷺ alimuona Abu Dharr akimtendea vibaya mtumwa pasipo kujua. Akionyesha kuhuzunishwa na kitendo hicho, alimuonya kwa kumwambia:

“Yaonekana bado unafuata mila na desturi za kijahilia.”

Kisha akaendelea kusema:

“Usikidhuru kilichoumbwa na Allah. Iwapo huyo mtumwa haendani na mwenendo wako, basi muache huru. Usimpe kazi zilizo nje ya uwezo wake; na iwapo utampa kazi basi msaidie.” (Bukhari, Iman, 22; Muslim, Ayman, 38; Abu Dawud, Adab, 123 – 124)

Mtu mmoja aliwafungisha ndoa watumwa wake wawili, baadaye akataka kuwatenganisha. Mtumwa wa kiume akapeleka mashtaka yake kwa Mtume ﷺ. Mtume akamwambia bwana huyo:

“Acha jambo lako hilo ... huna haki juu ya kuoana kwao na kuachana kwao.” (Ibn Majah, Talaq, 31; Tabarani, Kabir, XI, 300)

Katika kukabiliiana na matendo kama hayo, wakati wote maswahaba walikuwa wakipendelea kuwaacha huru watumwa kuliko jambo lingine, na hivyo utumwa ukapata kuko-meshwa hatua kwa hatua mpaka sasa. Hii ina maana kwamba, Uislamu uliondosha mnyororo wa utumwa shingoni mwanadamu, utumwa ambao ulikuwa katika historia ya mwanadamu kutokana na athari za vita.



Mara zote Uislamu ulikuwa ukimuamuru anayemiliki mtumwa amlishe chakula anachokula yeye na amvishe kile anachovaa yeye, asimpe kazi ngumu na agharamie mahitaji yake yote. Uislamu ulibainisha kuwa kuwaacha huru watumwa ni tendo jema na ni njia ya uhakika na ya haraka sana ya wokovu kwa waumini. Zikawekwa haki za watumwa zinazotakiwa kulindwa kiasi kwamba zinamfanya yule asiyekuwa na mtumwa awe bora kuliko yule mwenye mtumwa, na kwa kiasi kwamba yule mwenye mtumwa anakuwa sawa na mtumwa mwenyewe. Maneno yafuatayo yaliyotamkwa na Mtume ﷺ katika saa za mwisho za uhai wake, yanafaa kutafakariwa na kuzingatiwa sana.



“Kuweni makini na swala, kuweni makini na swala! Muogopeni Mwenyezi Mungu katika wale walio chini ya mikono yenu.” (Abu Dawud, Adab, 123 – 124/5156; Ibn Majah, Wasaya, 1)


Hivyo, Mtukufu Mtume ﷺ aliifunga milango inayoelekea kwenye utumwa na kuifungua mpaka mwisho milango ya kuwaacha huru, akahamasisha na kuhimiza suala hilo katika kila fursa iliyopatikana. Je kuna njia bora ya kukomesha utumwa kuliko hii?

Maelezo yafuatayo yanatosha kuweka wazi daraja ambayo Uislamu uliwainua watumwa:

Licha ya ukweli kwamba Bilal Al- Habashi kabla ya kusilimu alikuwa mtumwa, lakini baada ya kusilimu Mtume ﷺ alimfanya kuwa muadhini mkuu na kiongozi wa waadhini wote ulimwenguni. Mfano mkubwa wa hilo tunaona juu ya kuta za misikiti mingi duniani pameandikwa: *Ya hadhrat Bilal Al- Habashi!*



Mtu mwingine ni Zaid ibn Harithah, ambaye alikuwa mtumwa aliyetolewa na Bibi Khadija kama zawadi kwa Mtume  naye Mtume akamuacha huru. Swahaba huyu alikuwa mfano mkubwa wa unyooфу wa hali ya juu na maisha yaliyojaa upendo mkubwa kwa Mtume .

Vilevile, mwanaye wa kiume, Usamah aliteuliwa na Mtume  kuwa kamanda wa jeshi la Kiislamu akiwa bado kijana mdogo.

Tariq ibn Ziyad, aliyeifungua Hispania, alikuwa mtumwa aliyekuwa akifungwa mnyororo shingoni mwake akiuzwa na kununuliwa. Lakini kwa sababu ya Uislamu alinyanyuliwa kwenye daraja inayolingana na utu na hadhi yake ya ubinadamu, na akawa kamanda wa jeshi la Waislamu.

Kwa kifupi, Uislamu uliwabadilisha watumwa kuwa mabwana. Hiyo ndiyo iliyokuwa sababu kubwa ya Washirikina wa Makka kuupiga vita Uislamu. Sasa je, wapinzani na makafiri wa karne ya 21 hawafanyi kitu hichohicho? Je madhalimu wa leo hawajawafanya watu wengi walio huru kuwa watumwa? Je hawatunii jina la uhuru kupokonya haki za wanyonge na watu wasiokuwa na hatia ili kupora rasilimali zao? Je kuna tofauti gani kati ya ukandamizaji wa zamani na mfumo mpya wa utumwa usiokuwa na huruma unaofanywa ulimwenguni kote kwa kutumia majina na kaulimbiu zenye kuvutia?

Kwa hivyo, Uislamu ambao ulikomesha utumwa kwa misingi na kanuni zake za hali ya juu na kumnyanyua mwanadamu, ndio unaoweza kutoa tiba sahihi kwa binadam. La sivyo, ubinadamu utaangukia katika makucha ya fikra za kinyonyaji ambazo hutumia jina la uhuru kuwatia watu utumwani.



Kuna tofauti kubwa sana baina ya maovu ya ukoloni unaoendelea kunyonya damu za wanyonge na kuwatia utumwani, na baina ya misngi ya Kiislamu ya hali ya juu nay a kudumu ambayo kila mara ilitoa ulinzi madhubuti kwa mateka wa vita na watumishi, na ambayo inaelezwa na Mtukufu Mtume ﷺ katika maneno yake matukufu:

“Ni ndugu zenu ... wapeni mavazi kama mnayovaa nyinyi na wapeni chakula mnachokula nyinyi.”<sup>31</sup>

Kwa hakika njia pekee ya kumkomboa mwanadamu wa leo ndio njia ileile iliyomkomboa hapo zamani, nayo ni kufuata muongozo wa Mtume ﷺ na kushikamana nao. Yeye aliweka vipimo madhubuti vya namna ya kuamiliana na watu. Alimpa mwanadamu hadhi yake na hakuwa akibagua kati ya maskini na tajiri, kiongozi au raia, bwana au mtumishi.

Baadhi ya maswahaba walikuja kwa Mtume ﷺ na kumuuliza iwapo walitakiwa kuwasamehe watumishi wao mara ngapi. Akawausia akisema: “Wasameheni mara sabini kila siku.” (Abu Dawud Adab, 123 – 124; Tirmidhi, Birr, 31/1949)

Wosia ufuato wa Mtukufu Mtume ﷺ ambaye ni bahari isiyokuwa na ufukwe, unafichua kiwango kisichoelezeka cha kuwajali watu wengine:

“Watumishi wenu wanapowaletea chakula, kama hamtokaa nao, basi angalau wapeni sehemu ya chakula hicho ... kwani wao ndio wanaovumilia joto na shida katika kupika.” (Bukhari, Atimah, 55; Tirmidhi, Atimah, 44)

---

31. Muslim, Ayman, 36 – 38.



Lau Allah akitaka anaweza kufanya mambo kuwa kinyume kwa kumfanya mtumishi kuwa bwana na bwana akawa mtumishi. Hivyo tunawajibika kumshukuru Allah na kuishi vema na wale walio chini ya uangalizi wetu.

### **Muamala Wa Mtume ﷺ Kwa Wanawake**

Mwanamke katika zama za ujahilia alikuwa akiamiliwa kwa muamala unaoondosha utu wake kama mwanamke na kama mtu anayestahiki kuheshimiwa. Watu wa zama hizo walikuwa wakiwazika hai watoto wao wa kike bila huruma yoyote ile kwa hofu ya kupata aibu. Nyoyo zao za mawe zilikuwa zikitenda jinai hiyo mbaya ili kujinda na balaa walitengenezalo katika akili zaokwa ujinga tu.

Allah Mtukufu anaelezea hali yao hii ndani ya Quran tukufu 66 na mmoja wao anapopewa habari ya kuzaliwa mtoto wa kike, uso wake huwa mweusi, naye kajaa chuki” (an - Nali 16:58)

Watu wa zama za ujahiliya (yaani kabla ya Uislamu) walikuwa wakiamiliana na wanawake na mabinti kwa namna inayoshusha thamani yao. Walikuwa wakiwafanya kama chombo cha kujistareheshea na kukidhi matamania yao. Ni pale alipokuja Mtume ﷺ akaweka misingi ya haki za wanawake, na hapo mwanamke akawa alama ya staha na wema katika jamii. Taasisi ya umama ikawa alama ya utukufu.

Sifa iliyotolewa na mtume ﷺ katika hadithi tukufu isemayo:



“Pepo ipo chini ya nyayo za akina mama”<sup>32</sup> inaonyesha kwamba mwanamke alifika kwenye kilele cha heshima, hadhi na cheo anachostahili.

Upole, huruma na adabu aliyokuwanayo Mtume ﷺ kwa wanawake inabainika vyema kama tukio lifuatalo: siku moja akiwa safarini, kijana aliyekuwa naye aitwaye Anjasha alianza kughani ili kuongeza mwendo wa ngamia.<sup>33</sup> Kwa kuhofia kwamba mwendo kasi wa ngamia unaweza kuidhuru miili ya wanawake walio wapanda, Mtume ﷺ akamwambia kijana huyo:

“kuwa makini, Anjasha, usivunje vioo!” (Bukhari, Adab,95; Ahmad, III,117)

Katika hadithi nyingine Mtume ﷺ alisema:

“Ewe Allah! Hakika mimi ninaumizwa na watu wanaovunja haki za watu wawili waliodhaifu; yatima na wanawake.” (Ibn majah, Adab, 6)

“Mwislam hatakiwi kumchukia mkewe, kwani kama ana tabia asiyoipenda, kuna nyingine anayoipenda.” (Muslim, Rada, 61)

Wanawake si mashamba ya miba mpaka wastahiki kuchukiwa na kubughudhiwa, bali ni mabustani yanayostahili heshima ya kupendwa; na kimsingi upendo huu ni zawadi na tunu adhina kutoka kwa Allah Mtukufu. Kuhusu hilo Mtu-kufu Mtume ﷺ anasema katika hadithi tukufu;

32. Nasai, Jihad, 6; Ahmad, III, 429; Suyut, I, 125.

33. Ngamia huvutiwa na ghani ya sauti nzuri, hivyo wachungaji wanapoghani kwa sauti ya kuvutia huwafanya ngamia waende kwa kasi.



“katika dunia yenu, nimefanywa kuwa mwenye kupenda wanawake na manukato ... Na swala imefanywa kuwa tulizo la macho yangu” (Nasai, Ishratun-Nisa, 10; Ahmad, III,128,199)

Mwanamke ambaye kupitia kwake binadam ameletwa duniani, ameonekana kuwa kipenzi cha Mtume ﷺ na hivyo hatakiwi kuangaliwa kwa mtazamo wa kijahiliya.<sup>34</sup> Yatajuwa ueleweke kwamba upendo huu uliwekwa na Allah ndani ya maumbile na silica, nasilika hiyo ikawekwa katika daraja ya kuwa tayari kwa ajili ya upendo wa juu zaidi. Hivyo upendo wa Mtume ﷺ kwa wanawake haukuwa upendo wa kawaida, bali ni upendo uliokusudia kuwapa hadhi na heshima ya juu wanayostahili. Katika historia ya binadamu mwanamke amepata hadhi yake hiyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia dini tukufu ya Uislam. Kwa hakika mifumo yote iliyoada kumpa mwanamke hadhi yake – isipokuwa Uislam imem-

---

34. Katika ndoa zote za Mtukufu Mtume ﷺ hatuwezi kuona aina yoyote ya mwelekeo wa matamano na mhemko wa kinafsi. Katika ujana wake hakuo binti mdogo, na mkewe wa kwanza alikuwa mjane mwenye watoto ambaye alikuwa na miaka arobaini, yaani Bibi Khadija ؓ; na aliishi naye maisha matamu ya umri wake. Baada ya kifo cha bibi huyu, mtume ﷺ alikuwa na umri wa utu uzima, na wanawake wote aliwaoa aliwaoa baada ya kufikisha miaka hamsini na nne, na hakuwaoa kwa matamano yake binafsi, bali kwa amri ya Mwenyezi Mungu, pamoja na hekima nyingine nyingi, ndoa hizo zililenga hasa kuwafanya wawe walimu kwa wanawake wa kiislam. Vile vile, wanawakewengi walioolewa na Mtume ﷺ walikuwa watu wazima wenye umri mkubwa, wasiokuwa na jamaa na wengi wakiwa na watoto. Hivyo, mafanikio makubwa aliyoyapata Mtume ﷺ katika kazi yake ya utume yanaonyesha wazi kwamba ndoa hizo zilifanyika kwa maelekezo ya Mwenyezi Mungu kwa lengo la kufikisha Uislam kwa watu kwa urahisi mkubwa sana.

Kwa maelezo zaidi, tazama: Othman Nuri Topbas, Hazrat Muhammad Mustafa, I, 130 – 140.





pa hadhi kama chombo tu cha urembo na mapambo, ama kuhusu mambo mengine, ukweli ni kwamba mifumo hiyo imemkanyaga, ikamuangamiza na kumtumia kama bidhaa ya kiuchumi na kujistarehesha.

Kwa hiyo, mtazamo wa leo kuhusu mwanamke unatakiwa uwe juu ya msingi sahihi na adhimu wa Uislam na kuwekwa katika daraja yake anayostahiki mwanamke na mwanaume, tangu mwanzo wa kuumbwa kwao, ni dunia mbili pana zinaz-okamishana. Lakini katika mchakato huu wa kukamishana Allah Mtukufu, amempa mwanamke jukumu muhimu na lili- lokuwa kubwa zaidi; na kwa nmna hiyo mwanamke anauwezo wa kuzijenga au kuziharibu jamii. Kwa sababu hiyo, Uislam umeifanya kazi ya kumlea mwanamke mwenye kuijenga hadhi ya juu. Mtume ﷺ anabainisha hilo katika hadithi ifuatayo:-

“Mwenye kuwa na mabinti watatu au dada watatu, akawa- tunza na kuwalea vizuri akawaozesha na kwendelea kuwa- saidia, basi ataingia peponi.” (Abu Dawud, Adab, 120 – 121/5147; Tirmidhi, Birr, 13/1912; Ahmad, III, 97)

Mtume Mtukufu ﷺ anasema katika hadithi nyingine:

“Mwenye kuwatunza na kuwalea mabinti zake wawili mpaka wakakuwa, Mimi nay eye siku ya kiyama tutakuwa bega kwa bega kama hivi” alikusanya vidole vyake viwili kama ishara ya kuwa pamoja. (Muslim, Birr, 149; Tirmidhi, Birr, 13/1914)

Katika kusesitiza juu ya hadhi ya mwanamke mwema anasema:

“Dunia ni yenye faida ya muda tu, na wenye manufaa zaidi katika watu wake ni mwanamke mwema, mchamungu.” (Muslim, Rada, 64; Nasai, Nikah, 15; Ibn Majah, Nikah, 5)



Nyuma ya kila mwanaume mwenye mafanikio kuna mwanamke mwema. Kwa mfano, Bibi Khadija(ria) ndiye aliyekuwa mhimili mkubwa mwanzo wa safari ya mahubiri ya Mtume ﷺ. Mtume ﷺ hakumsahau katika umri wake wote.

Vile vile Bibi Fatimah alikuwa na mchango wa wazi katika mafanikio ya sayyidna Ali ﷺ.

Hivyo, mwanamke mwema ndio neema kubwa katika dunia. Ni kwa sababu hii kwamba Mtume ﷺ aliweka sharti ambalo mja mwema hutambuliwa, nalo ni muamala wake mwema kwa wanawake. Anasema:

“Muumini mkamilifu zaidi ni yule mwenye maadili bora zaidi, na mtu mwema zaidi kati yenu ni yule anayeamiliana na kuwatendea wema wanawake.” (Tirmidhi, Rada, 11/1162)

Hivyo, ni uovu mkubwa na utovu wa hadhi kumfanya mwanamke kuwa mahali pa kujistareheshea tu na kumtazama kama chombo cha kukidhi haja ya matamanio na kuutazama mwili wake tu. Hakika kutomheshimu mwanamke ni aina ya upofu dhidi ya sifa zote za juu ambazo Allah Mtukufu alim-tunukia. Kwa sababu mwanamke wa leo anatumiwa kama chombo cha matangazo na ni uvunjifu mkubwa wa heshima, hadhi na thamani ya mwanamke.

Kwa hakika mwanamke anatakiwa, kulelewa na kutunzwa kama mjenzi na muasisi wa kweli wa jamii na walezi kutoka mbinguni wanaolea waledi wa kesho. Hakuna kiumbe aliyewahi kuumbwa anayestahili heshima na upendo wa kweli kuliko mama zetu, ambao wametubeba matumboni mwao kwa kipindi cha muda, wakatulea mikononi mwao mpaka



kifo. Mama mwaminifu ambaye ameyatoa mhanga maisha yake kwa ajili ya familia yake anastahili upendo mkubwa, hes-hima yakina na kushukuriwa kwa kipindi chote cha uhai wetu.

Ama kuhusu harufu nzuri kupendwa na Mtume ﷺ, hes-hima yake inapatikana katika taswira na hisia zitolewazo na harufu hiyo kwenye moyo. Harufu nzuri huleta upepo mwanaana wa baraka na pia hupendwa na malaika. Aidha, harufu nzuri ni alama ya usafi, kwani mtu msafi hutoa harufu nzuri yenye kunukia. Kwa hakika mwili wa mtukufu Mtume ﷺ siku zote ulikuwa ukinukia kana kwamba umepuliziwa kwa mawaridi; zaidi ya hilo nikana kwamba mawaridi yalikuwa yameumbwa kutokana na jasho litokalo mwilini mwake. Pindi anapopapasa kichwa cha mtoto, kichwa hicho kingeendelea kunukia harufu ya miski kwa muda mrefu.

Kuhusu swala, ilifanywa kuwa nuru ya macho ya Mtume ﷺ, kwa sababu swala ni kukutana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa ajili hiyo ni ibada inayotakiwa kutekelezwa kana kwamba mja yuko mbele ya mola wake; na kwa hiyo, swala ni tulizo la macho.

### **Muamala Wa Mtume ﷺ Kwa Yatima**

Allah Mtukufu alimleta duniani kipenzi chake kama yatima ili kuupa uyatima hadhi maalum. Mtume Mtukufu ﷺ alikuwa akionyeshakuguswa sana na malezi ya yatima na akiwaangalia kwa upole wa hali ya juu. Katika Quran tukufu kuna aya nyingi zinazohusu uchungaji wa haki za yatima. Allah Mtukufu katika kitabu chake anawaelekeza watu mambo wanauopaswa kuyafanya kwa yatima:



“Basi yatima usimwonee!” (Surat Dhuh’aa, 93:9)

Kuna hadithi mbali mbali zinazotoa wito kama huo:

“Nyumba yenye faida kubwa kwa Waislam ni ile ambayo ndani yakeyumo yatima anayetendewa wema na nyumba mbaya zaidi ni ile ambayo ndani yake yumo yatima anayetendewa ukatili” (Ibn Majah, Adab, 6)

“Mwenye kumchukua yatima, miongoni mwa waislam, akampeleka nyumbani kwake kumlisha na kumpa mavazi, Allah atamuingiza peponi, isipokuwa kama atafanya dhambi isiyosameheka” (Turmidhi, Birr, 14/1917)

“Mwenye kupapasa kichwa cha yatima kwa upendo kwa ajili ya Allah, atapata thawabu kwa kila unywele utakaoguswa na mkono wake” (Ahmad, 5, 250)

Mtukufu Mtume 🌿 alikuwa akiusia sana watu kutekeleza wajibu wao wa kijamii katika kuwatunza na kuwaangalia yatima:

“Mimi na yule mwenye kumlea vizuri yatima tutakuwa pamoja peponi” alisema hivyo akivikusanya vidole vyake kuonyesha ukaribu watakao kuwa nao pamoja siku hiyo. (Bukhari, Adab, 24)

Siku moja alimshauri na kumuusia mtu mmoja aliyekuja kumlalamikia kuhusu ugumu wa moyo, Mtume 🌿 akamwambia:

“ukitaka kuulainisha moyo wako, basi mlishe maskini na ukipapasa kwa upendo kichwa cha yatima” (Ahmad, II, 263,387)



Kwa mara nyingine mtume ﷺ anafika kwenye kilele cha huruma na upole, anasema ;

“Mimi nipo karibu zaidi na waumini kuliko nafsi zao, mwenye kufariki na kuacha mali basi ni za warithi wake. Laki-ni anapoacha nyuma yake deni binafsi au yatima, basi deni hilo ni langu, na yatima wake nitawatunza” (Muslim, Jumuah, 43; Ibn Majah, Muqaddimah, 7)

### **Mtume ﷺ Na Wanyama**


Kila tabia ya Mtume wa rehma ﷺ ilikuwa ikisimama kwenye msingi wa huruma na upendo. Alikurubiana na viumbe wote kwa huruma na kuwa na hima ya kutatua shida zao. Wanyama nao walipokea fungu lao katika bahari hii pana ya huruma. Katika enzi za ujahilia watu hawakuwa na huruma hata kidogo kwa kuwatendea ukatili wanyama. Walikuwa wakikata nyama za kula kutoka kwenye wanyama wao wakiwa haina kuandaa mashindano ya kuwapambanisha wanyama. Mtume ﷺ alikomesha matendo hayo ya kikatili.



Maelezo yafuatayo yametolewa na Abu Waqid :


“watu wa Madina walikuwa wakikata nundu za ngamia na kukata miguu ya kondoo wakiwa hai kwa ajili ya kula. Mtume ﷺ akakataza jambo hilo na kusema: “Kile chenye kukatwa katika mnyama akiwa hai ni mzoga na hivyo haufai kuliwa” (Tirmidhi, Sayd, 12/1480)

Siku moja Mtume ﷺ alimuona punda ambaye uso wake ulikuwa umetiwa alama. Alihuzunishwa sana akasema: “laana ya Allah iwe juu ya yule aliyefanya hivyo!” (Bukhari, Dhabaih, 25)





Kundi moja lililosababisha kwani kwa ndege kwa kuchukua vifaranga vyake, lilikumbana na onyo kutoka kwa Mtukufu Mtume  “yeyote aliyechukua vifaranga vya huyu ndege, mrudishieni viranga vyake; (Abu Dawud, Adab, 164 – 164/5268)

Siku moja Mtume  akiwa na maswahaba alitoka Madina kwenda Makka kwa ajili ya Ihram. Alipofika eneo liitwalo usayah, alimuona paa amejikunja na kulala chini ya mti. Mtume  alimuamuru sahaba mmoja kumlinda paa huyo na kuhakikisha kuwa hakuna mtu atakayefanya jamba lolote la kumtisha mnyama huyo. (Muwatta, Haji, Nasai, Haji,78)

Siku nyingine, akiongoza jeshi kubwa la askari elfu kumi kwenda kuifungua Makkah, Mtume  akiwa njiani alimuona mbwa akinyonyesha vitoto vyake. Haraka sana alimuita Juayl ibn suraqa akamuamuru kuwalinda hao mbwa, akaliagiza jeshi kutofanya jambo lolote linaloweza kusababisha dhiki na hofu kwa mbwa na wanaye. (Waqidi,II, 804)

Siku moja alimuona ngamia amekonda kutokana na kutopata chakula cha kutosha, akasema:

“Muogopeni Allah katika hawa wanyama wasiozungumza. Wapandeni wakiwa na afya njema na watumieni kwa chakula wakiwa na afya njema” (Abu Dawud, Jihad, 4412548)

Siku moja akiwa katika bustani ya ansari mmoja alimuona ngamia. Ngamia huyo alipomuona Mtume  alianza kutiririsha machozi. Mtume  alimsogelea na akaanza kumpapasa nyuma ya masikio ambapo ngamia huyo akanyamaza. Mtume akauliza “huyu ngamia ni wa nani?”



Akatokea kijana mmoja katika Ansari akasema “Ni ngamia wangu”

Mtume ﷺ akauliza

“je humuogopi Allah kwa huyu mnyama ambaye amekujaalia kummiliki? Hakika analalamika kwamba unamuacha na njaa na kumfanyisha kazi nyingi zaidi ya uwezo wake? (Abu Dawud, Jihad, 44/2549)

Katika tukio lingine, Mtume ﷺ alikutana na kundi la watu wakizunguma na kupiga soga wakiwa wamekaa juu ya wanyama wao. Akawashauri akisema:

“Wapandeni wanyama wenu kwa uangalifu, bila kuwachosha na wapumzisheni mnapokuwa hamuwatumii. Msiwatumie kama viti mkifanya mazungumzo myafanyayo mitaani. Huwenda mnyama akawa bora kuliko yule aliyempanda na kumtaja Mwenyezi mungu sana kuliko yeye” (Ahmad, III, 439)


Siku nyingine Mtume ﷺ alimuona mtu akitaka kuchinja. Mtu huyo, baada ya kumlaza kondoo wake ardhini alianza kunoa kisu chake mbele ya macho ya mnyama huyo. Mtume ﷺ akamzindua kuhusu kitendo hicho kisichokuwa na huruma, akamwambia; “je wataka kumuua zaidi ya mara moja? Kwa nini hukunoa kisu chako kabla ya kumlaza kondoo ardhini? (Hakim, 4, 257,260)

Mara nyingine aliwaambia maswahaba: “Je nikwambieni aliy mbali na moto na moto uko mbali naye?”



Wakasema: ndiyo ewe Mtume wa Allah.


Akasema: “kila aliye mpole, laini wa moyo, mwenye huruma, mwenye urafiki na upendo...” (Ahmad, I, 415)



Mtume  anabainisha tofauti ya watu wenye huruma na wale wasiokuwa na huruma katika maelezo yafuatayo: “Mwanamke mmoja mwenye dhambi alimuona mbwa katika janwa akiramba udongo kutokana na kiu. Mwanamke huyo alihuzunishwa sana na hali ya huyo mbwa, akatumia kiatu chake kuchota maji katika kisima kilichokuwa jirani akaikata kiu ya mbwa huyo. Hivyo Allah akamsamehe dhambi zake.

Mwanamke mwingine mzembe, alimuacha paka wake katika njaa; alimzuia hata kujisaidia kwa kumruhusu angalau kukamata wadudu ili kuondosha njaa. Hitimaye paka huyo alifariki kwa njaa, na mwanamke huyo akaingia motoni kwa ukatili wake”.<sup>35</sup>

Kwa vipimo hivi, Mtume  aliibadilisha jamii ya kijahilia kuwa jamii bora na zama zake kuwa zama neema, Asrus – Saadah. Watu ambao hapo awali walikuwa wakiwazika watoto wao wakike wakiwa hai wakabadilika na kujaza huruma ambayo ilivuka mpaka kwa wanyama. Kwa sababu Mtume  ambaye alikuwa kiigizo chema kwao, alikuwa akichunga haki ya kila kitu hata kama kitakuwa kidogo sawa na ndege. Aliweza kuwajaza hisia ya upendo na ulaini wa moyo ambao ni vigumu kuelezea.

Hata wanyama hatari kama vile nyoka na nge, wakati fulani mtu akitaka kuwaua kwa ajili ya kujilinda, Mtume  alielekeza wauliwe katika namna isiyosababisha mateso makubwa kwao:

“Mwenye kuua nyoka kwa pigo moja atapata mawili anathawabu za chini ya hiyo, na chini zaidi ni kwa yule atakaye





muua kwa mapigo mengi” (Muslim, Salam, 147; Abu Dawud, Adab, 162 – 163/5263, sayd, 14/1482)

Kwa hakika hii ni huruma ya hali ya juu inahusu hata kuua wanyama hatari.

Mtukufu Mtume ﷺ hakuwa akijisikia sifa na fakhari wakati wowote ule kwa yeye kuwa na maadili haya ya hali ya juu na kwa yeye kuwa mja wa Mwenyezi Muungu, lakini humalizia kwa kusema kwa unyenyekevu mkubwa “la fakhari – sio fakhari”. (Tirmidhi, Manaqib, I, Ibn Majah, Zuhd, 37; Ahmad, 1,5,281)

Fakhari na sifa huleta majivuno na ujivi na hatimaye kuwasha moto wa kiburi cha wanadam. Licha ya kuwa mbora wa watu wote na kusifiwa na Mwenyezi Mungu, Mtume ﷺ siku zote aliwaambia wafuasi wake wamuite:

“Mja wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake” (Bukhari, Anbiya, 48; Ahmad, I, 23).

Binadam wanahali ya kujihisi utumwa. Mtu huwa mtumwa wa mali na vitu anavyovimiliki, au atakuwa mtumwa wa mola humlinda mtu dhidi ya kuwa mtumwa wa nafsi na mali.

Uwiano ulioasisiwa na Mtukufu Mtume ﷺ baina ya pande mbali mbali za maisha hauonyeshi upungufu au dosari hata kidogo. Haiwezekani kupata mfano mwingine wenye tabia na sifa hiyo katika historia yote ya binadam.

Katika maisha tunaweza kuona watu waliokuwa mashujaa wengi ustadi na umahiri katika baadhi ya mambo. Lakini Mtume ﷺ ni mfano pekee na wa kwanza wa sifa na ubora wote kukusanyika ndani ya mtu mmoja. Kwa ufupi; yeye ndiye



mtu pekee katika historia yote, katika vipengele vyote, aliye-wapa binadam wote mambo mazuri yasiyo kifani, kimwili na kiroho, mambo mema yasiyoweza kufikiwa na yoyote katika unyenyekevu, ibada, maingiliano ya kijamii na maadili mema.

Kwa hiyo, Mtume ﷺ alikuwa kiongozi wa furaha ya milele aliyetambua kwa kina jukumu zito la kuwa kiigizo kwa ummah wake...

Ni muhimu kueleza kuwa Mtukufu Mtume ﷺ alikuwa akiipa swala Umuhimu maalum kupita kila kitu. Usiku alikuwa akilala kidogo, na nyakati nyingi mwili wake mtukufu ulikuwa haupati ladha ya kitanda. Wakati watu wakiwa wamezamaaa katika raha ya usingizi, macho yake yalikuwa ni mwenye kusujudu. Hata muda mfupi kabla ya kifo chake wakati maradhi yake yaliposhtadi, alikuwa akitoka chumbani kwake kwenda msikitini kuswali swala ya jamaa kila alipopata nguvu ya kufanya hivyo.

Abdullah ibn shikhkir ؓ anaeleza kuhusu unyenyekevu na umakini wa Mtume ﷺ katika swala kama ifuatavyo:

“Siku moja nilimkaribia Mtume ﷺ. Alikuwa akiswali, na kutokana na kilio chake ilikuwa kama kuna jungu linachemka kifuani mwake” (Abu Dawud, salat, 156 – 1571/ Q04; Nasai, Sahw,18)

Ukiacha mwezi Mtukufu wa Ramadhan, hakuna mwezi ambao Mtume ﷺ alionekana bila kufunga.

Bibi Aisha ؓ anasema:

“Mtume ﷺ alikuwa akifunga mpaka tunadhani kuwa hatofunga” (Bukhari, Sawm, 53)



Daima alikuwa akifunga siku kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano za kila mwezi, siku sita za shawwal na funga ya Ashura katika tarehe kumi ya mwezi wa Muharram. Vile vile, ilikuwa ni ada kwake kufunga siku za Jumatatu na Alhamisi ya kila wiki.

Ingawa aliwahimiza Waislam kutoa zaka na sadaka, ili-poteremka aya ya zake, Mtume ﷺ alikuwa akiitekeleza kwa kutoa kiwango kikubwa cha sadaka na misaada. Aliishi katika kiwango cha juu cha sifa inayoelezwa na Mwenyezi Mungu pale anaposema:

“...Ambao huyaamini ya ghaibu na hushika sala, na hutoa katika tuliyowapa” (Al, Baqara, 3)

Alikuwa akitoa sifa kwa mali zinazotolewa katika mambo ya kheri, pamoja na kuwasifu wafanyabiashara wanaomcha Mungu na kutoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu.

### **Viwango Vya Juu Kama Nyota**

Mtukufu Mtume ﷺ hakulimbikiza kitu chochote cha kudunia, na badala yake kila kilichokuwa kikimfikia alikuwa akikitoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Abu Dharr  anaelezea yafuatayo:

“Nilikuwa nikitembea pamoja na Mtume ﷺ nje ya mji wa Madina katika eneo lililokuwa na mawe. Kwa mbali mlima wa Uhud ulionekana. Mtume ﷺ akasema: “Ewe Abudharr!”

Nikajibu: Labbeika, ewe Mtume wa Allah”



Akasema: “kuwa na dhahabu nyingi kama mlima uhud kusingenifurahisha tofauti na kitu ambacho nigeikiweka kwa ajili ya kulipia madeni yangu, nisingekaa na mali hizo zaidi ya siku tatu” (Muslim, Zakat, 32; Bukhari, Istiqrad, 3)

Wakati fulani alikuwa akifunga siku mbili au tatu mfululizo, bila kufungua, na maswahaba wanapotaka kufunga kama yeye alikuwa akiwatahadharisha kwa kusema: “hamuwezi kuistahmilia” akawakataza kujaribu kufanya kama yeye. (Bukhari, Sawm, 48)

Hivyo ni lazima tuweke wazi jambo moja, nalo ni kuwa; kama ambavyo tunatakiwa kujua kwamba Mtume ni muongozo na kiigizo chetu kikuu, ndivyo ambavyo tunatakiwa kuvielewa viwango vya kumuiga, kwa sababu tabia na matendo yake yamegawanyika katika sehemu mbili.

1. Yale yanayomhusu yeye tu.
2. Yale yanayowahusu watu wote.

Kwa mfano huu hatuwajibiki kumuiga Mtume 🌿 katika matendo yanayomhusu yeye tu; Kwa sababu matendo hayo ya hali ya juu ni ya viwango vya juu kama nyota ambavyo hatuna uwezo wa kuvifikia na kuvitekeleza. Ama matendo na tabia zilizopo katika fungu la pili kila mmoja anaweza kuyaiga na kuyafuata kulingana na utayari, juhudi na uwezo.

Ingawa hakuna yeyote awezaye kufikia kiwango cha Mtume 🌿, lakini anaweza kuwa “Muhammad” mdogo katika ulimwengu wake mwenyewe. Kwa mfano, Waturuki waliwapa jina la “Mehmetcik”, yaani Muhammad mdogo, kwa



wanajeshi wao waliopambana kutetea ardhi za Waislam. Walifanya hivyo kwa kuzingatia ukweli huu.

Hatutakiwi kusahau kwamba tunaweza kukielewa kiwango cha mali tunayotakiwa kuitoa katika kutekeleza ibada ya Zaka. Lakini hatuwezi kujua kwa usahihi kiwango tunachowajibika kukitoa kwa ajili ya fursa na vipawa vingine vyote tulivyobarikiwa na Allah Mtukufu, ambazo ndio sababu ya sisi kutakiwa kuishi maisha ya kuwa watumwa wa Mungu mpaka siku yetu ya mwisho.

Katika jambo hili kipimo bora cha kujipima ni Ansari na Muhajirina; ambao walilelewa na kufundwa na Mtukufu Mtume ﷺ. Maswahaba hawa katika kulipa shukranikwa neema walizojaaliwa walisafiri kwenda mpaka Asia ya kati na China ili kufikisha ujumbe. Hawakuonyesha aina yoyote ya mchoko katika hamasi yao ya kueneza dini na imani hiyo.







---

# *Sehemu Ya Tatu*

---



- ✿ Usafi Wa Moyo Katika Kumfuata  
Mtume Wa Allah ۞
- ✿ Kumfuata Mtume ۞ Kwa Kumpenda
- ✿ Kioo Cha Upendo Na Maadili Yake:  
Asr'us – Saadali
- ✿ Tungo Zenye Mguso Katika Kumpenda Mtume ۞
- ✿ Salawat'us – Sharifah





## Usafi Wa Moyo Katika Kumfuata Mtume ﷺ

Maswahaba walifaidika sana na Mtume ﷺ na kumchukulia kwa namna ya dhati kabisa kuwa ni kiigizo chema kwao. Ili sisi tufikie tabia bora za maswahaba tunatakiwa kwanza kuzirekebisha nyoyo zetu. Aya Tukufu inasema dhahiri na wazi:

“Hakika mnayoruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anayemtaraji Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana” (Al-Ahzab, 21)

Kama aya inavyoweka wazi, “kumtaraji Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho” na “kumkumbuka Mwenyezi Mungu sana”, mambo haya mawili yanaunda hatua muhimu inayotakiwa ili kupata mwazo (kiigizo) njema ya Mtume ﷺ. tofauti na matendo ya ibada yanayotekelezwa katika nyakati maalum, kulinda imani ni jambo linalotakiwa kufanyika muda wote. Muda wote ni wakati wa kulipa thamani ya kumuamini Mwenyezi Mungu na kutaka radhi zake. Kwa hivyo, katika jambo hili, ni sharti muumini awe katika hali ya kumdhukuru Mwenyezi Mungu muda wote (dhikrud – Daim) ili kwamba moyo wake usidhoofike na aweze kupambana kikamilifu na wasiwasi wa shetani na nafsi, na zaidi ya yote asimsahau Mwenyezi Mungu hata kidogo.



Katika kitabu kitukufu, Allah anasema: “Enyi mlioamini! Mdhukuruni Mwenyezi Mungu kwa wingi wa kumdhukuru”<sup>36</sup>

Lakini kwa kuwa ayah ii haijaweka kikomo cha idadi inayotakiwa kufanya dhikr, hivyo amri hii itakuwa inaashiria kuwa dhikri hiyo inatakiwa kufanyika kwa kiwango kikubwa kinachowezekana,<sup>37</sup> Hivyo, muumini anatakiwa kumdhukuru Allah wakati wote na mahali pote kwa kiwango cha juu cha uwezo wake. Katika aya nyingine, Allah anasema; “Na wanasema wale waliokufuru: kwa nini hakuteremshiwa Muujiza kutoka kwa Mola wake? Sema: Hakika Mwenyezi Mungu humpoteza ambaye anataka na humuongoza anayetaka kujeja kwake. Wale walioamini na zikafulia nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu, sikilizeni! Kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu, nyoyo hutulia” (ar – Rad, 27-28)

Kumdhukuru Mwenyezi Mungu sio tu kurudia rudia neno “Allah”, bali yatakiwa kulithubutisha neno hilo ndani ya moyo ambao ni kituo cha hisia za kiroho na mwanadam ahisi ladha na utamu wa kumdhukuru Allah ndani ya moyo wake. Kuingiza hali ya kumdhukuru Allah katika moyo huondosha maradhi, huusafisha moyo dhidi ya uchafu na ususuavu, hujaza nuru na kuupatia ulaini na hisia za kiroho, na humfanya muumini huyo awe mwenye kiu ya kuvumbua siri mbalimbali za Mwenyezi Mungu. Pindi mapigo ya moyo yanapopatanishwa na Allah, nia na matendo hupata kuinuliwa kwa daraja,

36. Al – Ahzab, 41, Tazama pia, al – Jum’ah, 10.

37. Amri isiyotaja kiwango na kikomo husika, hukusudia jambo husika lifanyike kwa kiwango kikubwa kinachowezekana.



thamani na cheo. Mtume ﷺ anasema: “Alama ya kumpenda Mwenyezi Mungu ni kupenda kumdhukuru” (Suyuti, II, 52)

Wapenzi kamwe hawawasahau wale wanaowapenda, hawaachi kuwataja na nyoyo zao haziachi kuwafikiria.

Kwa hakika watu wenye dhamira ya kupata utamu wa imani hudumisha kumdhukuru Mungu katikati ya vina vya nyoyo zao. Wakiwa wamesimama, wakiwa wamekaa au wakiwa wamelala, huzama katika taamuli na tafakuri nzito nay a kina kuhusu hekima za ndani na za siri zinazopatikana katika umbaji wa mbingu na ardhi, na husema kwa heshima na unyenyekevu: “Mola wetu! Hukuviumba hivi bure, utukufu ni wako, basi tuepushe na adhabu ya moto!” (Ali Im ran: 191)

Ama nyoyo ambazo hazijapata ulaini huu na kuwa na sifa hizo, bila shaka hazina dhamira ya kuelekea kwa Allah. Aya ifuatayo inaelezea hali zao; “Basi adhabu kali kwa wale wenye nyoyo ngumu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu, hao wamo katika upotovu dhahiri” (Zumar : 22)

Mtu yeyote anayejitenga mbali dhidi ya kumdhukuru Allah, kama isimavyo ayah ii, hukosa hisia na sifa yake ya ubinadam.

Kwa hivyo, ili mtu aweze kumfuata Mtume ﷺ na kufaidika naye kama inavyotakiwa, lazima moyo wake ujae mapendo ya kumpenda Mungu, ajiepushe na matamania ya nafsi na starehe za dunia, ajipambe kwa sifa ya kumdhukuru Allah sana pamoja na kutaraji kukutana naye na kutaraji siku ya mwisho.



### **Kumfuata Mtume Kwa Kumpenda**

Matunda ya kweli ya kumpenda mtume ni kuifuata kwa dhati njia yake, kuridhika naye na kujisalimisha kwake kwa moyo mmoja.

Mtukufu Mtume katika vipengele vyote ni rehma halisi nay a milele kwa wanadam. Aya ifuatayo imeelezea namna moyo wake ulivyojaa rehma na huruma kubwa sana kwa waumini: “Bila shaka amekufikieni Mtume kutoka miongoni mwenu, yanamhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangai-kieni, kwa waumini ni mpole, Mwenye kurehemu” (at-Tawba: 128)

Hadithi ifuatayo inaonyesha huruma aliyokuwa nayo kwa ummali yake:

“Enyi waumini! Allah akuwekeni salama! Allah akuangalieni, akulindeni dhidi ya ubaua na akusaidieni! Allah akuinueni na akuongozeni! Allah akunusuruni! Allah akuondosheni katika kila aina ya taabu na akulindieni dini yenu!”<sup>38</sup>

Mtume alikuwa njia, muongozo na rehma iliyowaenea watu wote kwa matendo, kauli na maisha yake ya kimaadili. katika njia ya mahubiri yake alikabilia na shida, dhiki na tabu kubwa mno. Katika subira na hamasa yake alifikia hatua ambayo wakati fulani aliweka nafsi yake katika hatari ili kwamba ummah wake upate muongozo na rehma. Mpaka Mwenyezi Mungu akamhadharisha asiangamize nafsi yake katika kazi yake ya da’wah. Anasema katika Qur’an Tukufu;



“Basi huenda utajiangamiza nafsi yako kwa kusikitikia hali yao ikiwa hawayaamini mazungumzo haya!” (Al-kah: 6)

“Huenda utaangamiza nafsi yako kwa sababu hawawi waumini” (as – Shuara: 3)

Aya hizi tukufu zinaonyesha raghabu aliyokuwa nayo Mtume ﷺ ya kutaka kila mtu anayeishi katika hii dunia amuamini Mwenyezi Mungu, na kutaka kuwaokoa dhidi ya adhabu ya jahannam kwa kuwa hurumia watu wa ummah wake.

Ama kuhusu huruma na mapenzi makubwa ambayo Mtume ﷺ alikuwa akiyaonyesha kwa ummah wake, tunatakiwa sisi kama ummah tutafakari kile tunachotakiwa kumpa kwa upendo huo. Kipimo cha mapenzi yetu kwa Mtume ﷺ kitaonekana kwa sisi kuifuata Qur’an na kufuata mwenendo wake, na hali yetu kuwa kama yake.

Maswahaba waliompenda na kutoa kila kitu chao kwa ajili yake, walikuwa wakimtambua vipi na ni ipi hisia yao kwake? Walizibadili vipi hali na tabia zao kuwa kama zake? Sisi tuko wapi na tabia hizi? Tunatakiwa kuyapima mapenzi yetu kwake kwa vipimo hivi, na tuzipime nyoyo zetu kwa maadili na tabia zake. Tunatakiwa kuzitakasa nafsi zetu dhidi ya dhambi, makosa na mapungufu yetu kwa kuziosha katika chemchem safi ya tabia zake, bahari ya hekima na maarifa, ambayo kutoka humo tunapaswa kupata maji ya uhai kwa ajili ya kuzihuisha roho zetu.

Siri inayoweza kutufikisha kwa Allah inapatikana katika kujikuruhisha kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna tukufu za Mtume wake kwa moyo salama na safi. Vile vile siri




inapatikana katika kupenda kile kinachopendwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kuchukia kile wanachokichukia.

Kupenda kile kinachopendwa na Mungu huhuisha nyoyo, huzipa afya na kuzifanya zisimame kwenye kheri muda wote. Upendo na kinyume chake haviwezi kuwa pamoja katika moyo moja kwa wakati mmoja. Pindi moyo unapoipukana na kimoja wapo hujawa na kingine na tofauti kati ya vitu hivi viwili ni kama umbali kati ya ala'ul-illiyyin, (juu ya waliojuu), na asfal'us-safilin, (chini ya waliochini). Mshairi kanal Adib Kurkuoglu anatanabahisha na kuonya waumini wanaopuza upendo kwa Mtume na sunnah zake:

“Kutupwa mbali na upendo wake, kunatosha kuwaangamiza wanaompua katika maisha ya sasa nay a akhera ...”

Tunamuomba mola wetu atufanye kuwa umma unaompenda kwa dhati...

Akiwa amepigwa mawe na watu hao hao ambao alikuwa akihangaika kuwaokoa, ajabu ni kwamba aliendelea kuwaombea kheri. Jambo hili lilimshangaza sana Zayd ibi Harithah ambaye hakuficha mshangao wake kwa kusema:

“Ewe Mtume wa Allah, wakati wamekupa mateso na misukosuko mikali bado unawaombea?” Mtume  aliendelea kusema;

“Wanitaka nifanye nini? Hakika nilitumwa kuwa rehma na sio kuwa katili!”

Je hilo pekee halitoshi kuonyesha kiwango cha juu cha wema na kufikiwa na mtu yeyote?



Kupitia utume wa Nabii Muhammad ﷺ binadam waliunganishwa kwa nuru ya muongozo wake uliokamili. Hivyo yule atakayeendelea kuishi katika ubinafsi baada ya kuiona ruwaza njema ya Mtume ﷺ anawajibika sana kwa kosa lake hilo kuliko wale walioishi maisha ya kijahilia kabla ya kaja kwa Mtume ﷺ

Binadam katika zama zetu hizi anaishi kwa kushikamana na ubabe unaompelekea kwenye ubinafsi, kwa hiyo anahitajia sana kujenga shakhsia kama ya Mtume ﷺ.

Bila shaka msukumo mkubwa uliopatikana katika zama tukufu za historia yetu ni kuwepo kwa waumini, watu wenye matendo mema ambao walikuwa warithi wa kweli wa Mtume Mtukufu ﷺ, ambao pia waliipa jamii tabia zao njema katika uhalisia wake. Kinyume chake, kwa masikitiko makubwa tunashuhudia mambo yanayovunja moyo katika hizi, yaani kushuka kwa kiwango cha maadili, kutokana na ukosefu wa idadi ya kutosha ya watu kama hao wanaoweza kuchukuliwa kama mfano na kiigizo chema.

Ili kwa mara nyingine tufikie kiwango cha maadili ya kiroho cha Mtume ﷺ na wale waliofuata njia yake, na zaidi, mashujaa wa imani waliokuwa wamejaa katika historia yetu, lazima tupate watu kama hao ambao ni kiigizo na mfano mwema.

Kwa ajili hiyo, tunatakiwa kuwasika, tuzijue njia zao na hivyo tuweze nasi kupata sehemu ya utajiri wao wa kiroho. Yaani, lazima tujue namna walivyoamiliana na dunia hii ya mpito na kufungua njia ya furaha, kwa ajili yao na kwa binadam wote, kwa namna walivyotumia maarifa yao, maisha yao, uhai wao na nyenzo mbalimbali walizojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.



### **Kioo Cha Upendo Na Maadili Yake: Asrus-Saadah**

Athari ya ndani na tabia za nje zilizotolewa na Mtume 🌿 zilikuwa kama kitovu kilichoibadilisha jamii ya kijahilia ambayo hapo kabla ilikuwa imezama katika unyama na ujinga wa kutojua hata misingi ya wao kuwa binadam, akaifikisha kwenye kiwango ambacho haiwezekani hata kukiota, jamii ambayo inahusudiwa na binadam mpaka leo, jamii hiyo ni Maswahaba. Waliunganisha chini ya dini, bendera, sheria na utamaduni mmoja, chini ya bendera ya serikali na ustaarabu wa pamoja.

Maeleze hayo yaliwabadilisha watu hawa wajinga kuwa watu wenye ustaarabu. Akawatoa kwenye ukatili na unyama akawafanya kuwa watu wenye maendeleo na wema, kama ambavyo aliwabadilisha watu waovu kuwa wachamungu wanaoishi kwa kumpenda na kumuogopa Mwenyezi Mungu.

Jamii hiyo ya kijahilia ambayo kwa karne nyingi haikuweza kutengeneza mtu hata mmoja mwenye umuhim na hadhi ya kiroho – ilishuhudia kuibuka kwa idadi kubwa sana ya watu wenye sifa kuu waliolelewa chini ya malezi ya kiroho ya Mtume 🌿.

Watu hawa ambao walikuwa kama miale ya maarifa na elim, waliibeba imani na mvuto ndani ya nyoyo zao na kuipeleka katika pembe nne za dunia. Kwa hakika nuru iliyoteremka jangwani na kudumu chini ya kivuli chake, ilieneza na kutawanya haki, uadilifu na uongofu kwa watu wote. Siri ya law'laka law'laka<sup>39</sup> ikadhihiri, na sababu ya kuumbwa kwa ulimwengu ikatimia.

39. Tazama hadithi inayoelezea ukweli huu; "lau kama si kwa ajili yako nisingeumba ulimwengu" hakini, II, 672/4228.





Hawa maswahaba waliolelewa na Mtume ﷺ walitengenezajamii yenye maarifa ya kweli. Zama za elimu na tafakuri ua kina, na zama za kumjua Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa ukaribu. Waliifanya tawhid kuwa kitovu cha fikra na mawazo yao wakafanikiwa kuyaondosha mapenzi ya manufaa ya kidunia ndani ya nyoyo zao. Walionja utamu wa imani. Mali na uhai vikawa nyezo badala ya kuwa lengo. Waliipanua huruma yao na ikawa msingi wao mkuu wa maisha ni kuwatumikia na kuwahudumia watu wengine. Kiwango kikubwa sana cha kujitolea kilitumika kwa ajili ya lengo hili. Vile vile wametupatia kielelezo cha tabia ya kiislam. Inaelezwa kuwa ili tu kusikia hadithi ya Mtume ﷺ, swahaba angesafiri umbali wa mwezi mmoja kwenda kutafuta hadithi moja na angerudi bila kuipata. Kitendo cha kumuona mpokezi wa hadithi husika akimdanganya farasi wake kingemtosha swahaba hiyo kutoichukua hadithi.

Sasa, kitu gani walichopata maswahaba kutoka kwa Mtume ﷺ?

1. In-qas: Kuifanya hali yao kuwa sawa na hali ya Mtume ﷺ.

2. Kupata Aqrabyyah: kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu na kumtambua kwa moyo.

Kwa mambo hayo mawili kheri na haki vilijidhihirisha kwa uzuri wake wote ndani ya nyoyo zao, na shari na batili ukaonekana ubaya wake wote. Maana mpya ya kumfahamu Mwenyezi Mungu, ulimwengu na nafsi ikadhihiri kwao. Lengo lao ikawa ni kuivaa hali ya Mtume ﷺ kama jua linavyoakisi mwanga wake kwenye kioo kidogo.



Mipaka ya dola ndogo ya kiislam mjini Madina, iliyokuwa na familia mia nne, katika kipindi cha miaka kumi ilifika Iraq na palestina wakati wa kifo cha Mtume ﷺ dola hiyo ilikuwa katika mapambano na madola makubwa ya warumi na waa-jemi. Lakini Maswahaba hawakubali mkondo wa maisha yao ikilinganishwa na miaka kumi ya kabla waliendelea na maisha yao ya unyoofu na ibada ingawa viwango vya maisha vilikuwa vimebadilika.

Utumiaji kupita kiasi, ulafi, anasa na ufahari havikuwa na nafasi katika maisha yao. Walikuwa wakitambua kwamba” mafikio ya nafsi hii kesho ni kaburi”. Hivyo siku zote walikuwa wakiepuka kujilimbikizia mali za dunia na kuzama ndani yake kupita kiasi. Badala yake walizitumia neema hizo kama nyezo ya kuwaongoza na kuwaokoa wanadam kuelekea kwenye imani.

Bila shaka miongoni mwa sababu kuu za kuenea Uislam kwa kasi, kama mwanga wa asubuhi, miongoni mwa jamii zilizodhulumiwa ni kwamba Maswahaba walionyesha tabia na sifa kamili ya Mwislam kila mahali walipofika. Wanafunzi watukufu wa Mtume ﷺ, Maswahaba walikuwa waumini wa kipekee, wakweli na waadilifu, wakibeba wema katika nyoyo zao zilizong’arishwa na nuru ya Utume, wakawatazama waja wenzao wa Mwenyezi Mungu kwa jicho la huruma.

Walimuweka Mungu na Mtume wake katikati ya kitovu cha urafiki ambao uliinua jamii isiyojua kusoma wala kuandika na kuifikisha kwenye kilele cha ustaarabu. Nyoyo zao kusi-simka zikiwaza “Allah anataka nini kutoka kwetu? Na Allah na Mtume wake wangependa kutuona tukiwa katika hali gani?”



Walizitengeneza vizuri zama na wakaukirimu ubinadam kwa zama za furaha.

Waumini hawa waliwekwa huru dhidi ya shari ya nafsul-ammara (nafsi inayoamrisha maovu), wakawa waumini ambao muda wote walikuwa ni wenye kujiuliza, kufanya uhakiki, wakainuka kutoka kwenye unyama wakawa kama malaika.

Mtaalam wa mifumo ya sheria ya kiislam, Qarafi (aliyefariki 684 Hijriya) anasema:

“Lau kama Mtume ﷺ asingekuwa na muujiza mwingine, maswahaba wanyoofu aliowalea wangetosha kuthibitisha utume wake”

Walikuwa mfano hai wa muujiza wa Qur’an, wakafika kwenye kilele cha werevu, ushindani na tunu zote za kibinadam.

Katika zama hizo akili na moyo, ambavyo humpatia muumini ukamilifu, walivitumia vyote kwa pamoja kwa uelewano wa hali ya juu. Tafakari ya kina iliyochanganyika na hisia, hamasa na roho iliongezeka sana. Watu waliishi na uhakika wa kwamba hii dunia ni nyumba ya majaribu na mitihani. Nyoyo zao zikawa ni zenye kuutambua ukuu, uwezo wa Mungu. Safari za maeneo ya mbali kama Samarkand na China, kwa ajili ya kuamrisha mema na kukataza mabaya ikawa jambo la kawaida mno, zikifuatiwa na safari za baadaye za kwenda Andalusia (Hispania). Jamii hiyo ya kijahilia ikabadilika kuwa jamii yenye maarifa ya kweli. Kwaosiku ukawa mchana na majira ya kipupwe yakawa majira ya








kuchipua. Tafakuri yao ikapiga hatua ya juu, wakaanza kuta-fakari kwa kina kila kinachowazunguka. Walitafakari kwa kina namna binadam alivyoumbwa kutokana na tone la maji, ndege walivyoumbwa kutokana na mayai madogo madogo, miti na mtunda ilivyoumbwa kutokana na mbegu zisizokuwa na thamani, na maajabu mengine mengi. Waliyapangilia na kuyaelekeza maisha yao juu ya kumridhisha muumba. Hisia za huruma na huvuma na upendo zilifikia kilele cha hali ya juu cha kueneza ukweli na kuutekeleza.

Kwao, nyakati za furaha na raha ni zile ambazo walizo-kuwa wakizitumia katika kufikisha ujumbe wa tawhid kwa watu wote. Ajabu ni pale swahaba ambaye alikuwa amebaki na dakika tatu kabla ya kuuawa, akamshukuru yule aliyempa-tia muda huo akimwambia: "...hiyo ina maana kwamba nina dakika tatu nyingine za kuamrisha mema"

Kwa ufupi, Maswahaba waliishi kwa pamoja na Qur'an, wakayatoa hiki kitukufu, wakionyesha hamasa na moyo wa kujitoa ambao haukuwahi kushuhudiwa katika historia yote. Pamoja na kwamba waliteswa, wakandamizwa na kuonewa, lakini kamwe hawakuiacha hata kidogo misingi ya imani yao. Waliacha mali, nyumba na kila kitu wakahama ili kuziweka katika maisha yao aya zilizoteremshwa na Mwenyezi Mungu. Ili kufikia jambo hilo walikitoa muhanga kila walichokuwa nacho.

Mara zote walikuwa na raghba na hamasa ya kujif-unza Qur'an na maisha kwa kila aya iliyomo ndani yake. Hawakuiacha hata katika nyakati za hatari. Mfno wa hilo ni huu ufuatao:



Abbad  aliyekuwa amepewa jukumu na Mtume  la kuwa mlinzi, alimpa mwenzake Ammar  taarifa ya kushambuliwa baada tu ya kuwa ameshapigwa mishale miwili au mitatu. Ammar akashtuka huku akishikwa na mshangao, akamuliza mwenzake huyo kwanini hakumpa taarifa baada ya mshale wa kwanza. Abbad  akajibu: “Nilikuwa nikisoma surah ya Qur’an na sikutaka kukatisha swala yangu kabla ya kumaliza kuisoma. Lakini mishale iliponipiga mmoja baada ya mwingine niliacha kusoma nikaenda kurukuu. Lakini naapa kwa Allah, lau kama si hofu ya kupoteza ulinzi wa eneo hili nililokabidhiwa na Mtume , ningependelea kifo kuliko kukatisha kisomo cha sura hiyo.” (Abu Dawud, Taharat,78/198; Ahmad,III,344; Ibn Hisham, III, 219; Waqidi, 397)

Maswahaba waliishi maisha ambayo mhimili wake ni Qur’an. Kila wajibu wa kidini, kwao, ilikuwa kama ladha isiyokuwa na kifani. Kila aya inayoteremka ilikuwa kama karamu kutoka mbinguni. Walifanya Qur’an Tukufu na wakaifanya kuwa njia bora wanayoweza kuishi kwao.

Katika mambo yanayoonyesha mapenzi na hamasa kubwa waliyokuwa nayo juu ya Qur’an Tukufu, ni pale ambapo swahaba wa kike alikuwa radhi kufundishwa aya za Qur’an kama mahari yake.<sup>40</sup>

Walikuwa wakiamka usiku kuswali, kusoma dua na wakipendelea kusoma Qur’an kuliko kulala usingizi waraha vitandani mwao. Mtu ambaye angepita karibu na nyumba zao wakati wa giza la usiku angesikia sauti za kisomo cha Qur’an na dhikr kana kwamba ni mvumo wa nyuki. Hata

---

40. Bukhari, Nikah, 6, 32, 35; Fadhailul-Qur’an, 21, 22; Muslim, Nikah, 76.



katika mazingira magumu Mtume ﷺ angewafundisha Qur'an. Anas ﷺ anasimulia kuwa siku moja Abu Talha ﷺ alikwenda kwa Mtume ﷺ, ambaye alikuwa amesimama akiwafundisha Qur'an wanafunzi wa suffa, huku akiwa amefunga jiwe tumboni mwake kuupa nguvu mgongo wake, ambao ulikuwa umepinda kwa sababu ya njaa kali. (Abu Nuaym, Hilya, I, 342)

Raghba na hamu yao yote ilielekezwa kwenye kukifaham na kujifunza kitabu cha Allah, wakishughulishwa na kuisikiliza na kuisoma mara kwa mara.

Kutokana na kumfanya Mtume ﷺ kuwa kiigizo, hatimaye mji wa Madina ulijaa wasomi na watu waliohifadhi Qur'an yote. Hizo zilikuwa zama za furaha.

Ni hali ya ajabu mno, kwani hata kama wataalam wote wa saikolojia, elimujamii, sayansi ya uelimishaji, uhandisi na falsafa wakiungana pamoja hawawezi kutengeneza hata jamii ndogo yenye sifa bora ilizokuwa nazo jamii ya enzi hizo. Hawawezi kutengeneza angalau hata jamii inayokaribiana nayo. Hata kitabu cha farabi kitiwacho Madinatul – Faadhilah (mji bora), ambacho ni mradi unaohusu jamii ya mfano, kimebaki kama chakula katika vinywa vya mchwa.

### **Tungo Zenye Mguso Katika Kumpenda Mtume ﷺ**

Mtukufu Mtume ﷺ ni chemchem moja nay a kipekee ya huruma na upendo inayompeleka mtu kwenye bahari ya upendo wa Mungu. Kumpenda na kumtii ni kumpenda Allah Mtukufu, na kumuasi ni sawa na kumuasi Allah.



Mwenyezi Mungu anasema katika Qur'an Tukufu: "Sema: Ikiwa nyinyi mnapenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni, Mwenyezi Mungu atawapenda na atawasamehe madhambi yenu, na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa msa-maha, mwenye kurehemu" (Ali Imran, 31)

Baada tu ya kifungu cha lailaha illallah (Hakuna Mungu ila Allah) katika tamko la tawhid kinafuata kifungu cha Muhammad Rasulullah (Muhammad ni Mtume wa Allah). Kila neon la tawhid na kila neno la kumtakia rehma Mtume ni rasilimali ya kuelekea kwenye ukaribu na kumpenda Mwenyezi Mungu. Kila furaha ya dunia na akhera na kila ushindi wa kiroho unapatikana kwa rasilimali ya kumpenda. Ulimwengu ni dhahirisho la upendo wa Mungu, na nuru ya Muhammad ndio chimbuko na kiini cha dhahirisho hilo, na kumpenda Mtume ﷺ ndio njia pekee ya kuifikia dhati ya Mwenyezi Mungu.

Utulivu wa kiroho katika matendo ya ibada, madaha ambayo hutapakaa katika tabia, upole unaoyatawala maadili, ulaini katika moyo, uzuri katika muonekano, ufasaha katika lugha, uzuri unaopenya katika hisia, kuzama kwa kina katika kufikiri, na kwa ufupi mambo yote mazuri ni mng'aro tu uto-kao katika mapenzi ya Mtume na kuakisi juu ya nyoyo.

Maulana Rumi anaelezea kwa uzuri kabisa akisema: "Njoo, ee moyo, kwenye sikukuu ya kweli ambayo ni kuungana na Muhammad... kwani nuru unayoiona katika ulimwengu ni mng'aro tu unatoka katika uso wa mtu huyo aliyebarikiwa"

Ni kwa sababu hiyo kwamba njia pekee ambayo lazima kuitipita ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu na upendo wake



ni kufuata mwenendo wa Mtume ﷺ. muumini yeyote hawezi kuwa Insaanul-kamili (binadam kanili), ambalo ndio lengo la Uislam – bila kupita, kuiga na kuandamana na sunnah ya Mtukufu Mtume ﷺ, na hawezi kupata amani na furaha ya kweli ya kidini. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ameonyesha kielelezo na mfano wa “binadamu kamili” ndani ya Mtume ﷺ, akamfanya kuwa rehma kwa walimwengu na mfano kwa waumini wote.

Kwa hali hiyo utiifu huu una umuhim kiasi gani mpaka Mwenyezi Mungu aufanye kuwa sharti la kuwapenda waja wake?

Hakuna shaka kwamba hali hiyo ya juu naya ukuu inaanza kwa kumpenda Mtume ﷺ kutoka moyoni na kupata sehemu ya utajiri wake wa moyo, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Qur’an Tukufu kuhusu kumfuata Mtume ﷺ ambaye ni “kiigizo chema” kwetu! “Anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni basi jiepusheni, na mcheni Mwenyezi Mungu, kwa hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu” (Al-Hashr, 7) “Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume wala msiviharibu vitendo vyenu” (Muhammad, 33)

“Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao (watakuwa) pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu, miongoni mwa Manabii, na Masiddiki, na Mashahidi na watu wema, na hao ndio marafiki wema” (an – Nisaa, 69)

Qur’an Tukufu, ambacho ni kitabu kilichoteremshwa na Mwenyezi Mungu, kimeonyeshwa vyema kutoka katika ulimwengu wa ndani ya Mtume ﷺ. kwa hakika siri za kitabu hiki kitukufu hudhihiri na kuwa wazi pindi mtu anapofanywa





ndani ya hali ya kiroho ya Mtume wa Allah ﷺ. Iau tungepata heshima, kama maswahaba ﷺ ya kuingia katika ulimwengu huo tungeweza kufika kwenye kilele cha furaha na kushuhudia ishara za uzuri wa ki-Mungu, ishara za amri na makatazo, maarifa na hekima zilizo ndani ya siri hizo.

Kwa ufupi, Iau tungeweza kusoma maneno ya Mungu kwa ishara na dalili zilizowekwa ndani ya moyo wa Mtume ﷺ, na nyoyo zetu zingekuwa kama vipepeo zikimzunguka Mtume ﷺ kama ilivyokuwa kwa maswahaba wa zama za furaha ambao walimpenda sana Mtume ﷺ. Tungeweza pia kufahamu kila neno, kila amri na hata kila ishara ya Mtume ﷺ, na kufikia kilele na daraja ya upendo wa ndani unaopatikana katika maneno yafuatayo:

“Ee Mtume wa Allah! Baba yangu, Mama yangu, mali na roho yangu viwe fidia yako”

Uwepo wa Mtume ﷺ ni chemchem ya nuru na shamirisho la upendo kwa binadamu. Watambuzi wanajua kuwa sababu ya kuwepo kwa viumbe vyote ni kutokana na upendo wa Mungu kwa Nuru ya Muhammad ﷺ. Kwa hiyo, ulimwengu wote ni kama zawadi kwa Muhammad Mustafa ﷺ, nuru ya viumbe. Viumbe vyote vimeumbwa kwa heshima ya Nuru yake. Ni kwa sababu hiyo kwamba, Shakhisia hiyo inastahiki kuitwa na Allah kwa kusema: “Ee kipenzi changu”.<sup>41</sup>

Furaha iliyoje kwa hao waumini waliompa Mwenyezi Mungu na Mtume wake nyoyo zao na kumfuata kwa upendo. Upendo huo ambao kwao uko juu ya aina yoyote ya upendo....

---

41. Tazama: Tirmidhi, Manaqib, 1/3616; Darimi, Muqaddima, 8; Ahmad, 6,241; Haythami, 9/29.



Kuwa karibu na hakika ya Muhammad 🌸 yaweza kupatikana kwa upendo zaidi kuliko akili.

Mbingu za Rabiulawwal – zilizopata heshima ya ujio wake katika huu ulimwengu zilifunguka kama rehema na msamaha kwa waumini.

Kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, Bibi Thuwaybah alikuwa miongoni mwa wanawake waliopata bahati ya kumnyonyesha Mtume 🌸. Bibi huyu alikuwa kijakazi wa Abu lahab, Ami yake Mtume 🌸 na adui yake mkubwa.

Bibi Thuwaybah alipofikisha taarifa za uzao wa Mtu-kufu huyu kwa Abu lahab, Abu lahab aliamua kumuacha huru kijakazi huyu kutokana tu ma mapenzi ya kiukoo. (Halabi, I, 138)

Hata furaha iliyotokea kwa sababu ya mapenzi ya kiudugu yalitoshia kumpunguzia Adhabu Abu lahab kila Jumatatu jioni. Abbas anaelezea jambo hili akisema: “Mwaka mmoja baada ya kifo chake nilimuona ndugu Abu lahab katika ndoto. Alikuwa katika hali mbaya. Nikamuuliza, “Ulitendewa vipi?”. Akanambia, “kwa kumwacha huru Thuwaybah kwa kusherehekea kuzaliwa kwa Muhammad, adhabu yangu hupunguzwa kila Jumatatu. Katika siku hiyo huchangamshwa kwa chemi-chemi inayotoka kwenye kitundu kidogo kilichopo kati ya kidole gumbo na kidole cha shahada”.<sup>42</sup>


Ibn Jazari anasema:


“Kama Abu lahab, adui wa Mtume, anapunguziwa adhabu kwa sababu tu ya furaha aliyoionyesha kwa hisia za kik-





abila siku ya kuzaliwa Mtume, ni kiasi gani cha ukarimu na neema atakazo muumini kwa kuonyesha heshima kwa usiku wa kuzaliwa Mtume, akaufungua moyo wake kwa kumpenda! Basi kinachotakiwa kufanyika, katika mwezi aliozaliwa, ni kuhuisha shauku kwa kujishughulisha na mazungumzo ya kiroho, kuandaa karamu mbalimbali kwa ajili ya waumini ili wafaidike na baraka za mwezi huu, kuzifurahisha nyoyo zenye huzuni kwa kuwafanyia kila aina ya hisani yatima, maskini, wapweke, na wenye shida, kuwafurahisha kwa kuwapa sadaka, na kusoma na kusikiliza Qur'an Tukufu..."

### **Upendo Wa Maswahaba Kwa Mtume**

Maswahaba walimpenda sana Mtume , upendo ambao ni vigumu kuelezea kiwango chake. Upendo kama huu huweza kupatikana kwa mapenzi na baraka ya Mwenyezi Mungu pekee, kinyume na hivyo ni muhali kufikiwa.

Maswahaba walitengeneza pingu madhubuti ya kumtii Mtume  kama ngome ya upendeo, wakawa nyota katika anga ya utii kiasi kwamba kuna baadhi yao ambao, kwa sababu ya shauku kubwa ya kumfuata, walipita katika njia aliyopita, wakasimama mahali aliposimama na wakanusa uaridi alilonusa, kwa sababu alifanya hivyo.

Misemo ya mshabaha wa tendi za upendo waliokuwa nao maswahaba kwa Mtume  haihesabiki. Ifuatayo ni mifano tu michache ya hisia hizo:

Bibi Aisha alikuwa akiuelezea uzuri wa Mtume  kama ifuatayo:



*“Lau watu wa Misri wangeusikia uzuri wake,  
Wasingepoteza muda kubishana na Yusuf,  
Wale waliomlaumu Zulayha wangeuona uso wake,  
Wangezidata nyoyo zao badala ya mikono.”*

Mtume 🌿 kwa hakika ni “mja” na mwanadam kama anavyoeleza na tamko la Tawhid, ingawa kwa dhati yake, yeye ni “Bwana wa Mitume”

Aziz Mahmud Hidayi anaeleza kwa ufasaha uzoefu wake baada ya kuushuhudia ulimwengu wa siri hizi: “Ulimwengu huu ni kioo, kila kitu kimesimama kwa haki,

Kutoka katika kioo cha Muhammad Allah anaonekana...”

Mtukufu Mtume 🌿 ni kitovu cha siri ya mapenzi ya Mungu, ambayo huyakuza mapenzi yote ya sitiari na kuyapeleka kwenye ukuu.

Pindi muumini anapoanza kutetemeka mbele ya haiba ya kiroho ya Mtukufu Mtume 🌿 na kuhisi hisia nzuri zikichipua ndani ya moyo wake, na kuisafisha roho yake dhidi ya picha na taswira zote za maumbo ya tamaa, bila shaka huo unakuwa mwanzo wa njia ya kuchukua fungu lake litokanalo na kumpenda, kumfuata na kuungana naye. Kuhusu hilo, Mawlana Rumi 🌿 anasema: “Ulimwengu wote wa aina mbili uliumbwa kwa ajili ya moyo mmoja. Tafakari maana ya ibara isemayo,” Lau isingekuwa kwa ajili yako, nisingeumba ulimwengu”

Kwa sababu hiyo kumpenda Mtume 🌿 ni nyenzo kuu inayowapa watu heshima katika dunia na akhera. Kwa upendo huo maswahaba walipata daraja za juu zisizoweza kufikiwa na yeyote.



Ufuatao ni mfano mwingine wa upendo usio kifani waliokuwa nao Maswahaba kwa Mtume ﷺ: Wakati wakielekea katika pango la Thawr katika safari ya Hijrah, Abu Bakr ﷺ alikuwa akitembea nyuma ya Mtume ﷺ na muda mwingine akitembea mbele yake.

Mtume ﷺ alipoona hali hiyo alimuuliza Abu Bakr: “Kwa nini watembea hivyo?” Abu Bakr akasema: “Nahofia kwamba washirikina wanaweza kunikamata kutokea upande wa nyuma, ndiyo maana natembea nyuma yako. Na ninapohisi kuwa wanaweza kukamata kutokea upande wa mbele hapo nani hufanya haraka sana na kutembea mbele yako”

Ilikuwa jioni walipowasili kwenye mlango wa pango hilo. Abu Bakr ﷺ akamwambia: “Ewe Mtume wa Allah! Tafadhali subiri niondoe uchafu pangoni” Kisha aliliandaa pango, akachunguza matundu na kuyaziba moja baada ya lingine kwa kutumia vitambaa alivyokuwa akivichana kutoka kwenye nguo zake. Mpaka mwisho alikuwa ametumia nguo yake ya kujifunika katika kuziba matundu, likabaki tundu moja ambalo aliliziba kwa kutumia wayo wa mguu wake. Baada ya kazi hiyo akamwambia:

“Sasa waweza kuingia, ewe Mtume wa Allah”.

Asubuhi baada ya kumuona, Mtume ﷺ alimuuliza kwa mshangao: “Nguo yako iko wapi, ee Abu Bakr?” Abu Bakr ﷺ akamueleza alichofanya jioni ya jana. Akiwa ameguswa sana na kitendo hicho cha moyo na ukaarimu wa hali ya juu Mtume aliinua mikono yake na kumuomba.<sup>43</sup>

---

43. Tazama: Ibn Kathir, al-Bidaya, III,222 – 223; Ali al-Qaaro, Mir kaat, Beirut 1992, 10, 381 – 382; Abu Nuaym, Hilyah, I, 33.



Mfano mwingine ni ule unaoelezea mapenzi ya ajabu aliyokuwa nayo mama mmoja ambaye mume wake, baba yake na watoto wake wawili walikuwa wameuawa kishahidi katika vita vya uhud:

“Muhammad ameuawa!” zilikuwa habari mbaya zilizo-litikisa anga la mji wa Madina siku ya Uhud, kwa mayowe na kelele za woga zikifika mawinguni. Watu wote walimiminika mitaani kwa matumaini ya kupata habari kutoka kwa watu wanaoingia mjini. Ingawa Bibi Sumayra 🌿 alikuwa amepata habari za kusikitisha kwamba mumewe, watoto wake wawili na baba yake wote walikuwa wameuawa kishahidi katika madani ya vita vya Uhud, hakkuhuzunika, bali akili yake ilishughulishwa na shauku ya kutaka kujua hali ya Mtume 🌿 akawa anawauliza wale waliokuwa wakirudi kutoka vitani:

“Je yeye hajambo?”

Wakamjibu: “Alhamdulillah, yu hai na hajambo, yuko kama upendavyo” Akiwa bado na wasiwasi, akawajibu: “moyo wangu hautotulia mpaka nimuone. Nionyesheni nimuone Mtume wa Allah”

Walipomuonyesha, mwanamke huyo shupavu, Sumayra, alimkimbilia na kumwambia: “Wazazi wangu wawe fidia yako, ewe Mtume wa Allah! Madam upo hai hakuna kinachoweza kunipa wasiwasi tena” (Waqidi, I, 292; Haythami, 6, 115)

Anas ibn Malik 🌿 anasimulia kuwa:

“Mtu mmoja alikuja kwa Mtume wa Allah na kuuliza: “Kiama kitakuwa lini?”

Mtume 🌿 akamuuliza: “Kiama umekiandalia nini?”



Mtu huyo akajibu: “kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake”

Hapo Mtume ﷺ akamwambia: “Basi utakuwa pamoja na wale uwapendao”

Akiitolea maoni simulizi hii, Anas ؓ anaongeza kwa kusema:

“Baada ya kuingia katika Uislam, hatukupata kufurahi sana kama tulivyoifurahia kauli ya Mtume wa Allah “utakuwa pamoja na wale unaowapenda” Mimi binafsi pia nampenda Allah na Mtume wake, pamoja na Abu Bakr na Omar; na ingawa sijaweza kufanya jambo linalolingana nay ale waliyofanya, ninatarajia kuwa pamoja nao” (Muslim, Birr, 163)

Bila shaka, ili kwamba muumini aweze kuingia katika ahadi hiyo iliyotajwa na Mtukufu Mtume ﷺ anatakiwa kuu-pamba moyo wake kwa upendo wa Mtume ﷺ na kuwangaza kwa nuru yake.

Hali ya Maswahaba wakati wa kifo cha Mtume, ilikuwa kama mishumaa iliyongua kwa huzuni mpaka ikayeyuka. Siku hiyo, nyoyo ziliungua ghafla kwa moto mkali wa shauku iliyotokana na kutengana na rafiki yao mkubwa.

Maswahaba walitupwa kutoka katika hali moja ya mchanganyiko kwenda nyingine. Hata Omar ؓ alipoteza fahamu kwa muda, mpaka aliposimama Abu Bakr na kuwatuliza watu. Nyoyo zenye mapenzi makubwa, ambazo hazikuzoea kutomuona hata kwa siku mmoja, sasa zisingemuona tena katika dunia hii. Abdullah ibn Zayd ؓ ambaye alishindwa kustahimili uchungu wa utengano huu mrefu, aliinua mikono



yake mbinguni akiwa mwenye huzuni, akamuomba Mungu akisema: “Ee Mwenyezi Mungu... yazibe macho yangu! Nisio- ne chochote katika dunia hii baada ya Mtume ambaye nilim- penda kuliko mtu yeyote yule!” Aliomba dua hii kutoka moy- oni mwake hali ya kuwa macho yake yakibubujika machozi, akawa kipofu hapo hapo na hakuona tena.<sup>44</sup>

Baada ya hapo pindi Abu Bakr ﷺ alipokuwa akijaribu kusumulia hadithi ya Mtume ﷺ kumbukumbu zake ziliku- wa zikimliza;na kujikuta anashindwa hata kutamka neno. Akielezea hali hiyo, Abu Hurayra ﷺ anasema: “siku moja Abu Bakr alipanda kwenye mimbari na kusema:

“Kama mjuavyo, Mtume wa Allah, mwaka uliopita, ali- kuwa amesimama mahali hapa niliposimama sasa hivi na” Akaanza kulia, akashindwa kuendelea. Kisha akayarudia maneno haya, lakini kwa mara nyingine alilia. Akajaribu kwa mara ya tatu, lakini alizidi kububujikwa na machozi” (Tirmidhi, Daawat, 105/3558; Ahmad, I, 3)

Licha ya kwamba muda wote alikuwa pembezoni mwa Mtume ﷺ katika uhai wake, lakini Abu Bakr ﷺ muda wote alikuwa na shauku yake ilizidi na kutamani kukutana naye



Bibi Aisha ﷺ anaelezea msisimko alikuwa nao baba yake wakati wa kifo chake kwenda kuungana na Mtume ﷺ: “Baba yangu alipokaribia kufariki aliuliza: “Leo ni siku gani?” Tukamwambia: “Jumatatu”.




Hapo akasema:








“Iwapo nitakufa usiku wa leo, msisubiri kunizika kesho ...kwani muda niupendao zaidi ni ule ambao ninakuwa karibu na kuungana na Mtume wa Allah”. (Ahmad, I, 8)


Baadhi ya maswahaba walikuwa wakiwahusudu wagonjwa waliokuwa katika hatua ya mwisho ya uhai wao kwa sababu wanakwenda kukutana na kipenzi chao, Mtume  walikuwa wakiwapa wagonjwa hawa salamu kwenda kwa sultan wa nyoyo .

Muhammad ibn Munqadir  alimtembelea Jabiri  aliyekuwa katika hatua ya mwisho wa uhai wake. Alipotambua kuwa kifo chake kilikuwa karibu, alimwambia Jabir  ili kumfurahisha:

“Ee Jabir fikisha salamu zangu kwa Mtume wa Allah...”  
(Ibn Majah, Janaiz, 4)

Maswahaba, waliokuwa na upendo wa dhati kwa Mtume , walikuwa wakipata furaha kubwa wanapomsikia Mtume akizungumziwa.

Bara  anaelezea raghba aliyekuwa nayo baba yake kusikiliza kumbukumbu zinazomhusu Mtume  kila alipopata fursa hata ndogo:

“Baada ya Abu Bakr as-siddiq  kununua tandiko la farasi kutoka kwa baba yangu kwa kiasi cha dirham kumi na tatu, alimuomba akisema:

“Muamuru Bara alete tandiko hili nyumbani kwetu kama ataweza”



Baba yangu akamwambia: “Hapana mpaka utuhadithie mliyovofanya wewe na Mtume ﷺ wakati wa hijra ya kutoka makka kwenda madina huku washirikina wakiwatafuta!”

Abu Bakr ؓ alielezea kwa muhtasari safari hiyo kama ifuatavyo:

“Tuliondoka pangoni tukaanza kutembea. Tulitembea usiku wote na siku iliyofuata. Ilipokuwa mchana nilitazama huku na kule kwa matarajio ya kupata kivuli. Nikaona mwamba uliokuwa na kivuli kidogo. Nilikwenda haraka kusawazisha udongo uliokuwa chini ya kivuli hicho kisha nikamtandikia Mtume ﷺ ili apate kukaa. Nilimwambia: “Tafadhali pumzika hapa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu” Mtume ﷺ akajipumzisha kidogo.

Nilianza kuangalia huku na kule kuona kama kuna mtu anakuja. Badala yake nikamuona mchungu kondoo akiwaongoza kondoo wake upande tulipokuwa hali ya kuwa ni mwenye kutafuta kivuli. Nikamuuliza: “Wewe ni kijana wa nani?. Akanitajia jina la mtu ninayemfahamu katika Maquraishi. Kila nikamuuliza: “Je kondoo wako wana maziwa?”. Akanijibu “ndiyo” “waweza kutukamulia maziwa?” nilimuuliza.<sup>45</sup> Akasema: “Bila shaka ninaweza..”

45. Ilikuwa ni desturi ya Waarabu kutowanyima wasafiri maziwa ya wanayama wao. Walikuwa wakiwatanabahisha wachungaji wao kutomnyima maziwa msafiri yeyote. Katika hilo Mtume ﷺ anasema: “Watu watatu Mwenyezi Mungu hatozungumza nao siku ya kiama: Mtu aliyemnyima msafiri maji ya ziada aliyooanayo, yule ambaye baada ya asr hutoa kiapo cha uwongo ili tu kuza bidhaa zake, na yule anayekula kiapo cha utii kwa khalifa kisha anatekeleza kiapo hicho pale anapopewa kitu na khalifa, na anaacha kutekeleza kiapo chake pale asipopewa kitu” (Abu Dawud, Buyuu, 60/3474)



Haraka sana alimkamata kondoo mmoja, nikamwambia aisafishe mikono yake na azisafishe chuchu za kondoo huyo. Aliisafisha mikono yake kwa kuipiga pamoja kabla ya kukamua maziwa kidogo na kunipatia. Nilikuwa nimechukua kiribi cha ngozi kwa ajili ya Mtume ﷺ, ambacho nilikuwa nimekifunga kwa kitambaa. Nilimimina kiasi cha maji kwenye maziwa mpaka yakapowa kiasi. Niliyapeleka kwa Mtume ﷺ na kumkuta ameamka kutoka mapumzikoni, nikamwambia: “Tafadhali, ee Mtume wa Allah, kunywa maziwa”, Akanywa na hapo ndipo nafsi yangu ikapata kutulia” (Bukhari, As-habun-Nabi, 2; Ahmad, I, 2)

Maswahaba walikuwa wakimpenda na kumheshimu mno Mtukufu Mtume ﷺ kiasi kwamba kuna baadhi ambao walikuwa hawathubutu kukata nywele zao kwa sababu tu ziliguswa na mikono ya Mtume ﷺ. (Abu Dawud, Salat, 28/501)

Ishara adhimu ya upendo wao kwa Mtume ﷺ ni tukio lifuatalo linaloonyesha Maswahaba wanawake walivyopan-dikiza mbegu ya upendo huo kwa watoto wao. Walikuwa wakiwakaripia pindi wanapokuwa hawajamuona Mtume ﷺ kwa muda mrefu. Miongoni mwao ni hudhayfa ة, aliyegombeza na mama yake kwa kutomuona Mtume ﷺ kwa siku kadhaa. Hudhayfa mwenyewe anasema: “Mama yangu aliniluliza kuhusu siku ya Mwisho niliyokutana na Mtume wa Allah. “Ni siku kadhaa sasa”, nilimwambia. Alinilaumu na kunikaripia vikali. Nikamwambia: “Nitakwenda mara moja kwa Mtume ﷺ kuswali maghribi pamoja naye na kumuomba atuongee maghfira, mimi na wewe” (Tirmidhi, Manaqib, 30/3781; Ahmad, 5, 391 – 392)



Hali ya bila ﷺ, huadhini mkuu wa msikiti wa Mtume, ilikuwa zaidi ya hiyo. Mara Mtume ﷺ alipofariki dunia ilikuwa kana kwamba ulimi wake umekatwa na hakuweza kufungua mdomo wake. Licha ya ukubwa wa mji wa Madina lakini ulionekana mdogo machoni pake.

Katika kukumbushia enzi tamu za adhana ya wakati wa Mtukufu Mtume ﷺ, Khalifa Abu Bakr ﷺ alimuomba Bilal ﷺ mara nyingi atoe adhana kwa mara nyingine. Lakini Bilal mwenye maumivu na huzuni alikuwa akitoa udhuru na kusema: “Ewe Abu Bakr, kama ukitaka kujua ninavyojihisi, sina nguvu kabisa za kuto adhana baada ya kifo cha Mtume wa Allah...hivyo, ninakuomba tafadhali, niache na hali ya nafsi yangu”

Lakini Abu Bakr ﷺ alikuwa akiendelea kumuomba aukumbushe umma enzi tamu za wakati wa Mtume ﷺ kwa kumwambia: “Je ummah utanyimwa adhana ya Mtume kama ulivyoondokewa na Mtume wa Allah?”

Ni kutokana na msisitizo huu ndipo alfajiri moja bilal alipanda mnarani akiwa ameinamisha kichwa chake na macho yaliyojaa machozi. Ingawa alijaribu kuzishinda hisia zake, lakini kumbukumbu ya zama za Mtume ﷺ ilifanya ashindwa kutoa sauti yake, akarejea pasipo kutoa adhana. Abu Bakr ﷺ hakumsisitiza tena.

Bilal ﷺ hakuweza kubaki tena Madina, mji uliojaa kumbukumbu za Mtume ﷺ kila kona. Hivyo baada tu ya sala ya alfajiri ya siku hiyo alielekea Damascus. Akichochea na matumaini ya kuungana na kipenzi chake, Mtume ﷺ bilal alishiriki katika vita vingi ili afe kishahidi za kwenda kuungana naye. Lakini kila mara alirudi salama. Miaka mingi ilipita.



Licha ya balaa la maradhi lililoikumba Damascus na kuwa watu elfu ishirini na tano, bado Mwenyezi Mungu alimuokoa bilal ؓ ambaye moyo wake ulikuwa ukiungua kwa shauku ya kuungana na Mtume ؓ.

Siku moja alimuona Mtume ؓ ndotoni akimwambia kwa huzuni: “Ni mtengano gani huu ewe Bilal? Je haujafika muda wa wewe kunitembelea?” Akiwa mwenye huzuni, Bilal aliamka. Bila kuchelewa alifunga safari kwenda kulitembelea kaburi la Mtume ؓ mjini Madina. Alipokuwa mbele ya kaburi la Mtume ؓ akilia sana kwa huzuni, Hassan na Husein wakafika. Akijawa na furaha ya kuwaona wajukuu hao wa Mtukufu Mtume ؓ ambao alikuwa akiwathamini sana kama “mirehani mitam ya peponi”, Bilal ؓ aliwakumbatia kwa furaha.

“Ee Bilal, tungependa kusikia adhana yako”, walimuomba sana Bilal, naye akawakubalia ombi lao. Adhana yake iliutikisa mji wa Madina. Aliposema: Ashadu anna Muhammadan Rasulullah, wanaume na wanawake wote walimiminika mitani na kuanza kujazana msikitini wakidhani kuwa Mtukufu Mtume ؓ amefufuka. Tangu alipofariki Mtume ؓ, hakuna siku ambayo watu wa Madina walilia sana kuliko siku hiyo. <sup>46</sup>

Swahaba huyo aliyekuwa na mapenzi makubwa kwa Mtume ؓ alifariki dunia mjini Damascus. Wakati huo alikuwa na umri wa zaidi ya miaka sitini.

Muda mfupi kabla ya kifo chake, alikuwa akisema kwa furaha: “Allah akipenda, kesho nitaungana na marafiki zangu wependwa, Mtume wa Allah na Maswahaba zake”

---

46. Ibn Athir, Usdul – Ghaba, I, 244 – 245; Dhahabi, Siyaru A'lamin – Nubelaa, Beirut 1986 – 1988, I, 357 – 358.



Mke wake akilia na kuhuzunika kwa kifo cha mumewe, wakati huo Bilal alikuwa akionyesha furaha, akisema, “furaha iliyoje...” (Dhahabi, Siyar, I, 359)

Upendo wa hali ya juu waliokuwa nao Maswahaba kwa Mtume unaweza kuonekana pia katika kupokea hadithi. Walipokuwa wakisimulia hadithi ya Mtume nyuso zao zilikuwa zikibadilika rangi na kuwa na rangi ya njano na viungo vyao vikitetemeka kwa kuhofia kusema jambo ambalo hali-kusemwa na Mtume.

Kwa mfano Abdullah ibn Masoud alikuwa akitetemeka sana pindi anapoanza kumnukuu Mtume

Maswahaba wengi, baada ya kumnukuu Mtume, haraka sana walikuwa wakisema: “Au kama alivyosema, au alisema yanayokaribiana na hayo” (Ibn Majah, Muqaddimah, 3)

Mtume alikuwa mtu Mtukufu kiasi kwamba gogo la mtende alilokuwa akisimama juu yake kuhutubia watu lililia kwa kifo chake. Maji yalibubujika kutoka katika vidole vyake ili kukata kiu ya ummah wake. Wagonjwa walipona kutokana na maji yake aliyofanyia wudhu. Wale waliokuwa naye katika chakula walisikia chakula kikifanya tasbihi mikononi mwake.<sup>47</sup>

Nywele na ndevu zake tukufu zimehifadhiwa katika misikiti mpaka leo, zikithaminiwa kama urithi wa upendo kwake.

Yeye ndiye kiongozi wa uwanda wa ufufuo siku ya kiyama, yeye ndiye muombezi wa wako saji,



Bendera ya liwaaul-Haud ya siku ya kiama itakuwa miko-  
no ni mwake,

Mitume wote watakuwa chini ya kivuli chake, mkono wa  
kwanza kufungua milango ya pepo ni mkono wake...

Sheikh Ghalib anaelezea kwa uzuri hali hii akisema:

Katika mimbari za ughaibuni, khutba yako inasomwa,  
katika mahakama ya mwisho, hukumu yako inafanya kazi,  
ujio wako unapokelewa katika Arshi.

### **Chemchem Ya Upendo Baada Ya Maswahaba**

Msafara wa kumpenda Mtukufu Mtume ﷺ, ambaye ni  
rehma kwa walimwengu wote baada ya maswahaba uliende-  
lea kwa shauku ile ile kumiminika kam mto mkali kuelekea  
kwenye bahari ya muungano mpya, kwa kutambua kikamilifu  
kwamba amani na neema katika dunia na akhera vinapati-  
kana tu kwa kumpenda.

Mtume ﷺ alieleza kwamba wale wanaompenda wata-  
endelea mpaka siku ya mwisho:

“Katika watu wenye mapenzi sana na mimi, katika  
ummah wangu, watakuwa katika wale watakaokuja baada  
yangu. Watakuwa tayari kupoteza familia na mali zao ili  
kuniona” (Muslim, Jannat, 12; Hakim, 4, 95/6991)

Tunamuomba Allah Mtukufu atujaalie sisi, waja wake  
dhaifu, tuwe katika watu hao waliosifiwa katika hiyo hadithi!  
Amin...



Maelezo yafuatayo, yaliyotolewa na Abdullah ibn Mubarak, yanaonyesha kwamba upendo wa watu kwa Mtukufu Mtume ﷺ ulikuwa ukivuka mipaka ya maumivu na shida zote zenye kukoma: “Nilikuwa kwa Iman Malik wakati za Mtume wa Allah. Wakati akiendelea kusoma, uso wake ulidhihirisha wasiwasi na maumivu, ukabadilika rangi na kuwa ya njano. Hata hivyo aliendelea kufikisha maneno ya mtume ﷺ na kukamilisha darsa. Watu walipoondoka nilimwambia” “Ewe Abu Abdillah leo nimeona kwako jambo la ajabu”. Akania-mbia “Ndiyo. Wakati nikisomesha kadhaa, lakini nilifanya subira kwa kuheshimu maneno ya Mtume wa Allah”<sup>48</sup>

Imam Malik alikuwa hapandi ngamia au farasi katika mji wa Madina kwa heshima ya udongo na ardhi iliyokanyagwa na Mtume ﷺ, na anapotembea alikuwa havai viatu. Anapojiwa na mtu kumuuliza kuhusu hadhithi fulani kwanza hufanya wudhu, hufunga kilemba (Imamah) hujipulizia manukato, hukaa juu ya kiti kirefu ndipo huweza kumjibu.

Alikuwa akijiandaa kiroho kwa ajili ya heshima ya Mtukufu Mtume ﷺ, na akichukua tahadhari kubwa sana ya tabia zinazofaa katika kufikisha maneno ya Mtukufu Mtume ﷺ. siku zote imam alizungumza kwa sauti ya chini anapokuwa katika eno la Rawdhah (eneo tukufu lililopo baina ya mimbari na kaburi tukufu la Mtume). Ni kwa sababu hiyo kwamba Khalifa Abu Jafar Mansur alipozungumza kwa sauti ya juu mahali hapo, Imam maliki alimtahadharisha kuwa: “Ewe Khalifa! Punguza sauti yako mahali hapa. Kwani Allah

---

48. Munwi, Faydhul-Qadir, Beirut 1994, III, 333; Suyut, Miftahul Jannah, Uk.52.





alikataza kuzungumza kwa sauti ya juu mbele Mtume ﷺ na maonyo na makatazo hayo yaliwaonya watu waliokuwa na ubora na hadhi ya juu kuliko wewe..”

Mara nyingine Imam malik alimsamehe Gavana wa mji wa Madina ambaye alikuwa amemsababishia tabu, akamwambia: “Mimi ninaona tabu kutaka haki zangu siku ya kiyama kutoka kwa mmoja wa wajukuu wa Mtume ﷺ”.

Sayyid Ahmad Yasawi, mmoja wa viongozi wakubwa wa ummah waliokuwa na mapenzi makubwa kwa Mtume ﷺ aliacha kuishi juu ya uso wa ardhi baada ya kufikia umri wa miaka sitini na tatu, ambao ni sawa na umri wa Mtume ﷺ, na kwa muda wa miaka kumi mpaka kifo chake, aliendelea kuwaita watu kwenye njia ya haki katika sehemu inayoshabihi kaburi.

Naye mwanachuoni mkubwa wa hadithi, Imam Nawawi, hakula tikitimaji kwa sababu tu kwamba hakujua namna Mtume ﷺ alivyokuwa akilitumia.

Ama Yavuz Sultan Selim, ambaye alikuwa mtawala wa dunia wakati huo, anamuona mtu mwema anayeipeleka nafsi yake kwenye uhalisia wa Mtume ﷺ kuwa yuko juu ya chochote kile katika uso wa ardhi. Hisia hii anaielezea katika beti zifuatazo akiweka msisitizo juu ya kuwa karibu na marafiki wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake:

“Kuwa mtawala wa dunia ni vurugu na maudhi lakini kuwa mwanafunzi wa mtu mwema ni bora kuliko chochote...”

Hapo zamani palikuwa na desturi ya kuzinakishi pete kwa ubeti au mkuu. Katika kuonyesha jinsi Mwenyezi Mungu alivyouumba ulimwengu kwa heshima ya upendo wake kwa



nuru ya Muhammad, Bezmi Alem Valide Sultan aliinakishi pete yake kwa maneno yafuatayo:

“Kutokana na upendo, Muhammad alizaliwa, Bila Muhammad ...

Upendo hauna kitu kutokana na ishara za upendo huo Bazmi Alem alitokea...”

Fudhuli anaelezea moto huu wa upendo katika utenzi wake mashuhuri uitwao Su kasidese kama ifuatavyo:

Ewe jicho langu usimwage chozi la maji yako ya upendo kwa ajili ya moto ulio katika moyo wangu, kwani maji haya-toweza kuizima miale itokanayo na moto wa upendo.

Nimefadhaika, macho yangu hayajui mbinguzi napata wapi rangi zake,

Je machozi yangu amezifanya zitande au kweli zina rangi ya maji?

Basi mtunza bustani na ayaelekezi maji yote kwenye bustani mpaka liharibike kwa sababu hata akimwagilia mabustani elfu moja hayawezi kutoa au linalofanana na uso wa Mtume 🕌.

Lau nikifa kabla ya kuibusu mikono yake Mitukufu,

Basi, enyi wenzangu, tengenezeni bilauri kutoka katika udongo wa kaburi langu na ndani yake mpeleke maji kwa mpendwa wangu.

Maji yanatembea bila kujitambua yakijipiga kwenye miamba ili kufika kwenye nyanda alizokanyaga. Naye Suley-



man Shelabi akieleza kuwa hata jua linamzunguka Mtukufu Mtume ﷺ, anasema: “yeye ni Nuru ambayo jua linaizunguka”

Ama Sultan Ahmad, yeye alichora nyoyo za mtume ﷺ kwenye kilemba chake kwa nia ya kupata msukumo wake, na akaandika ushairi kuhusu jambo hilo akisema:

Laitani nigekuwa nimebeba kichwani mwangu kama taji,  
Miguu halisi ya sultan wa Mitume?  
Yeye ni uaridi la bustani la Mitume,  
Hivyo, ee Ahmad, weka taji kwa nyayo za uawiridi hilo.  
Upendo kama huo unaelezwa na Aziz Mahmud Hudayi:  
Ujio wako ni rehma na furaha yenye raha,  
Kukuona wewe ni dawa kwa wenye maradhi ya upendo,  
Muombe Hudayi nje na ndani,  
Amejikunja mlangoni kwako,  
Yeye ni mateka wa masaibu.

Mshairi Naabi, msafara ulipokaribia Madina katika safari yake ya Hijja, alisikitika sana kumuona pasha (Jenerali wa Jeshi) akiwa ameunyoosha mguu wake kwa bahati mbaya kuelekea upande wa Rawdhah Tukufu.

Akaandika shairi lifuatalo akiwa katika hali ya kuhuzunika akielezea heshima yake kwa Mtukufu Mtume ﷺ:

Jizuie na utovu wa adabu kwani hii ni ardhi ya kipenzi cha Allah,



Hili ni eneo linalotazamwa na Allah na ni eneo la Mtume, Ee Naabi ingia katika eneo hili tukufu kwa sharti la kucunga adabu,

Hili ni eneo linalotembelewa na watakatifu na mahali panapotukuzwa na Mitume”.

Kutokana na msukumo wa dhati uliotoka katika moyo wa Naabi, kwa ishara ya muujiza wa Mtume wa Allah, waadhini wa Rawdhah Tukufu walilisoma shairi hilo kwa sauti wakati wa sala ya alfajiri katika minara ya Rawdhah hiyo. Naabi, akiwa ameathiriwa sana na hali hiyo, aliingia katika Msikiti huo hali ya kuwa ni mwenye machozi.

Muhammad As’ad Effendi, mmoja wa Masheikh wakubwa wa zama hizi, anaelezea kwa namna nzuri sana kuhusu namna nyeyuko anaohisi kutokana na miale ya upendo wa Mtume ❀ inayounguza taratibu:

“Kutokana na muonekano wako wenye kuteka nyoyo, ee kipenzi changu, majira ya kuchipua yamewaka moto.

Mawaridi, kurumbiza, udongo na mwiba vimewaka moto.

Miale ya uso wako wenye nuru ndio uliowaunguza wapendao wote.

Ulimi, moyo na macho yanayolia kutokana na upendo wako yamewaka moto.

Inawezekanaje kuwaosha mashahidi wa upendo pamoja na huu moto wote?

Mwili, Sanda na hata maji safi ya kuuoshea yamewaka moto”



Uzuri ulioje wa mashairi yaliyoandikwa na mshairi mmoja wa zama hizi aitwaye Yaman Dede! Mshairi huyu alikuwa mkristo, kwa bahati nzuri aliutambua ukweli na hakika ya dhati ya Muhammad, akabadilika kuwa muumini wa kweli mwenye kulia na mwenye upendo wa kweli katika watu wenye maradhi ya upendo wa Mtume ﷺ.

Mshairi huyo anasema:

“Ningeshikwa na kiu kali na kuisalimisha roho yangu katikati ya jangwa lenye kuchoma moto nisingehisi maumivu,

Volcano zinazolipuka katika moyo wangu, hata kama bahari zingemiminika juu yangu nisingehisi ubichi na unyevu,

Lau mbingu zingenyesha miale ya moto nisingehisi chochote,

Nipe faraja kwa uzuri wako, ee Mtume, hakika mimi ninaungua.

Furaha iliyoje kwa mtu kufumba macho yake kwa ajili ya kukupenda na akaitoa roho yake katika njia yako,

Je haiwezekani kwangu kuitoa roho yangu kwenye mlango wako, ee Bwana wangu?!

Itakuwa rahisi sana kuisalimisha roho yangu huku macho yangu yakisalim amri,

Nipe faraja kwa uzuri wako, ee mtume hakika moyo wangu waungua.

Nimevunjika moyo, nimedhoofika, na dawa yangu iko kwako.



Kinywa changu kimeungua huku kikinong'ona kwa kuli-taja jina lako mbele ya enzi yako, Mbariki huyu mtu wa kawaida pindi utakapo moyo wako.

Nipe faraja kwa uzuri wako adhimi, ee Mtume, hakika moyo wangu waungua.

Kama Adib Kurkcuglu anaeleza kwa ufasaha shauku na hamasa ya mbingu kutokana na tukio la miraj (safari ya Mtume ﷺ kwenda mbinguni):

Usiku wa Miraj kwa kuuona uso wake,

Mbingu zilisujudu kuonyesha shukrani.

Na Roho Mtakatifu akiwa na msisimko hali ya kuwa ni mwenye kuvaa ihram kila usiku, huteremka kama mgeni kwenye lango lake,

Kila anayemuona mara moja hupiga kilele "Allah Allah" akirukwa na akili na kutamani kuuona uso wake kwa mara nyingine.

Huyo ni Mtume wa Allah ambaye wale wote waliom-kubali kama muongozo na kumfuata wamekuwa watu wa kipekee, kama nyota zing'aazo mawinguni.

Maswahaba marafiki wa Allah, waliweza kupata ubora na hadhi ya juu kutokan na kiwango cha ukaribu wao kwa Nuru hiyo Adhimu ya viumbe, yaani Mtume ﷺ.

Tuna kiwango gani cha hisia za moyo kama zile za Abdullah ibn Zayd, Bilal Habashi, Imam Nawawi, Sayyid Ahmad Yasawi na mfano wao? Kwa hali hiyo, tunapaswa kupima kiwango chetu katika kumpenda Mtume ﷺ, na tuzi-



ulize nafsi zetu ni kwa daraja ipi tunayostahiki kuwa katika ummah wa Muhammad ﷺ na kuzilisha roho zetu mwamko na uhuisho wa kiroho.

Yote hayo tunatakiwa kuyafanya ndani ya wigo wa ishara ya upendo huo uliofirika kutoka enzi za Maswahaba ﷺ.

Kwa hakika hali za watukufu wa kiislam waliotajwa hapa ni za viwango vya juu sana kama nyota. Lakini kilichowafanya kuwa nyota katika anga za nyoyo za waislam ni upendo wa hali ya juu waliokuwa nao kwa Mtume ﷺ na mafungamano waliyokuwa nayo kwake.

Twajua kuwa upendo ni kama mkondo wa umeme unaoziunganisha nyoyo mbili. Na ili uwe muumini wa kweli, sharti moyo wako uupatie uwezo huu. Na kihoro kinachomsumbua binadamu wa leo kinatokana na moyo wake kukosa uwezo huu wa kimoyo. Ni kwa sababu hiyo kwamba misingi mikubwa imepote na kuangukia chini ya nyundo nzito ya matamano ya nafsi. Na pindi mielekeo yote inapokuwa ya kinafsi na kidunia hakuna awezaye kupata njia katika kuitia nguvu roho.

Binadamu hawezi kupaa kutoka kwenye upendo wa istiaari (wa bandia) na kwenda kwenye upendo wa kweli, na kama ambavyo Qays ajulikanaye kama “Majinun” hawezi kufika kwa Bwana katika safari yake iliyoanza kwa Layla, isipokuwa kwa kuufunda moyo na kuupa mazoezi ya kupata uwezo wa kuwa na upendo huu wa kweli, ambao binadamu wa leo anauhitajia sana. Maovu, jinai na uhalifu ulioeena kwa kasi sana unasababishwa na kukosekana kwa upendo huu.



Ukubwa na upana wa upendo hupimwa kwa namna ambavyo mtu hujitolea na kuingia katika mazingira hatari kwa ajili ya yule anayempenda. Kwa sababu mtu mwenye upendo wa kweli huwa yu tayari kuitoa muhanga roho yake kwa ajili ya yule anayempenda, na wala hahisi hata kidogo kwamba amejitolea muhanga, bali huhisi kuwa amelipa deni lililokuwa juu yake. Lakini wale wasioujua hata chembe upendo huo kikamilifu, hawawezi kuingia kikwelikweli katika njia iendayo kwenye ukamilifu, huzipeleka nyoyo zao kwenye hasara na huziangamiza na kuzifunga kwenye minyororo ya matamania na nafsi.

Kukubali kubeba *amanah*, ambayo hata milima ilikataa kuibeba, kimsingi ni upendeleo na heshima kubwa ambayo Mwenyezi Mungu alimtunuku mwanadamu. Na sharti la kupatikana kwa heshima na upendeleo huo kwa maana yake halisi lipo katika uwezo wa kuufikia upendo wa kweli. Kwa sababu migogoro na mapambano yaliyopo katika roho ya mwanadamu huyeyuka na kutoweka katika upendo huo wa kweli tu. Binadamu aliyekamilika hutakasa roho yake dhidi ya matakwa ya kihayawani kwa kuakisi nguvu kutoka kwenye kiigizo cha mfano na kuubadilisha moyo wake kuwa bustani ya pepo, ambayo ndani yake madirisha ya moyo hufunguliwa kwa ajili ya kutazamwa na Mwenyezi Mungu.

Mola wetu Mtukufu anatueleza ndani ya Qur'an Tukufu:

“... Nikampulizia roho inayotokana na Mimi”. (al- Hijr:29)

Mwenyezi Mungu anamkumbusha mwanadamu juu ya asili yake Kuu itokanayo na Mungu. Asili hii ambayo mwanadamu alipewa na Mungu. Pindi asili na dhati hii kuu







inaoweza kumfikisha muumini kwenye ukamilifu kwa njia ya upendo, hapo moyo huanza kukata masafa kuelekea kwenye ulimwengu wa siri za Kimungu. Na kwa hiyo, siri za ukweli wa vitu, mwanadamu na ulimwengu hupata kudhihiri, na mja huwa ishara ya moyo safi.

Mja anapofikia kwenye ukamilifu huu, huanza kuondoa mapazia baina yake na Mola wake, na kupata sehemu ya siri za “**Kufa kabla ya kifo**”. Dunia na hadaa zake za muda huondoka ndani ya moyo wake, na hapo roho hupata kuonja ladha tamu isiyoelezeka ya ukaribu na Muumba wake.

Ama wale ambao hawajaonja upendo wa kweli hawawezi kuzivunja kuta za matamano ya kihayawani yanayomzunguka mwanadamu na kushindwa kupiga hatua kuelekea kwenye uwanja wa malaika. Na moyo usiojua upendo ni kama ardhi isiyokuwa na rutuba. Upendo ni makazi ya maarifa, na ndio sababu ya uhai.

Rehema ya Mwenyezi Mungu iliyomkomboa mwanadamu na kumwinua kutoka kwenye upotovu na uduni kumpeleka kwenye furaha, rehema hiyo ni Mtume  aliyeletwa kama kiigizo na ruwaza njema kwa watu. Na njia ya furaha ya kweli inapatikana kwa kujifunza upendo wa kweli kutoka kwake, kuingia katika tabia zake, kufuata muongozo wake na kuenenda katika njia ya upendo wake.

Mtukufu Mtume  ni kpenzi cha ulimwengu mzima na ndiye sababu ya kuwepo kwake. Yeye ndiye muongozo unaunganisha baina ya mja na Mola wake. Kwa mfulululizo wa matendo yake yenye ukuu, yale yanayoweza kuelezeka na yale yasiyoweza kuelezeka hata kidogo, mpaka mwisho wa




uhai wake, ametupatia mfano bora wa namna ya kuwa mja wa Mwenyezi Mungu.

Kwa ufupi, yeye ni rehema na upendo uliooenea katika kila uwanda wa ulimwengu. Nyoyo zenye upendo wa dharti kwake klatika ulimwengu huu, zitaendelea kuungua kwa kumpenda. Kila mara zitakunywa kikombe cha shauku ya kuungana naye; na kutokana na miale hii ya moto wa upendo katika nyoyo zao, wataomba wakisema:

“Nipe faraja kwa muonekano wako ulio jamali, ee Mtume wa Allah, hakika mimi ninaungua”. Kilio hiki kitafungua wigo wa hewa ya upendo.

Upendo huu ndio uliowafanya watu kama Bahauddin Naqshibandi, Yunus na Mawlana Rumi wawe nyota zing’azo katika anga za kiroho. Ni kwa upendo huu kwamba Mawlana Rumi alipiga hatua ndani ya yulimwengu wa furaha ya kweli na ya milelel; furaha ambayo ni njia ya kuelekea kwa Muumba Mwenye ukuu na uweza wa milele. Watukufu hawa walijivua minyororo ya mwili wenye kukoma, wakakata masafa kuelekea akhera. Hakuna kilichokuwa kikiwafurahisha zaidi kuliko maisha ya akhera na ya milele. Itawezekanaje mtu ahisi furaha ya kweli pamoja na wale wanaokufa na kutoweka! Hivyo, njia ya furaha ya milele hupita kwenye njia ya kuusalimisha upendo pahali unapostahiki.

Katika jambo hili, maneno yafuatayo ya Mawlana Rumii yanaonyesha chanzo cha furaha yake pale anaposema:

*“Mimi ni mtumishi wa Qur’an kwa muda wote nitakuwa hai. Mimi ni vumbi la njia ya Muhammad . Mimi*



*niko mbali na maneno ya yule atakayefikisha maneno mengine tofauti na haya ninayosema”.*

Maana ya kuwa vumbi la njia ya Mtukufu Mtume ﷺ na kuitoa muhanga nafsi yako kwa ajili yake ni wewe katika umri wako wote kuendelea kumfuata yeye na sunna zake na uishi kwa kufungamana naye moja kwa moja katika mambo yako yote, madogo na makubwa.

Njia nyingine ya mafungamano yanayotakiwa katika kumfuata na kuingia ndani ya upendo wake ni kuifanya *Salawat’us-Sharifah* (kumtakia rehma Mtume) iendeleo kuzunguka katika ndimi zetu. Kwa sababu *salawat* hizo zitaimarisha mafungamano yetu ya kiroho kwake na nyoyo zetu zitapata nuru ya upendo wake.

### **Salawat’us – Sharifah**

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameapa kwa maisha ya Mtume ﷺ ndani ya Qur’an Tukufu. Akafanya kuamini utume wake kuwa sharti la mtu kuwa muumini wa kweli, na hakuwa radhi kwa yeyote kuinua sauti mbele ya Mtume ﷺ, akionya juu ya kuliita jina lake kama majina mengine. Zaidi ya hayo, Mwenyezi Mungu ameeleza kuwa Yeye na malaika wake humtakia rehma, na akaamuru *ummah* wake ufanye hivyo humtakia rehma, na akaamuru *ummah* wake ufanye hivyo. Allah anasema ndani ya kitabu chake kitukufu:

*“Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi Mlioamini msalieni na mumsalimu kwa salam”.*

(al – ahzab: 56)



Kumtakia rehma Mtume ni wajibu uliowekwa na Mwe-nyezi Mungu kwa waumini wote.

Hadithi ifuatayo inasimuliwa na Ubayy ibn Kab ؓ:

“Theluthi ya usiku ilikuwa imepita ambapo Mtume wa Allah aliamka na kusema:

‘Enyi watu! Mkumbukeni Allah, mkumbukeni Allah! Mpulizo wa mwanzo wa baragumu utavitikisa viumbe vyote, na kisha utafuatiwa na mpulizo wa pili. Mauti yatakuja na nguvu zake; mauti yatakuja na nguvu zake...’

Nikasema: ‘Ee Mtume wa Allah, hakika mimi ni mwingi wa kukutakia rehma, je ninatakiwa kuifanya mara ngapi?’

Akaniambia: “Kiwango utakacho’.

Nikauliza tena: ‘Itakuwa sawa iwapo nitatumia robo ya maombi yangu?’

Akasema: ‘Kiwango chochote utakacho, lakini ukizidisha ni bora kwako’.

Nikasmea: ‘Nusu’.

Akasema: ‘Kiwango chochote upendacho, ukizidisha ni bora kwako’.

Nikasema: ‘Basi theluthi mbili’. Akasema: ‘upendavyo, lakini ukizidisha ni bora kwako’.


Nikasema: ‘nitakutakia rehma kwa muda wote ninaotumia kwa maombi yangu’.

Akasema: ‘ikiwa ni hivyo Allah atakuondoshea matatizo yako na kukusamehe dhambi zako’”. (Tirmidhi, Qiyamat, 23/2457)



Hivyo, wale wenye mapenzi ya dhati kwa Mtume ﷺ wali-fanya kumtakia rehma na amani kama nyiradi katika ndimi zao. Kwa sababu kumtakia rehma na amani ni nyenzo ya kuzidisha hali ya kumpenda ndani ya nyoyo za waumini. Kwa hakika, kumfuata Mtume ﷺ kwa namna inayomstahili, na kumtumia kama kiigizo na ruwaza njema, bila shaka inawezekana kwa kuutambua vyema uhakika wa Qur'an na Sunnah. Jambo hili linawezekana tu kufikiwa kwa kujikurubisha zaidi na maadili na tabia njema za Mtume ﷺ, na kuzama ndani ya kina cha moyo wake.

Hakuna kiumbe mwenye sifa ya kufa, aliyeweza kuelezea sifa zake halisi kabisa na kuweza kiutambua *fitrah* na tabia zake za juu kwa namna inayostahili. Watambuzi, masultani wa nyoyo, na hata Jibril, wote waliitambua heshima kubwa katika kufuata njia yake, na neema isiyoelezeka kwa wao kusi-mama mlangoni kwake.

Kwa upande mwingine, kwa mujibu wa adabu za Kiislamu katika dua, maombi yote yanatakiwa kuanza na kumalizika kwa kumhimidi Allah na kumtakia rehma Mtume ﷺ. Kuna uthibitisho kuwa kamwe Allah haikatai wala kuirudisha dua iliyoombwa kwa kumtakia rehma Mtume ﷺ. Kwa hali hiyo kuupamba mwanzo na mwisho wa dua zetu kwa kumtakia rehma Mtukufu Mtume ﷺ huzipa uhakika wa kujibiwa. Omar  anasema:

“Dua huachwa ikining'inia baian ya mbingu na ardhi, na haipandi kwa Mwenyezi Mungu mpaka umtakie rehma Mtume ﷺ”. (Tirmidhi, Witir, 21/486)



Siku moja Mtukufu Mtume 🌿 alimuona mtu mmoja ambaye, baada ya swala, alikuwa akiomba dua bila kumhimidi Allah na kumtakia rehma Mtume 🌿. Mtume akasema: “amefanya haraka huyu”, kisha akmuita na kumshauri akimwambia: “Wakati wa kuomba, yatakiwa kuanza kumhimidi na kumsifu Allah na kumtakia rehma Mtume, na baada ya hapo uendelee kuomba utakavyo”. (Tirmidhi, Da’awat, 60/3477)

Umuhimu wa kufanya *tawassul* katika dua kupitia kwa Mtume 🌿 unaelezewa katika tukio lifuatalo:

“Wayahudi wa Khaybar walikuwa wakipambana na watu wa kabila la Ghatafan, na kila mara Wayahudi walikuwa wakishindwa. Hatimaye walimuomba Mungu kwa maombi yafuatayo:

‘Mola wetu! Tunakuomba ushindi kwa jina la Mtume asiyesoma wala kuandika ambaye umeahidi kumleta katika zama za mwisho.’” Baada ya dua hiyo waliwashinda maadui zao wa Ghatafan. Lakini, pindi Allah alipomleta Nabii huyo waliyemtaja katika maombi yao waliukanusha utume wake pamoja na kitabu alichoteremshiwa; ambapo Allah anatueleza akisema:

*“Na kilipowajia kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu kinachothibitisha waliyonayo – na wao walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri – yalipowajia yale waliyokuwa wakiyajua waliyakanusha. Basi laana ya Mwenyezi Mungu juu ya wakanushao”.* (al – baqarah, 89) (Qurtubi, II, 27; Wahidi, uk. 31)

Hii inaonyesha ukweli kwamba hata wasiokuwa Waumini waliweza kufaidika na neema na rehma iliyoenea ulimwen-



guni kwa ujio wa Mtume wa rehma ﷺ, kutokana na hadhi yake mbele ya Mwenyezi Mungu.

Allah Mtukufu anamwambia Mtukufu Mtume ﷺ akisema:

*“Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaadhibu nawe umo pamoja nao, wala Mwenyezi Mungu si wa kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha”.* (al- anfal: 33)

Hakikisho hili kutoka kwa Mwenyezi Mungu liliteremshwa pia kuhusu Makafiri. Ikiwa wamepata heshima hiyo kwa sababu tu ya kuwa karibu kimwili na Mtume ﷺ, bila shaka neema zinazowasubiri waumini ni nyingi kupita maelezo; hususan ikichukuliwa kwamba wanaamini daraja kuu ya Mtume ﷺ, na zaidi ya hilo, wana fungu kubwa litokanalo na upendo wao kwake ambao ni kiini cha imani yao. Hapa maelezo hukosa nguvu.

Kwa hakika, moyo wa muumini ukipata daraja yoyote katika kupenda Mtume ﷺ, bila shaka kiwango hicho kitampandisha cheo huko akhera na kumuongeza furaha anayoipata katika dunia.

Hivyo, usisahau kumtakia reham na amani, kwani siku ya kiyama utahitajia uombezi wake.









# *Sehemu Ya Nne*



✿ Hitajio Kuu La Moyo Na Akili: Shahisia Ya  
Kielelezo Malezi Yanayomtengeneza  
Mwanadamu: Mafundisho Ya Kimungu



## Hitajio Kuu La Moyo Na Akili: Shakhisia Ya Kielelezo Malezi Yanayomtengeneza Mwanadamu: Mafundisho Ya Kimungu

Mwenyezi Mungu amezifanya mbingu na ardhi zimtumikie mwanadamu,<sup>49</sup> na hakumuacha kurandaranda bila jukumu lolote mbele ya vitu hivi na mbele ya nafsi yake.<sup>50</sup> Yaani, Mwenyezi Mungu alimpa muongozo mwanadamu na ulimwengu kupitia kanuni mbalimbali za Kimungu, akiweka uwiano (balance) mzuri kati ya uhuru na uwajibikaji katika maisha haya ya majaribio. Aya zifauatzo zinafafanua jambo hili na kusema:

*“Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani. Ili msidhulumu katika mizani”.* (ar – Rahman: 7 – 8)

Aya hizi zinasisitiza juu ya ulazima wa mwanadamu kuungana na kufungamana na mizani iliyowekwa na Allah ndani ya ulimwengu. Kama ambavyo hakuna kasoro hata ndogo katika mfumo wa ulimwengu huu mpana, ndivyo ambavyo mwanadamu anatakiwa kutekengeuka katika safari yake ya kumuelekea Allah.

Watambuzi pekee ndio wenye bahati kubwa kuliko watu wengine, kwa sababu maisha yoyote wanaishi ndani ya

---

49. Tazama: Surah al – jaathiyah: 13.

50. Tazama: Surah al – qiyama: 36.



mfumo sawa na huu wa ulimwengu. Lakini wale wasioishi katika mizani, wakazijaza nyoyo zao kwa matamania yenye kwisha, na wakapendelea kile chenye kutoweka, hao hawaitambui siri ya kuja na kuondoka ulimwenguni. Watu hawa, vilevile, hawawezi kuungana na uelewano mzuri ambao Allah ameuweka ndani ya ulimwengu, huku wakishindwa kuutambua. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba, maisha ya watu hawa hupita katika dimbwi kubwa la mghafala, huku akhera yao ikiwa ni hasara na majuto makubwa.

Jawabu la suala hili limo katika hakika ya binadam. Na hakika hiyo ni kwamba, binadamu alipoletwa duniani kwa ajili ya majaribu haya, iliumbwa ndani mwake hali ya kupenda kheri na shari. Kwa sababu mtihani huwa ni mtihani pale tu mtu anapokuwa na uwezo wa kufanya mambo yote mawili, yaani kukosea na kupatia (baya na jema).

Ni kwa sababu hiyo kwamba katika maisha yake yote mwanadamu huwa katika mapambano ya daima kati ya kheri na shari (uovu na wema) katika ulimwengu wake wa nje na ndani. Kwa sababu vitu vyote hivyo viwili hutaka kumtawala na kumdhibiti. Kama ambavyo ndani mwake kuna nguvu ya kheri, ndivyo ambavyo kuna nguvu ya shari, nguvu ya nafsi inayoamrisha maovu, na ambayo haijalelewa na kufundwa.

Katika mapambano haya makali, jeshi la akili, ufahamu na utashi havitoshi kuipatia kheri ushindi dhidi ya shari na uovu. Lau kama vitu hivyo vingekuwa vinatosha, Allah asingemuimarisha baba yetu Adam ؑ kwa kumpa utume na kumpatia siri za kimungu ili kwamba mwanadamu apate furaha na utukufu duniani na akhera. Kila wakati alikuwa akiwaongoza wanadamu kuelekea kwenye haki kupitia Mitume na *wahyi*



(ufunuo). Aliteremsha vitabu ili kuiimarisha akili na moyo, na akawalazimisha waja wake kuwa na malezi ya kiroho.


Akili ni kama upanga wenye pande mbili zenye ukali; inaweza kumpeleka mtu kwenye wema au uovu. Biandamu anaweza kufika kwenye daraja ya *'ahsanu taqwim'*, daraja ya juu kabisa, kwa kutumia akili. Lakini mara nyingi pia, kwa sababu ya akili, huporomoka mpaka kwenye daraja ya *'bal hum adhall'*, daraja ya chini kabisa inayokaribia kuwa sawa na mnyama katika upande wa utambuzi. Hivyo akili inatakiwa iwekwe chini ya nidhamu na utaratibu maalumu. Utaratibu huo si mwingine bali ni mafunzo na malezi ya ufunuo na muongozo wa Mitume. Akili, chini ya uangalizi wa ufunuo, humpeleka mwanadamu kwenye salama. Lakini kama akili ikinyimwa muongozo wa ufunuo huwa sababu ya mwanadamu kuingia katika mwisho mbaya.

Historia imishuhudia madhalimu wengi sana amba wali-kuwa katika kilele cha juu cha akili, lakini wakatenda mauaji na maangamizi ya kinyama na ya kutisha sana na hawakuhisi kujuta au kusikitika hata kidogo. Kwa sababu maovu waliyoyatenda waliyaona kuwa yalikuwa sahihi na kwamba yalikuwa katika kiwango cha juu kabisa cha akili. Kwa mfano, Hulagu Khan alipoingia Baghdad aliwazamisha katika maji yam to Tigris watu laki nne wasiokuwa na hatia, na hakuhi hata kidogo katika nafsi yake hatia ya uovu huo. Kabla ya Uislamu, wanaume wa Makkah walikuwa wakiwazika mabinti zao wakiwa hai katikati ya mayowe yao yenye ukimya yaliyozikata vipandevipande nyoyo za akina mama. Kumuuu mtumwa kwao ilikuwa sawa na kukata mti, na walifikia hatua ya kuona kuwa walikuwa na haki ya kufanya hivyo.



Watu hawa walikuwa na akili na hisia kama sisi, laki-ni walikuwa kama meno ya gurudumu yanayofanya kazi kinyume na uelekeo, na hivyo matokeo yake yanakuwa kinyume na matarajio.

Mifano hii yote inaonyesha wazi kuwa binadamu anahitajia muongozo na malezi kwa upande wa mapendeleo na raghba za chanya na hasi zilizomo ndani ya maumbile yake. Lakini sharti miongozo hiyo iendane na maumbile. Hilo linawezekana tu kwa njia yaw a mafunzo ya wahyi (ufunuo), yaani muongozo na mahubiri ya Mitume. Na pindi miongozo inapokuwa haiendani na maumbile yetu, huwa sababu ya uovu na mwisho mbaya.

Sifa yoyote ya kitabia inapomtawala mwanadamu hufuta kazi ya tabia hasimu. Kheri inapotawala, athari na nguvu ya shari hudhoofika na kutoweka. Na ubaya unapotawala huinyonga kheri na wema. Vita hivi ndani ya mwanadamu huendelea mpaka mwisho wa uhai wake. Ni kwa sababu hii kwamba Mwenyezi Mungu alimkirimu mwanadamu kwa kumletea Mitume na watu wema wawe muongozo na walimu kwake. Ni wale tu waliotelewa na mikono hii mahiri na nuru hizi zenye baraka ndio walioweza kugundua uzuri ulio ndani mwao, wakayageuza majira yao ya baridi kuwa majira yenye kuchipua na kuchanua. Kwa mfano, jamii katili ya zama za Ujahilia, iliyokuwa ikiwazika mabinti zao wakiwa hai ilibadilika na kuwa jamii iliyostaarabika na yenye kiwango cha juu cha utu, ustawi na maendeleo. Yote hayo yalipatikana kutokana na muongozo wa Mtume .

Sababu ni kwamba, binadamu wanaposhikamana na miongozo ya Mitume hubadilika na kuwa waja wanaoridhiwa na Mwenyezi Mungu, wanaostahiki kusifiwa. Ama wale



wanaoshindwa mtihani wa Mwenyezi Mungu uliopo katika mapambano ya nafsi na roho, hutumbukia katika shimo la watu wa chini kabisa. Na maisha ya dunia yameumbwa kwa ajili ya mwanadamu kufikia mojawapo kati ya malengo haya mawili. Mielekeo hasi au chanya iliyomo ndani mwake ndiyo itakayomuelekeza kwenye upande mmoja kati ya pande hizi mbili kwa utashi wake mwenyewe. Upande huo huamuliwa na matokeo yanayopatikana katika mapambano baina ya nafsi na roho. Lakini vita hivi vinapokamilika binadamu hubaki chini ya taathira nyingi.

Mwanadamu huzungukwa na hewa safi anapokuwa kati-bustani ya mawaridi. Lakini anapokuwa katika maeneo yanayonuka huchafuka kwa hewa mbaya. Ni kwa sabbau hii kwamba mwanadamu ni kiumbe anayehitajia sana muongozo na malezi kuliko viumbe vyote.

Hali ya mwanadamu kuangukia katika uovu unaoyapoteza maisha yake, inatokana na migongano mikali inayotoka ndani mwake. Sababu ya migongano hiyo ni kwamba, ndani ya mwanadamu kuna sifa na tabia njema za hali ya juu zinazomkurubisha kwa Mwenyezi Mungu. Lakini kwa upande mwingine kuna tabia chafu za kiahayawani zinazomuweka mbali na lengo lake hilo.

Kwa mtiririko huu, ulimwengu wa ndani ya wanadamu – ambao hawajapata mafunzo salama na nyoyo zao hazijatambua maana ya amani – ni kama pori lenye wanyama wa aina mbalimbali. Kila mmoja kati ya wanadamu ndani mwake amebeba tabia ya wanyama mbalimbali kulingana na mielekeo yake na sifa zake. Miongoni mwao kuna mjanja kama mbweha, huku mwingine akiwa katili kama fisi. Kuna waku-



sanyaji wenye pupa kama mduduchungu, na wengine wenye sumu kali kama nyoka. Wengine wanapuliza huku wanauma, na wengine wananyonya damu kaka konokono asiyekuwa na magamba. Kuna wale wanaokuchekea huku wakikuchimbia shimo. Kila mmoja kati ya hawa anabeba sifa zilizomo ndani ya wanyama mbalimbali.

Mtu ambaye hajaweza kujiokoa dhidi ya kutawaliwa na nafsi na matamanio kwa kutumia mafunzo na malezi ya kiroho na kutengeneza shakhsia salama, ataendelea kuwa ndani ya mzingo wa sifa duni. Wakati fulani mtu huweza kutawaliwa na sifa moja ya kihayawani, na wakati mwingine anaweza kutawaliwa na sifa nyingi za kihayawani. Pindi mwenendo wao unapoakisi picha zao inakuwa rahisi kwa wanaoelewa kuzigundua tabia zao zilizojificha. Tabia zao huwa kama kioo kinachokakisi ulimwengu wao wa ndani bila kudanganya hata kidogo.

Je mfumo wa Ukomunisti ulioasisiwa juu ya mafuvu ya vichwa vya wanga milioni ishirini, hauakisi moyo wa unyama? Na Mapiramidi ambayo pembezoni mwake walizikwa maelfu ya watu kwa ajili ya Firaun mmoja tu; hiyo sio kumbukumbu ya ukandamizaji na dhulma? Vitu hivi, kwa wale walioghafilika, huvichukulia kuwa ni kazi bora za kihistoria zenye kusababisha mshangao ndani ya akili zao. Lakini vitu hivi vinapotathiminiwa kwa mtazamo wa haki na ukweli; je havionekani kama ubao wa ukatili unaowatisha hata madhalimu na wakandamizaji wa hali ya juu?


Yote haya yanaonyesha kuwa, iwapo watu wenye sifa za chura wataitawala jamii fulani wataibadilisha kuwa madimbwi yao. Na lau kama itatawaliwa na watu wenye roho za nyoka, basi umma wote utangiwa na sumu ya hayo majoka





na kuanza fujo, vurugu na vitisho. Lakini iwapo jamii hiyo itatwaliwa na watu wenye tabia za mawaridi, basi jamii husika itabadilika na kuwa bustani na watu watapata furaha, utulivu na amani ya kweli.

Kwa sababu hii binadamu hana budi kupata malezi ya *wahyi*, kwa sababu wale wanaojitenga na malezi haya, hata kama hawatofanya maovu na unyama tulioutaja bado kila mara watafanya mambo yatakayowapelekea kuwa na sifa za unyama, hata kama kwa nje watonyesha mienendo mizuri. Hivyo, uzuri wote unaotoka nje ya malezi na mafunzo ya kimungu ni uzuri wa muda tu. Kwa sababu mielekeo yote isiyokuwa sawa pamoja na maovu yote ya wale wasiokuwa na malezi ya hali ya juu hujitokeza haraka sana hususan katika nyakati ngumu na wakati wa kuibuka kwa raghba zao za kimatamania. Kwa sababu nafsi ambayo haikupata malezi ni kama paka mwenye uchu na pupa ya panya. Anapowekewa chakula kitamu mbele yake na ghafla akamuona panya, ataa-cha vyakula vyake hivyo vitamu na ataanza kumfukuza ili amkamate. Hivyo, iwapo mwanadamu hatalelewa kwa vipimo vya Kimungu basi nafsi yake inayofafanana na paka inaufanya moyo wake – hata kama atakuwa na mazuri mengi – ukimbie nyuma ya kila panya anayemuona na hatimaye ataangamia.

Tunapowatazama Firaun na Namrud tunaona kwamba walifanya mauaji ya watu wengi bila haki kwa ajili ya kuzishibisha raghba zao zilizokuwa zikimfukuza panya. Wakati tunakuta kuwa malezi ya Kimungu yanatuamrisha kutetemeka mbele ya haki ndogo ya mtumwa kama moto wa mshumaa unavyotetemeka kutokana na upepo, achilia mbali kuua mtu bila ya haki! Hata Mtume  alikataza kukata tawi la mti



mbichi. Na alipokuwa akielekea Makka alilielekeza jeshi lipite njia tofauti ili kutomsumbua na kumkhofisha mbwa jike aliyekuwa akinyonyesha vitoto vyake.

Sehemu nyingine Mtume 🕌 alishikwa na mshituko alipoona mapango ya waduduchungu yamechomwa moto akauliza hali ya kuwa ameuumizwa na tukio hilo: “**Nani aliyefanya jambo hili?**”

Ni kwa namna hiyo kwamba watawala wa dola ya Othmaniya – ambao walichukua moyo huo huo – walianzisha *waqf* nyingi zilizofikia kilele cha juu katika kuhudumia watu au kuwahurumia viumbe wote. Kutokana na huruma waliyoyifunza kwa Mtume 🕌 walifikia hatua ya kuanzisha *waqf* mbalimbali zinazoshughulika na afya na siha ya wanyama. Miongoni mwa mambo yanayoonyesha huruma hiyo ambayo inaelezewa pia na wageni mbalimbali waliokuwa wakija katika dola ya Othmania ni kuwa, paka na mbwa katika makazi ya Waislamu walikuwa wakiwazunguka watu bila khofu, wakati katika maeneo mengine wanyama hao walikuwa wakijificha mara wanapowaona watu.

Mifano ilityotangulia ni vielelezo vya mwanadamu aliye-pata malezi na mwanadamu ambaye hajapata malezi. Yule anayemwaga damu na kuinyweshwa ardhi kwa damu hiyo ni mwanadamu, na yule anayejitolea damu yake kwa wanaoihitaji na kuwapatia mawaridi naye pia ni mwanadamu.

Hekma iliyoje kwa watu wenye tabia tofauti kuishi pamoja katika sehemu moja. Tukitoa mfano, tunaweza kusema kuwa jambo hili ni mfano wa adhabu anayoivumilia nsha dhaifu katika zizi la wanyama wakubwa wakali na wenye kutisha.



Wakati fulani bakhili huishi pembezoni mwa mtu karimu, na mpumbavu akaishi pamoja na mjuzi, na mpole akaishi na mtu mwenye huruma. Ama mtu karimu ni mwenye huruma, unyenyekevu na mwenye kuwahudumuia watu wengine. Na mpumbavu hamfahamu mjuzi. Dhalimu hudhani kuwa analofanya ni haki na hutumia nguvu dhidi ya wale wanaomzunguka. Yaani wale wenye nyoyo ngumu wanapoishi na watu wenye sifa za kimalaika pamoja katika maisha. Wakati mmoja wao anapoishi ili kumtambua Mwenyezi Mungu na kuwa mja wake mtiifu na kufanya juhudi ya kumfikia Mungu, tunamuona mwingine akidhani kuwa furaha ni yeye kuishi akiwa mfuasi wa tabia za watu wenye tabia duni kabisa, kiasi kwamba maisha yao wameyafanya kuwa na lengo la kupupia chakula, matamano ya kimwili, vyeo na mambo kadhaa wa kadhaa yenye kuondoka.

Kwa hakika ni mtihani mgumu sana kuishi katika dunia yenye watu wenye sifa zinazokinzana. Lakini mwanadamu lazima auvuke mtihani huu. Kwa sababu lengo la asili la mwanadamu ni kuishinda mitihani ya dunia na kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu. Na kwa ajili hiyo, mwanadamu analazimika kuzivua sifa mbaya na ajipambe kwa sifa njema zitakazomfanya aishi maisha yenye utukufu na heshima ya kibnadamu.

Mwanadamu ambaye ana asili ya mbinguni kwa upande wa roho yake, ameumbwa kwa udongo kwa upande wa mwili wake. Kwa sababu hiyo, roho yake itakaporudi mbinguni mwili wake utarudi mavumbini. Na kwa upande wa mwili wake amebeba sifa za viumbe wengine, na kwa hiyo ni lazima kwake ajitahidi katika kupatia nafsi yake malezi ya kiroho, aitakase, ayadhibiti matamano yake, na ailishe na kuiimari-



sha roho yake. Iwapo hali itakuwa kinyume na hivyo atashindwa na shetani kwa upande wa nje na matamania ya nafsi kwa upande wa ndani. Hapo nguvu ya roho hudhoofika. Aya tukufu inalizungumzia jambo hilo ikisema:

*“Na kwa nafsi na kwa aliye itengeneza. Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake. Hakika amefanikiwa aliye itakasa. Na hakika amekhasiri aliye iviza”.* (as – Shams: 7 – 10)

Mawlana Rumi anafafanua uovu na wema uliomo ndani ya ulimwengu wa mwanadamu na ambao umetajwa katika aya hiyo, katika namna ifuatayo:

*“Ewe unayepambana katika njia ya Mwenyezi Mungu, ukitaka kujua ukweli tambua kuwa Musa na Firaun hawajafa, bali wako hai wanaishi mpaka leo ndani mwako. Lakini wamejificha na wanaendelea kupambana ndani ya moyo wako. Hivyo unatakiwa kuwatafuta mahasimu hawa wawili ndani ya nafsi yako!”*

Anaendelea kusema:

*“Na usitazame tu kuulisha mwili wako kupita kiasi, kwa sababu mwishoni mwili huo utatolewa kama kafara ya udongo. Bali angalia katika kuustawisha moyo wako kwa sababu utapata heshima ya kwenda katika ulimwengu wa juu. Ulishe mwili wako kwa vitu vitamu na vyenye mafuta kidogo, kwani yule anayeulisha mwili wake kuzidi kiwango kinachotakiwa mwishoni ataangukia katika matamania ya nafsi na kuwa dhalili na kuaibika.*

*Istawishe roho yako kwa virutubisho vya kiroho. Fikiria yale yanaoendana na roho ili iweze kusafiri kwa nguvu kali katika safari yake”.*



# YALIYOMO

Utangulizi ..... 7

## SEHEMU YA KWANZA / 13

Shahsiah Ya Kipekee Iliyokamilika:

Mtume Muhammad Mustafa 齋 ..... 15

Uswatul-Hasanah / Mfano Bora Uliokamilika..... 26

## SEHEMU YA PILI / 39

Tabia Za Hali Ya Juu Za Mtume Wa Allah 齋..... 41

Uzuri Wa Sura, Umbile Na Tabia Za Mtume 齋..... 42

Unyenyekevu Wa Mtume 齋..... 48

Ukarimu Wa Mtume 齋..... 51

Uchamungu Wa Mtume 齋 ..... 53

Zuhdi ya Mtume 齋..... 56

Ulaini Wa Moyo Wa Mtume 齋..... 58






Adabu Na Hayaa Za Mtume 齋 ..... 62

Ushujaa Wa Mtume 齋..... 64





Upole Wa Mtume 齋 ..... 66

Mtume 齋 Mwenye Kusamehe..... 71



Mtume  Na Kuchunga Haki Za Jirani.....	75
Mtume  Na Mateka Wa Vita Na Watumishi.....	79
Muamala Wa Mtume  Kwa Wanawake.....	84
Muamala Wa Mtume  Kwa Yatima.....	89
Mtume  Na Wanyama .....	91
Viwango Vya Juu Kama Nyota .....	97


### SEHEMU YA TATU / 101


Usafi Wa Moyo Katika Kumfuata Mtume  .....	103
Kumfuata Mtume  Kwa Kumpenda .....	106
Kioo Cha Upendo Na Maadili Yake: Asrus-Saadah.....	110
Tungo Zenye Mguso Katika Kumpenda Mtume  .....	116
Upendo Wa Maswahaba Kwa Mtume  .....	121
Chemchem Ya Upendo Baada Ya Maswahaba.....	133
Salawat'us – Sharifah.....	145

### SEHEMU YA NNE / 151


Hitajio Kuu La Moyo Na Akili: Shakhshia Ya Kielelezo Malezi Yanayomtengeneza Mwanadamu: Mafundisho Ya Kimungu .....	153
---	-----











# FOR FREE IN PDF FORMAT

# ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT  
**1350 BOOKS IN 60 LANGUAGES** FOR FREE



Islamic books in different languages are waiting  
for you in PDF format at the web site  
[www.islamicpublishing.org](http://www.islamicpublishing.org)